**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24

**MACHI, 2023**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ASA | Agricultural Seed Agency |
| ASDP II | Agriculture Sector Development Programme II |
| ATC | Arusha Technical College |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited |
| ATMIS | Agriculture Trade Management Information System |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency |
| BTI | Beekeeping Training Institute |
| BTIP II | Backbone Transmission Investment Project - II |
| CAMARTEC | Centre For Agriculture Mechanization and Rural Technology |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation |
| COSTECH | Tanzania Commission for Science and Technology |
| CPB | Cereals and Other Produce Board |
| DCF | Development Cooperation Framework |
| DIT | Dar es Salaam Institute of Technology |
| DITF | Dar es Salaam International Trade Fair |
| DMDP | Dar es Salaam Metropolitan Development Project |
| DMI | Dar es Salaam Maritime Institute |
| DUCE | Dar es Salaam University College of Education |
| EAC | East Africa Community |
| EACOP | East Africa Crude Oil Project |
| e-GA | Electronic Government Authority |
| e-HRP | Electronic Human Resource Planning |
| EIA | Environment Impact Assessment |
| e-OPRAS | Electronic Open Performance Review and Appraisal System |
| EP4R | Education Program 4 Result |
| ESIA | Environment and Social Impact Assessment |
| ETH | Engineering Technology Hubs |
| FETA | Fisheries Education Training Agency |
| FORVAC | Forestry and Value Chain Development Programme |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| GST | Geological Survey of Tanzania |
| HCMIS | Human Capital Management Information System |
| HESLB | Higher Education Students’ Loans Board |
| HGA | Host Government Agreement |
| IDRAS | Integrated Domestic Revenue Administration System |
| IJA | Institute of Judicial Administration |
| IMF | International Monetary Fund |
| ISTA | International Seed Testing Agency |
| JNIA | Julius Nyerere International Airport |
| KIA | Kilimanjaro International Airport |

| | |
|---|---|
| LITA | Livestock Training Agency |
| LNG | Liquefied Natural Gas |
| LSP II | Legislative Support Project II |
| MMEM | Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi |
| MSD | Medical Stores Department |
| MSM | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MTAKUWWA | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto |
| MTDS | Medium Term Debt Strategy |
| MUCE | Mkwawa University College of Education |
| MUSE | Mfumo wa Ulipaji Serikalini |
| MUST | Mbeya University of Science and Technology |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NFRA | National Food Reserve Agency |
| NIDC | National Internet Data Centre |
| NIT | National Institute of Transport |
| NPMIS | National Project Management Information System |
| OECD | Organization for Economic Co-operation and Development |
| OSC | One Stop Centre |
| PFMRP | Public Financial Management Reform Programme |
| PPP | Public-Private Partnership |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| REA | Rural Energy Agency |
| REGROW | Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth |
| SELF | Small Entrepreneurs Loan Facility |
| SEZ/EPZ | Special Economic Zone/Export Processing Zone |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SMMRP | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| STAMICO | State Mining Company |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| SWIOFish | South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth |
| TADB | Tanzania Agricultural Development Bank |
| TAEC | Tanzania Atomic Energy Commission |
| TAFICO | Tanzania Fisheries Corporation |
| TAFIRI | Tanzania Fisheries Research Institute |
| TALIRI | Tanzania Livestock Research Institute |
| TAMCO | Tanzania Automobiles Manufacturing Company |
| TANESCO | Tanzania Electrical Supply Company |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute |
| TATC | Tanzania Automotive Technology Centre |
| TBC | Tanzania Broadcasting Cooperation |

| | |
|---|---|
| TBS | Tanzania Bureau of Standard |
| TCRA | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| TDCs | Technology Development Centres |
| TEA | Tanzania Education Authority |
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| TESP | Teacher Education Support Project |
| TGC | Tanzania Gemmological Centre |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization |
| TOSCI | Tanzania Official Seed Certification |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation |
| TTCL | Tanzania Telecommunications Corporation, |
| UTT - AMIS | Unit Trust of Tanzania- Asset Management and Investor Services |
| UVIKO-19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona - 19 |

## YALIYOMO


MUHTASARI ..... 1

SURA YA KWANZA ..... 3
HALI YA UCHUMI ..... 3
1.1. Utangulizi ..... 3
1.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi Kikanda na Kimataifa ..... 3
1.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia ..... 3
1.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea ..... 3
1.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ..... 3
1.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ..... 3
1.2.5. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ..... 4
1.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa ..... 5
1.3.1. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi ..... 5
1.3.2. Mfumuko wa Bei ..... 5
1.3.3. Sekta ya Nje ..... 8
1.3.4. Sekta ya Fedha ..... 9
1.3.5. Deni la Serikali ..... 14
1.4. Maendeleo ya Watu ..... 16
1.4.1. Ongezeko la Idadi ya Watu mwaka 2022 ..... 16
1.4.2. Viashiria vya Maendeleo ya Watu ..... 16
1.4.2.1. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ..... 17
1.4.2.2. Upatikanaji wa Chakula ..... 17

SURA YA PILI ..... 18
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO ..... 18
2.1. Utangulizi ..... 18
2.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2022/23 ..... 18
2.3. Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ..... 19
2.3.1. Miradi ya Kielelezo ..... 19
2.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ..... 21
2.3.2.1. Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma ..... 21
2.3.2.2. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi ..... 33
2.3.2.3. Mapinduzi ya TEHAMA ..... 39
2.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma ..... 41
2.3.3.1. Uzalishaji Viwandani ..... 42
2.3.3.2. Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II ..... 45
2.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia ..... 54
2.3.3.4. Huduma ..... 55
2.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji ..... 61
2.3.4.1. Huduma za Biashara na Masoko ..... 61

2.3.4.2. Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji ..... 62
2.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu ..... 63
2.3.5.1. Afya ..... 63
2.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii ..... 70
2.3.5.3. Elimu ..... 72
2.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ..... 79
2.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ..... 80
2.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ..... 83
2.3.5.7. Usimamizi wa Maafa Nchini ..... 85
2.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu ..... 86
2.3.6.1. Ujuzi na Uwezeshaji ..... 86
2.3.7. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma ..... 87
2.3.8. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ..... 87
2.4. Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo ..... 88
2.4.1. Ufuatiliaji wa Miradi katika kipindi cha Mwaka 2022/23 ..... 88
2.4.2. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23 ..... 89
2.4.3. Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto ..... 90

SURA YA TATU ..... 92
MIRADI YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2023/24 ..... 92
3.1. Utangulizi ..... 92
3.2. Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ..... 92
3.2.1. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ..... 92
3.2.2. Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2023/24 ..... 92
3.3. Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2023/24 ..... 93
3.3.1. Miradi ya Kielelezo ..... 93
3.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ..... 96
3.3.2.1. Kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji ..... 96
3.3.2.2. Mapinduzi ya TEHAMA ..... 113
3.3.2.3. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi ..... 115
3.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma ..... 124
3.3.3.1. Uzalishaji Viwandani ..... 124
3.3.3.2. Kilimo, Mifugo na Uvuvi ..... 127
3.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia ..... 135
3.3.3.4. Huduma ..... 135
3.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji ..... 139
3.3.4.1. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji ..... 140
3.3.4.2. Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ..... 140
3.3.4.3. Kukuza Sekta Binafsi ..... 140
3.3.4.4. Huduma za Biashara na Masoko ..... 141
3.3.4.5. Mahusiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia ..... 142

3.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu ........ 143
3.3.5.1. Afya ........ 143
3.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii ........ 147
3.3.5.3. Elimu ........ 148
3.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ........ 156
3.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ........ 157
3.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ........ 159
3.3.5.7. Hifadhi na Kinga ya Jamii ........ 162
3.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu ........ 163
3.3.6.1. Ujuzi na Uwezeshaji ........ 163
3.3.7. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ........ 164
3.3.8. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma ........ 165

SURA YA NNE ........ 166
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2023/24 ........ 166
4.1. Utangulizi ........ 166
4.2. Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2023/24 ........ 166
4.3. Mikakati ya Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Mpango kwa Mwaka 2023/24166
4.4. Mapato ya Ndani ........ 166
4.4.1. Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi ........ 166
4.5. Mikopo na Misaada ........ 167
4.5.1. Mikopo ya Nje ........ 167
4.5.2. Mikopo ya Ndani ........ 168
4.5.3. Misaada ya Nje ........ 168
4.6. Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo ........ 168

SURA YA TANO ........ 170
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ........ 170
5.1. Utangulizi ........ 170
5.2. Misingi na Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini ........ 170
5.3. Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini ........ 171
5.4. Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini ........ 171
5.5. Mgawanyo wa Majukumu ........ 171

SURA YA SITA ........ 172
VIHATARISHI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO ........ 172
6.1. Utangulizi ........ 172
6.2. Vihatarishi vya Ndani na Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo ........ 172

## MUHTASARI

Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Mpango huo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayotekelezwa kupitia Mpango Elekezi wa Muda Mrefu, 2011/12 – 2025/26. Mpango huu ni muhimu katika kuainisha maeneo mahsusi ya vipaumbele kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2023/24.

Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 yanajumuisha: Malengo na shabaha za Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24; maeneo mahsusi ya vipaumbele yaliyozingatia vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; mfumo wa ugharamiaji wa Mpango; wajibu wa sekta ya umma na binafsi na mgawanyo wa majukumu; na mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango.

Aidha, Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 yameandaliwa kwa mujibu wa matakwa ya Ibara ya 63 (3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Sheria ya Bajeti, Sura 439. Maandalizi ya Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 yamezingatia nyaraka za kisera za kitaifa, kikanda na kimataifa ambazo ni: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC) 2050; Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi wameshirikishwa katika Mchakato wa Maandalizi ya Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24. Vile vile, Washirika wa Maendeleo wameshirikishwa kupitia majadiliano katika maeneo mahsusi ya ushirikiano, ufadhili wa miradi ya maendeleo na programu za kisekta.

Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, Mwenendo wa uchumi wa Taifa umeendelea kuimarika ambapo Pato la Taifa katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022 lilikua kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, nakisi ya urari ilifikia dola za Marekani milioni 5,261.3 kwa mwaka ulioishia Januari 2023, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni

2,659.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kufikia asilimia 22.5 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 10 mwaka 2021 sambamba na kupungua kwa viwango vya riba za mikopo kutoka asilimia 16.59 mwaka 2021 hadi asilimia 16.18 mwaka 2022. Hata hivyo, mfumuko wa bei nchini umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021 kufikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022 kutokana na changamoto ya mlipuko wa UVIKO – 19 na athari za vita ya Urusi na Ukraine.

Kwa ujumla Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 yamejumuisha utekelezaji wa miradi miradi ya maendeleo kwa kipindi cha kwa mwaka 2022/23 na miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2023/24. Aidha, utekelezaji wa Mpango kwa mwaka 2023/24 utaendelea kutoa kipaumbele kwa miradi ya kielelezo na kimkakati ikiwemo: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge); Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; makaa ya Mawe (Mchuchuma - Njombe) na Chuma (Liganga - Njombe); na kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) – Njombe.

Katika kipindi cha Juali - Desemba 2022, Wizara ya Fedha na mipango ilifuatilia miradi na programu za maendeleo 112 ikijumuisha miradi ya kielelezo na kimkakati katika maeneo mbalimbali nchini. Ufuatiliaji huo ulibaini hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi, mafanikio, changamoto na mapendekezo. Ufuatiliaji na Tathmini uliwezesha kutolewa kwa maamuzi yanayoongozwa na taarifa sahihi na kwa wakati. Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua za haraka katika kukabiliana na vihatarishi vitakavyojitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hatua hizo zinajumuisha kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira ili kudhibiti uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu, kuendelea kufuatilia kwa karibu mfumuko wa bei ya bidhaa za chakula ili kutoa ruzuku ya mbolea itakayoongeza uzalishaji pamoja na kutoa ruzuku katika bidhaa za mafuta.

Kitabu cha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 kimegawanyika katika sura sita (6): Sura ya kwanza (1) ni mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya pili (2) ni mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/23 katika kipindi cha nusu mwaka ni; Sura ya tatu (3) inaelezea miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2023/24; Sura ya nne (4) ni ugharamiaji wa Mpango; Sura ya tano (5) inaainisha utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango; na Sura ya sita (6) inaainisha vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na namna ya kukabiliana navyo.

# SURA YA KWANZA

# HALI YA UCHUMI

## 1.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi nchini, kikanda na dunia kwa mwaka 2022 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2023. Mwenendo wa viashiria hivyo unajenga msingi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Kwa ujumla, mwenendo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2022 umepungua ukilinganisha na ukuaji katika kipindi cha mwaka 2021.

## 1.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi Kikanda na Kimataifa

### 1.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya January, 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutoka asilimia 6.2 mwaka 2021 na kufikia asilimia 3.4 mwaka 2022. Aidha, uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 2.9 mwaka 2023 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa China na Urusi, madhara ya janga la UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine na sera za kupunguza ukwasi katika chumi za Ulaya ili kukabiliana na mfumuko wa bei.

### 1.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea imepungua na kufikia asilimia 2.7 mwaka 2022 kutoka asilimia 5.4 mwaka 2021. Aidha, uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kupungua na kufikia ukuaji wa asilimia 1.2 mwaka 2023. Upungufu huu umesababishwa na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine inayoendelea kuyumbisha uchumi wa dunia hususan kuongezeka kwa gharama za maisha kulikosababishwa na mfumuko wa bei za nishati barani Ulaya na kuongezeka kwa bei za vyakula katika soko la dunia.

### 1.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ulipungua na kufikia asilimia 3.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2021. Hii ilitokana na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine ambayo imeendelea kuathiri uchumi wa nchi hizi. Aidha, uchumi katika Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi Barani Asia, ikijumuisha China na India ulipungua na kufikia ukuaji wa asilimia 4.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2021.

### 1.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2021. Upungufu huo ulitokana na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine iliyosababisha mfumuko wa bei za nishati ya mafuta na vyakula. **Jedwali Na. 1.1** linaonesha

mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia na matarajio.

**Jedwali Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Matarajio**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (asilimia) | | | | | Matarajio (asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Dunia | 3.8 | 3.5 | 2.8 | -3.1 | 6.2 | 3.4 | 2.9 |
| Nchi Zilizoendelea | 2.4 | 2.2 | 1.7 | -4.5 | 5.4 | 2.7 | 1.2 |
| Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia | 4.8 | 4.5 | 3.7 | -2.0 | 6.7 | 3.9 | 4.0 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 2.9 | 3.3 | 3.1 | -1.6 | 4.7 | 3.8 | 3.8 |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO), Januari,2023*

### 1.2.5. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Kiwango cha wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2022 kwa nchi nyingi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ni asilimia 4.0 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2021. Aidha, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afirka Mashairiki **(**EAC) ulikuwa ni asilimia 5.6 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2021 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1.2**. Uzalishaji na shughuli nyingine za kiuchumi katika nchi husika ulishuka kwa kiwango kikubwa mwaka 2020 kufuatia utekelezaji wa mikakati/masharti yaliyowekwa kuzuia maambukizi ya UVIKO-19 ikiwemo kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za kimataifa, kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi zinazohusisha mikusanyiko na kuzuia watu kutoka nje. Baada ya masharti hayo kuondolewa, nchi hizo zilirudi kwenye shughuli za kawaida za kiuchumi.

**Jedwali Na. 1.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

| **Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za SADC** | | | |
|---|---|---|---|
| **Nchi** | **2020** | **2021** | **2022** |
| Angola | -5.4 | 0.7 | 2.9 |
| Botswana | -8.7 | 12.5 | 4.2 |
| Comoros | 0.2 | 1.9 | 2.8 |
| Tanzania | 4.8 | 4.9 | 5.2* |
| DRC | 1.7 | 4.5 | 6.6 |
| Eswatin | -3.2 | 1.4 | 0.7 |
| Lesotho | -6 | 3.0 | 2.5 |
| Madagascar | -4.0 | 3.5 | 4.5 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Malawi | -1.7 | 3.3 | 6.2 |
| Mauritius | -15.0 | 3.9 | 6.7 |
| Msumbiji | -1.2 | 2.2 | 3.6* |
| Namibia | -8.5 | 0.9 | 3.3 |
| Seychelles | -7.7 | 8 | 5.9 |
| Zambia | -2.8 | 4.3 | 5.3* |
| Zimbabwe | -5.3 | 6.3 | 3.5 |
| Afrika ya Kusini | -6.4 | 4.9 | 1.6* |
| **Wastani** | **-4.3** | **4.2** | **4.0** |
| **Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za EAC** | | | |
| Burundi | 0.3 | 2.4 | 3.6 |
| Kenya | -0.3 | 7.2 | 4.7* |
| Rwanda | -3.4 | 10.2 | 10.0* |
| DRC | 1.7 | 4.5 | 6.6 |
| Sudani Kusini | -6.6 | 5.3 | 6.5 |
| Tanzania | 4.8 | 4.9 | 5.2* |
| Uganda | -1.4 | 5.1 | 7.5* |
| **Wastani** | **-0.7** | **5.7** | **5.6** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ya Shirikua la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Januari 2023, Taarifa ya Mwenendo wa Uchumi ya Benki ya Maendeleo ya Afrika na Ofisi za Takwimu za Nchi husika*

** Inamaanisha Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Kipindi cha Januari hadi Septemba kwa Mwaka husika*

## 1.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 1.3.1. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022, Uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji chanya wa uchumi ulichangiwa na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo: mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi; uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe na kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi. Aidha, ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za utalii kutokana na kampeni ya *Royal Tour*. Ukuaji huu wa uchumi unaashiria kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa ajira na mapato ya ndani.

### 1.3.2. Mfumuko wa Bei

Vita vya Urusi na Ukraine vimesababisha kupanda zaidi kwa bei ya mafuta duniani, ambayo yamechangia ongezeko la bei ya uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa. Aidha,

upandaji wa bei ya mafuta umekuwa na ongezeko la bei ya bidhaa zingine ikiwa ni pamoja na kupanda kwa viwango vya riba katika shughuli za kibenki.


**(a) Mfumuko wa Bei Nchini**

Mfumuko wa bei nchini ulifikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021. Hata hivyo, kiwango hiki kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Sababu zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika kipindi husika ni pamoja na: kupanda kwa bei za bidhaa (mafuta ya kula, mbolea na petroli) kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia uliotokana na athari za vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula nchini na nchi jirani kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

Katika kipindi cha mwaka 2022, wastani wa mfumuko wa bei wa vyakula na vinywaji baridi umeongezeka hadi asilimia 7.3 kutoka asilimia 4.2 mwaka 2021. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula na nishati *(Core Inflation)* ulifikia wastani wa asilimia 3.0 katika kipindi cha mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.1 katika kipindi cha mwaka 2021 **(Kielelezo Na. 1.3)**. Kushuka kwa kasi ya bei ya baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula na nishati ikiwemo saruji kumetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizi nchini.

Kwa upande mwingine mfumuko wa bei wa nishati, mafuta na bili za maji umeongezeka kutoka asilimia 3.1 mwaka 2021 na kufikia asilimia 9.1 mwaka 2022. Kuongezeka huko kumetokana na kuongezeka kwa bei ya nishati ya mafuta katika soko la dunia iliyotokana na vita nchini Ukraine. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha bei ya nishati ni stahimilifu ikiwepo utoaji wa ruzuku.

**Kielelezo Na. 1.3: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini Katika Kipindi cha Mwaka 2019 na 2022**




***Chanzo***: *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

**(b) Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki**

Mfumuko wa Bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifikia wastani wa asilimia 9.2 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2021. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa chakula kwa baadhi ya nchi wanachama na kuongezeka kwa gharama na mahitaji ya mafuta katika nchi hizi. Sababu nyingine ni pamoja na vita vya mara kwa mara katika nchi za Sudani Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, kwa wastani, viwango vya mfumuko wa bei kwa nchi ya Tanzania, Kenya na Uganda ndivyo pekee viliendelea kuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko usiozidi asilimia 8 kwa mwaka. Kiwango hiki pia kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2021 na kufikia asilimia 6.4 mwaka 2022. Kwa upande mwingine, nchi za Burundi na Rwanda ndizo zilikuwa na viwango vikubwa vya mfumuko wa bei mwaka 2022 uliofikia asilimia 18.8 na 13.2 mtawalia. **Jedwali Na. 1.3** linaonesha mfumuko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2021 na 2022.

**Jedwali Na. 1.3: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Januari 2021 hadi Disemba 2022**

| Nchi/Mwaka/ Mwezi | | Jan | Feb | Machi | Aprili | Mei | Juni | Julai | Agosti | Sept | Oktoba | Nov | Disemba | Wastani Kwa Mwaka |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tanzania | 2021 | 3.5 | 3.3 | 3.2 | 3.3 | 3.3 | 3.6 | 3.8 | 3.8 | 4.0 | 4.0 | 4.1 | 4.2 | 3.7 |
| | 2022 | 4.0 | 3.7 | 3.6 | 3.8 | 4.0 | 4.4 | 4.5 | 4.6 | 4.8 | 4.9 | 4.9 | 4.8 | 4.3 |
| Kenya | 2021 | 5.7 | 5.8 | 5.9 | 5.8 | 5.9 | 6.3 | 6.6 | 6.6 | 6.9 | 6.5 | 5.8 | 5.7 | 6.1 |
| | 2022 | 5.4 | 5.1 | 5.6 | 6.5 | 7.1 | 7.9 | 8.3 | 8.5 | 9.2 | 9.6 | 9.5 | 9.1 | 7.7 |
| Uganda | 2021 | 2.0 | 2.3 | 2.7 | 2.1 | 1.9 | 2.0 | 2.1 | 1.9 | 2.2 | 1.9 | 2.6 | 2.9 | 2.2 |
| | 2022 | 2.7 | 3.2 | 3.7 | 4.9 | 6.3 | 6.8 | 7.9 | 9.0 | 10.0 | 10.7 | 10.6 | 10.2 | 7.2 |
| Rwanda | 2021 | 3.5 | 2.2 | 3.9 | 2.7 | 0.4 | 0.1 | -1.1 | -1.8 | -3.2 | -3.3 | -3.4 | -2.0 | -0.2 |
| | 2022 | 4.3 | 5.8 | 7.5 | 9.9 | 12.6 | 13.7 | 15.6 | 15.9 | 17.6 | 20.1 | 21.7 | 21.6 | 13.2 |
| Burundi | 2021 | 7.6 | 7.5 | 7.5 | 7.4 | 7.0 | 7.1 | 7.3 | 10.5 | 10.5 | 9.9 | 8.6 | 10.1 | 8.4 |
| | 2022 | 12.3 | 13.3 | 12.8 | 16.1 | 18.6 | 17.6 | 19.1 | 19.6 | 20.9 | 22.0 | 26.8 | 26.6 | 18.8 |
| Sudani ya Kusini | 2021 | | 18.3 | 18.96 | | | 18.3 | | | | | | -8.5 | 11.8 |
| | 2022 | | | | -4.29 | | | 6.43 | -2.50 | | | | -11.57 | -3.0 |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 2021 | 6.23 | 4.92 | 4.3 | 4.1 | 4.35 | 4.37 | 4.4 | 4.1 | 3.94 | 3.9 | 4.0 | 4.2 | 4.4 |
| | 2022 | 4.16 | 5.51 | 5.94 | 7.07 | 7.26 | 8.4 | 9.0 | 9.99 | 11.38 | 12.19 | 12.88 | | 8.5 |
| **Wastani wa EAC Kwa Mwezi na Mwaka** | 2021 | 4.8 | 6.3 | 6.6 | 4.2 | 3.8 | 6.0 | **3.8** | 4.2 | 4.1 | 3.8 | 3.6 | 2.4 | 4.5 |
| | 2022 | 5.48 | 5.85 | 6.23 | 5.94 | 8.86 | 9.62 | **9.9** | 9.3 | 12.0 | 12.8 | 14.1 | 10.1 | 9.2 |

**Chanzo**: *Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi Husika*

### 1.3.3. Sekta ya Nje

Sekta ya nje imeendelea kukabiliwa na changamoto zitokanazo na vita kati nchi ya Ukraine na Urusi pamoja na kuibuka kwa maambukizi mapya ya UVIKO-19. Hali hii imesababisha usumbufu wa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma duniani na hivyo kupekelea kupanda kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali katika soko la dunia.

### (a) Urari wa Malipo ya Kawaida

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ilikuwa dola za Marekani milioni 5,261.3 kwa mwaka ulioishia Januari 2023, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,659.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ilitokana na ongezeko la gharama ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kufuatia kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

### (b) Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 7,377.4 kwa mwaka ulioishia Januari 2023, kutoka dola za Marekani milioni 6,752.5 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Mauzo ya bidhaa zisizo asilia yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 6,216.1 kilinganishwa dola za Marekani milioni 5,721.8 mwaka 2022. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, almasi na bidhaa za viwandani hususan chuma, mbolea na sementi. Aidha, mauzo ya dhahabu nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 2,904.0 mwaka 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,649.7 mwaka 2022, hali

iliyochangiwa zaidi na kuongezeka kwa bei katika soko la dunia. Mauzo ya bidhaa asilia yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 754.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 657.8 mwaka 2022. Katika kipindi hiki, mauzo ya bidhaa asilia zote yaliongezeka isipokuwa karafuu na chai.

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 14,299.9 kwa mwaka ulioishia Januari 2023 kutoka dola za Marekani milioni 10,315.8 kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa gharama ya uagizaji wa bidhaa za petroli kutoka nje kufuatia kuongezeka kwa bei katika soko la dunia. Bidhaa za petroli zilichangia asilimia 23.3 ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 19.6 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Ongezeko la bidhaa za petroli lilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia. Vilevile, ongezeko la thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi lilichangiwa pia na uagizaji wa mashine, vyombo vya usafiri pamoja na bidhaa za viwandani kama mbolea, plastiki na chuma; sanjari na ukuaji wa shughuli za uchumi nchini.

Mauzo ya huduma nje ya nchi yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 4,881.4 kwa mwaka ulioishia Januari 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,229.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii na usafirishaji. Mapato ya utalii yaliongezeka kwa takribani mara mbili hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,560.7 sambamba na kuongezeka kwa idadi ya watalii hadi kufikia 1,454,920 kutoka watalii 922,692. Ongezeko hili lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na hatua mbali mbali ambazo serikali imechukua katika kuboresha sekta ya utalii nchini.

Malipo ya huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa takribani mara mbili hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,530.9 kwa mwaka ulioishia Januari 2023 kutoka milioni 1,671.1 kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya huduma za usafirishaji sambamba na ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

**(c) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa katika viwango toshelezi, kufikia dola za Marekani milioni 5,177.2 mwezi Desemba 2022, kiasi ambacho kinatosheleza kuagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa miezi 4.7. Kiwango hiki ni ndani ya lengo la nchi la miezi isiyopungua minne na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza angalau miezi minne na nusu.

**1.3.4. Sekta ya Fedha**

**(a) Mwenendo wa Viwango vya Riba**

Katika mwaka 2022, riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki ilikuwa

chini na tulivu japokuwa wastani uliongezeka kidogo hadi asilimia 4.53 kutoka asilimia 4.44 mwaka 2021. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi zimeendelea kubaki katika wastani wa asilimia 4. Kwa upande mwingine, viwango vya riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi vimeendelea kupungua japo kwa kasi ndogo licha ya hatua za kisera zinazochukuliwa ili kushusha riba. Wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 16.18 mwaka 2022 kutoka asilimia 16.59 mwaka 2021. Mwenendo huu ulichagizwa zaidi na utekelezaji wa sera wezeshi ya bajeti, na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza riba za mikopo, hatua ambazo zimesababisha baadhi ya benki kutoa mikopo kwa riba ya chini ya asilimia 10 hususan katika shughuli za kilimo. Aidha, wastani wa viwango vya riba za amana za muda maalum na za mwaka mmoja uliongezeka hadi asilimia 7.11 na asilimia 8.53 mwaka 2022 kutoka asilimia 6.82 na asilimia 8.27 mwaka 2021 mtawalia.

**(b) Ujazi wa Fedha na Karadha**

Katika mwaka 2022, Serikali kupitia Benki Kuu imetekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi ili kukabiliana na shinikizo la kuongezeka kwa mfumuko wa bei bila kuathiri kasi ya ukuaji wa uchumi. Utekelezaji huu unalenga kuhakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye mabenki kinachoendana na mahitaji halisi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hadi kufikia Januari 2023, ujazi wa fedha ulikuwa sambamba na malengo ya sera ya fedha ukichangiwa na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na UVIKO - 19 na ongezeko la mikopo ya benki kwa sekta binafsi. Katika kipindi hicho, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 12.8 na kufikia shilingi bilioni 38,803.3 kutoka shilingi bilioni 34,395.6 mwaka 2022. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 12.3 kutoka kiasi cha shilingi bilioni 27,062.2 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 30,383.8 mwaka 2023. Aidha, ujazi wa fedha kwa tasfiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 6.7 na kufikia shilingi bilioni 18,833.0 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 17,651.5 mwaka 2022.

**(c) Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 27,372.5 mwaka 2022 kutoka shilingi bilioni 22,344.1 mwaka 2021 sawa na ukuaji wa asilimia 22.5 ikilinganishwa na asilimia 10 katika kipindi cha mwaka 2021. Ukuaji huu umetokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, pamoja na utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti. Katika kipindi hicho, ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi lilikuwa kwa kasi zaidi kwenye shughuli za kilimo, uchimbaji madini na mawe, uzalishaji viwandani na shughuli binafsi. Ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa shughuli za kilimo lilitokana pia na hatua za kisera zilizochukuliwa mnamo mwezi Julai 2021, kwa ajili ya kuchochea ongezeko la mikopo na kushusha viwango vya riba katika shughuli za kilimo. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo imeendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi (biashara ndogondogo na biashara za kati) kwa asilimia 38.2, ikifuatiwa na biashara kwa asilimia 16.8, uzalishaji viwandani kwa asilimia 10 na kilimo kwa

asilimia 8.6. Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi inatarajiwa kuendelea kuwa imara na ya kuridhisha kutokana na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, kuimarika kwa shughuli za uzalishaji mali na hatua zinazoendelea kufanywa na serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

**(d) Mwenendo wa Thamani ya Shilingi**

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara imeendelea kuwa tulivu, licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika uchumi wa dunia hususan ongezeko la bei za bidhaa. Hali hii imetokana na utulivu wa mfumuko wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wetu wa kibiashara, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, na uwepo wa chakula cha kutosha nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,314.5 ikilinganishwa na shilingi 2,309.1 kipindi kama hicho mwaka 2021, ikiwa ni sawa na punguzo la thamani ya shilingi la chini ya asilimia moja.

**(e) Mikopo Chechefu**

Ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika kutokana na kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu kufikia asilimia 5.8 mwezi Desemba 2022 kutoka asilimia 8.2 Desemba 2021. Hali hii ilichangiwa zaidi na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kwa kuongeza ukwasi katika uchumi uliowezesha wateja kulipa mikopo kwa wakati pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Benki Kuu ikiwemo kuongeza ufuatiliaji wa utoaji mikopo; kuwaondoa katika sekta ya benki wafanyakazi wa benki wasio waaminifu; kuamuru benki kutumia taarifa za mikopo kutoka kwenye makampuni ya kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; utekelezaji wa kanuni za kuwalinda walaji wa huduma za kibenki kwa kuhakikisha utunzaji wa haki na usawa wa walaji pamoja na wakopaji; kuhakikisha kunakuwa na uwazi wa taarifa pamoja na kutoa elimu ya fedha/ufahamu kwa walaji; kuziamuru benki kuwa na mifumo ya udhibiti na utawala bora kwa kupitia upya mifumo iliyopo ili kukidhi mabadiliko na maendeleo katika sekta ya benki; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu zao za utoaji wa mikopo na ufuatiliaji.

**(f) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki**

Sekta ya benki imeendelea kuwa imara na kutengeneza faida ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Viwango vya amana na rasilimali vimeendelea kuongezeka na kuimarisha sekta ya benki dhidi ya misukosuko ya ndani na nje. Uwiano wa mtaji wa msingi wa sekta ya benki ukilinganishwa na jumla ya rasilimali ulifikia asilimia 18.0 Desemba 2022, ikilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10.0. Aidha, uwiano wa ukwasi wa sekta ya benki kiujumla (Liquid Assets to Demand Liabilities) ulipungua kufikia asilimia 26.43 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 29.38 mwaka 2021. Hata hivyo, uwiano huo ni wa juu ukilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 20.0 na hivyo kuendelea kuwa toshelevu kwa mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sekta ya benki imeendelea

kutengeneza faida ambapo faida baada ya kodi (kabla ya ukaguzi wa fedha) kwa mwaka 2022 ilifikia shilingi bilioni 998.1 kutoka shilingi bilioni 655.0 kwa mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 52.4.

**(a) Soko la Upili la Hatifungani**

**Hatifungani za Serikali**

Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 15.4 na kufikia shilingi trilioni 3.0 katika kipindi kilichoishia Desemba 2022, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi trilioni 2.6 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Serikali kulitokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu iliyotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Hatifungani za Kampuni *(Corporate Bonds)***

Kwa upande wa hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Desemba 2022, mauzo yalikuwa shilingi milioni 626.41 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.5 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2021. Kupungua kwa mauzo ya hatifungani za kampuni kumetokana na sehemu kubwa ya wawekezaji kuwa na malengo ya kuleta matokeo chanya ya kijamii (social impact investors) na hivyo kuendelea na umiliki wa hatifungani zao hadi kipindi zitakapoiva.

**Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Collective Investment Schemes) katika kipindi kilichoishia Desemba 2022 ulikuwa wa kuridhisha. Thamani ya uwekezaji katika mifuko sita (6) ya uwekezaji wa pamoja inayoendeshwa na kampuni ya UTT AMIS iliongezeka kwa asilimia 61.1 na kufikia shilingi trilioni 1.2 katika kipindi kilichoishia Desemba 2022 ikilinganishwa na shilingi bilioni 744.9 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji. Jedwali Na. 1.5 linaonesha mwenendo wa uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

**Jedwali Na.1.5: Mwenendo wa Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

| | 31 Desemba 2022 | | 31 Desemba 2021 | | Ongezeko la thamani | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Mfuko | Thamani ya Mfuko | Bei ya Kipande | Thamani ya Mfuko (TSH) | Bei ya Kipande | Ongezeko la Thamani ya Mfuko | Ongezeko la Bei ya Kipande (%) |
| | (TSH Bilioni) | | (TSH Bilioni) | | (%) | (%) |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfuko wa Umoja | 302.29 | 877.04 | 269.46 | 776.68 | 12.18% | 12.92% |
| Mfuko wa Wekeza Maisha | 6.66 | 741.65 | 2.54 | 659.45 | 162.51% | 12.46% |
| Mfuko wa Watoto | 8.43 | 547.97 | 4.60 | 483.45 | 83.23% | 13.35% |
| Mfuko wa Jikimu | 19.12 | 159.12 | 17.32 | 151.52 | 10.40% | 5.01% |
| Mfuko wa Ukwasi | 559.27 | 342.52 | 304.34 | 302.44 | 83.77% | 13.25% |
| Mfuko wa Hatifungani | 322.54 | 114.76 | 146.67 | 111.65 | 119.92% | 2.78% |
| Mfuko wa Faida (Watumishi Housing Investment) | 12.95 | 100.00 | Mfuko wa Faida ulikuwa bado haujapata idhini ya kutoa huduma ya uwekezaji. | | NIL | NIL |
| **Thamani ya Jumla** | **1,231.26** | | **744.93** | | | |

***Chanzo**: UTT AMIS Plc*

**(b) Mwenendo wa Soko la Hisa**

Mwenendo wa biashara katika soko la hisa hupimwa kwa kuzingatia viashiria vya ufanisi wa soko. Viashiria hivyo ni pamoja na: Thamani ya Mauzo ya hisa; Mtaji wa Soko (*Market Capitalisation*); Fahirisi za Soko (Share Index); na ushiriki kwenye Soko la Hisa. Katika kipindi cha kuanzia Januari 2022 hadi Desemba 2022 mwenendo wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam ulikuwa wa kuridhisha. Ufanisi huu uliotokana na juhudi za Serikali katika kutoa elimu ya masuala ya uwekezaji na fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji na dhamana.

**Mtaji wa Soko la Hisa**

Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani yaani *Domestic Market Capitalisation* kufikia Desemba 2022 uliongezeka kwa asilimia 9.6 na kufikia shilingi trilioni 10.3 ikilinganishwa na shilingi trilioni 9.4 mwezi Desemba 2021. Kuongezeka kwa mtaji wa Soko la Hisa kumetokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Kampuni hizo ni pamoja na CRDB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited (NICO), NMB Bank Plc, Swissport Tanzania Plc, Tanga Cement Plc, na TOL Gases Limited. Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa (*Total Market Capitalisation*) katika kipindi kilichoishia Desemba 2022 ulipungua na kufikia shilingi trilioni 15.68 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.81 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 sawa na upungufu wa asilimia 0.8. Kupungua kwa Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa kumechangiwa na kupungua kwa bei za hisa za

kampuni zilizoorodheshwa kutoka Soko la Hisa la Nairobi yaani *Crosslisted Companies*. Kampuni hizo ni East African Breweries Limited (EABL), Nation Media Group (NMG) NMG, Kenya Commercial Bank (KCB) na Kenya Airways.

**Mauzo ya Hisa na Hatifungani**

Mauzo ya hisa katika Soko la Hisa yaliongezeka kwa asilimia 28.2 na kufikia shilingi bilioni 133.7 katika kipindi kilichoishia Desemba 2022, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 104.3 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021. Kuongezeka kwa mauzo kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji katika masoko ya mitaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Fahirisi ya Soko *(Market Index)***

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani yaani *Domestic Market Index* katika kipindi kilichoishia Desemba 2022, iliongezeka kwa alama 323.63 na kufikia alama 3,888.81 ikilinganishwa na alama 3,565.18 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2021. Kuongezeka kwa alama za fahirisi kunaashiria ufanisi wa soko hususan kuongezeka kwa bei za hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE. Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote katika kipindi kilichoishia Desemba 2022, ilipungua kwa alama 14.72 na kufikia alama 1,881.99 ikilinganishwa na alama 1,896.71 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2021. Kupungua kwa alama za Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote kumetokana na kupungua kwa bei za hisa za kampuni zilizoorodheshwa kutoka Soko la Hisa la Nairobi yaani *Crosslisted Companies*. Kampuni hizo ni East African Breweries Limited (EABL), Nation Media Group (NMG), Kenya Commercial Bank (KCB) na Kenya Airways.

### 1.3.5. Deni la Serikali

Deni la Serikali kwa mwezi Desemba 2022 lilikuwa shilingi bilioni 74,637.91, sawa na ongezeko la asilimia 9.30 ikilinganishwa na shilingi bilioni 68,286.18 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 49,069.98 na deni la ndani ni shilingi bilioni 25,567.93. Ongezeko la deni limetokana na: kupokea fedha kutoka mikopo ya zamani na mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya pamoja na kutolewa kwa hatifungani maalumu yenye thamani ya shilingi bilioni 2,176.7 kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999.

Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba, 2022 imeonesha kuwa deni ni himilivu na viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu **(Jedwali Na. 1.4)**.

**Jedwali Na. 1.4: Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (Asilimia) kwa Mwaka 2022**

| Viashiria Vya Uhimilivu | Ukomo | 21/22 | 22/23 | 23/24 | 24/25 | 25/26 | 26/27 | 27/28 | 32/33 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Deni la Nje** | | | | | | | | | |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Pato la Taifa | **40** | 18.1 | 17.7 | 17.3 | 16.4 | 15.8 | 15.8 | 16.3 | 15.4 |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | **180** | 119.6 | 113.4 | 108.1 | 104.0 | 101.9 | 101.3 | 99.7 | 92.1 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nchi | **15** | 13.5 | 14.1 | 9.6 | 8.9 | 8.5 | 8.2 | 8.8 | 10.6 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | **18** | 14.1 | 14.9 | 10.4 | 9.6 | 9.3 | 9.3 | 10.9 | 12.2 |
| **Deni la Serikali (Ndani na Nje)** | | | | | | | | | |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa pato la Taifa | **55** | 32.5 | 31.9 | 30.9 | 29.5 | 28.4 | 27.8 | 28.6 | 30.8 |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa Mapato | **N/A** | 217 | 207 | 202 | 196 | 194 | 195 | 207.7 | 207.1 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | **N/A** | 34.0 | 41.6 | 33.3 | 30.5 | 27.6 | 27.7 | 30.1 | 41.0 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango, Novemba 2022*

Katika kuhakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:

(i) Kuhakikisha mikopo inayopewa kipaumbele ni ile yenye masharti nafuu kwa lengo la kupunguza gharama za ufadhili na kutoa rasilimali za kutosha kutekeleza miradi ya kimkakati;

(ii) Mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi. Kukuza maendeleo ya soko la fedha za ndani kwa kuendelea kukopa katika soko la ndani; na

(iii) Kuboresha mikakati ya kukusanya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika bila kuathiri uendeshaji wa shughuli za Serikali.

## 1.4. Maendeleo ya Watu

### 1.4.1. Ongezeko la Idadi ya Watu mwaka 2022

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu Tanzania Bara imeongezeka na kufikia watu 59,851,347 mwaka 2022 kutoka watu 43,625,354 mwaka 2012 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.2. Kati ya idadi hiyo, wanawake ni 30,713,709 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 29,137,638 sawa na asilimia 49 ya watu wote. Matokeo ya sensa ni nyenzo muhimu katika mipango jumuishi na maendeleo endelevu ya nchi.

Aidha, kwa mujibu wa Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi 2020/21, idadi ya nguvu kazi yenye umri wa miaka 15 na kuendelea imeongezeka kwa asilimia 20.6 kutoka watu 25,750,116 na kufikia watu 31,047,894 sawa na asilimia 54.8 ya idadi ya watu wote mwaka 2020/21. Kuongezeka kwa nguvu kazi ni fursa kubwa nchini katika shughuli mbalimbali za uzalishaji pamoja na sekta za huduma na masoko. Kwa upande mwingine, ongezeko la watu linaweza kuwa na athari hasi ikiwepo ongezeko la bajeti katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

### 1.4.2. Viashiria vya Maendeleo ya Watu

Katika kuendelea kuboresha maendeleo ya watu, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo: uboreshaji wa huduma za afya; utoaji wa elimu msingi bila ada; usambazaji wa umeme mijini na vijijini; utoaji wa huduma ya maji mijini na vijijini; na utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo:

(i) Kuongezeka kwa makadirio ya wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 67.8 (2023) hadi miaka 68.3 (2024) na makadirio ya wastani wa miaka 68.8 kwa mwaka 2025. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, unakadiriwa kufikia miaka 70.7 kwa wanawake na miaka 65.7 kwa wanaume mwaka 2024;

(ii) Vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 (2015/16) hadi 45 (2020/21) kwa kila vizazi hai 1,000;

(iii) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 250 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020/21;

(iv) Kuongezeka kwa idadi ya watanzania wanaonufaika na huduma za bima za afya kutoka asilimia 21.2 ya Idadi ya watu mwaka 2019/20 hadi asilimia 30.6 mwaka 2021/22;

(v) Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka 1,631,085 mwaka 2021 hadi wanafunzi 1,680,365 mwaka 2022, sawa

na ongezeko la asilimia 3.0;

(vi) Ongezeko la upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini, ambapo upatikanaji wa maji vijijini umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 72.3 Juni, 2021 hadi wastani wa asilimia 74.5 Juni, 2022 na kwa upande wa mijini, huduma ya maji safi imeongezeka kutoka asilimia 86 Juni, 2021 hadi asilimia 86.5 Juni, 2022; na

(vii) Idadi ya vijiji vilivyounganishwa na umeme vimeongezeka kufikia vijiji 9,467 kati ya vijiji 12,318 sawa na asilimia 76.7 ya vijiji vyote Tanzania Bara.

#### 1.4.2.1. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

Serikali kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini imeendelea na jitihada za kupunguza umaskini nchini ambapo hadi Desemba, 2022 jumla ya kaya 1,371,078 zenye watu 5,180,684 katika Mamlaka ya Maeneo ya Utekelezaji 186 zimeendelea kulipwa ruzuku ambapo jumla ya shilingi bilioni 168.6 zilitumika. Aidha, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: jumla ya Vikundi 12,054 vyenye Wanachama165,608 (wanaume 28,157 na wanawake 137,451) vilianzishwa katika maeneo 55 ya utekelezaji; Mpango umeendelea na utekelezaji wa miradi ya ajira za muda katika maeneo 123 ambapo miradi 14,236 yenye thamani ya shilingi bilioni 56.76 imeibuliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

#### 1.4.2.2. Upatikanaji wa Chakula

Taarifa ya Tathmini ya Awali ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Msimu wa 2021/2022 kwa ajili ya kubaini upatikanaji wa chakula nchini kwa mwaka 2022/2023 inaonesha kuwa, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2021/2022 utafikia tani 17,403,880 kwa mlinganisho wa nafaka *(Grain Equivalent)* ambapo mazao ya nafaka ni tani 9,493,410 na mazao yasiyo nafaka ni tani 7,910,470.

Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2022/23 ni tani 15,073,855 ambapo tani 9,537,752 ni za mazao ya nafaka na tani 5,536,113 ni mazao yasiyo ya nafaka. Pamoja na upungufu wa uzalishaji kwa upande wa mazao ya nafaka utengamano wa hali ya chakula nchini utaendelea kuwepo kutokana na ziada inayotokana na mazao yasiyo nafaka. Kiwango cha Utoshelevu wa chakula (Self Sufficiency Ratio – SSR) nchini kinatarajiwa kuwa na ziada kwa uwiano wa asilimia 115 mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na asilimia 125 mwaka 2021/2022.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

## 2.1. Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa muhtasari utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya Mwaka 2022/23. Aidha, inaainisha bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, kiasi cha fedha kilichotumika na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo.

## 2.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2022/23

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 umetengewa jumla ya shilingi bilioni 15,006.0, sawa na asilimia 36.2 ya Bajeti ya Serikali ambapo shilingi bilioni 12,306.9, sawa na asilimia 82.0 ya bajeti ya fedha za maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,699.1, sawa na asilimia 18.0 ni fedha za nje.

Ridhaa ya matumizi ya fedha za maendeleo iliyotolewa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Januari 2023, ni shilingi bilioni 8,636.7 sawa na asilimia 97.8 ya lengo katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho kilichotolewa, shilingi bilioni 7,047.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,588.9 ni fedha za nje. Aidha, baadhi ya maeneo ya kipaumbele yaliyopatiwa fedha za maendeleo katika kipindi husika ni kama ifuatavyo:

(i) Shilingi bilioni 869.93 kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji – MW 2,115;

(ii) Shilingi bilioni 762.99 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge Railway)*;

(iii) Shilingi bilioni 710.86 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara kuu, barabara za mikoa, barabara za mijini na vijijini na madaraja;

(iv) Shilingi bilioni 257.5 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu;

(v) Shilingi bilioni 268.48 kwa ajili ya kuimarisha usafirishaji majini ikiwemo ujenzi na ukarabati wa bandari, ununuzi na ukarabati wa meli na vivuko katika bandari za maziwa makuu;

(vi) Shilingi bilioni 108.86 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini;

(vii) Shilingi bilioni 187.33 kwa ajili ya ukarabati wa Reli ya Kati (Mfuko wa Maendeleo ya Reli);

(viii) Shilingi bilioni 176.10 kwa ajili ya kugharamia elimumsingi bila ada ikijumuisha mahitaji ya wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari za Serikali na posho ya madaraka kwa wakuu wa shule, waratibu elimu kata na walimu wakuu;

(ix) Shilingi bilioni 125.28 kwa ajili ya mradi wa usambazaji umeme vijijini kupitia

Wakala wa Nishati Vijijini (REA); na

(x) Shilingi bilioni 125.90 kwa ajili ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na chanjo za watoto kupitia MSD.

## 2.3. Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

### 2.3.1. Miradi ya Kielelezo

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo ni kama ifuatavyo:

**(i) Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 97.91; kuendelea na ujenzi wa njia kuelekea bandarini (Port link) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 31.42; kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 92.23; kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 25.75; kipande cha Makutupora- Tabora (km 371) asilimia 4.59; na kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka (km 163); kupatikana kwa wakandarasi wa kipande cha Tabora – Kigoma (Km 506).

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Ununuzi wa vichwa viwili (2) vya treni na mabehewa 30 kwa ajili ya majaribio na uendeshaji wa awali; kufanyika kwa sehemu ya malipo kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni 17 vya umeme na seti 10 za treni (Electric Multiple Unit - EMU) kwa ajili ya uendeshaji ambapo utengenezaji umefikia asilimia 31.6 na seti moja (1) ya treni hizo inatarajiwa kuwasili mwezi Juni, 2023; kununuliwa kwa mabehewa 59 ambapo matengenezo yamefikia asilimia 92.0 na mabehewa 14 yameshawasili nchini; na ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo ambapo utengenezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 762.99 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 3172: Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa handaki la kuchepusha maji (diversion tunnel); kuendelea na ujenzi wa kingo ndogo za juu na chini ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98, ukuta wa bwawa kuu asilimia 90.70, handaki la kupeleka maji kwenye mitambo (power waterway) asilimia 97.01, jengo la mitambo (power house) (asilimia 62.74), kituo cha kupokea na kusafirishia umeme (switchyard) (asilimia 98), kingo saidizi kuzuia maji yasitoroke (asilimia 70), nyumba za makazi za watumishi (asilimia 87.40), barabara za kudumu (asilimia 34.07) na daraja la kudumu (asilimia 96.87). Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 81.86. Aidha, zoezi la ujazaji maji linaendelea ambapo kimo cha maji ya bwawa kimefika mita 134.39 kutoka usawa wa bahari. Jumla ya shilingi bilioni 869.93 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa sehemu ya malipo ya ununuzi wa ndege tano (5)

ambapo kati ya hizo, ndege moja (1) ni aina ya Boeing 767-300F ya mizigo inayaotarajiwa kuwasili Machi 2023, ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 zitakazowasili Julai 2023 na Oktoba 2023, ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner itakayowasili Novemba, 2023 na ndege moja (1) aina ya De Havilland Dash 8-Q400 inatarajiwa kuwasili Juni 2023; ukarabati wa miundombinu katika karakana ya KIMAFA katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA) unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Aidha, ununuzi wa vifaa na vipuri kwa ajili ya kuwezesha kufanya matengenezo makubwa na madogo kwa ndege zote unaendelea katika hanga zote za JNIA na KIA; kuanza ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA na ujenzi wa majengo matatu ya kuhifadhia mizigo katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Songwe. Aidha, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 14 vya ndani ya nchi pamoja na vituo 10 vya nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 20.52 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas - LNG)* – Lindi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na stadi za kisayansi (geoscience) na stadi za mitambo itakayosimikwa katika eneo la mradi; na kuendelea na majadiliano ya Mkataba Hodhi (HGA) kati ya Serikali na Wawekezaji. Aidha, Mshauri Elekezi (Kampuni ya Baker Botts) ambaye anaishauri Serikali kuhusu masuala ya sheria, fedha, biashara, uchumi na masoko ameendelea na kazi kwa kushirikiana na Timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT). Jumla ya shilingi milioni 963.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**

Hatua iliyofikiwa ni: Kulipwa fidia kwa wananchi 8,386 kati ya 9,508 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba; kuendelea kulipa hisa katika Kampuni ya EACOP na kufikia dola za Marekani milioni 131.0; kuendelea na ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba (thermal insulation plant) katika kijiji cha Sojo, Nzega Tabora ambapo utekelezaji umefikia asilimia 49. Jumla ya shilingi bilioni 30.39 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusafishwa kwa eneo lenye ukubwa wa hekta 600 kati ya hekta 845 ambapo hekta 219 zimelimwa na kupandwa miwa. Hii inafanya ukubwa wa eneo lililopandwa miwa kufikia hekta 2,974 sawa na asilimia 83; kuendelea na mchakato wa kumtafuta mkandarasi wa kufunga mifumo ya umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 500; Kupatikana kwa Mkandarasi wa ujenzi wa bwawa kubwa lenye uwezo wa kujaza maji kiasi cha mita za ujazo milioni 3.5; ujenzi wa kiwanda cha sukari Mbigiri umefikia asilimia 75; na kununuliwa kwa mtambo wa kupakia miwa "Cane Loader". Jumla ya shilingi bilioni 39.84 zimetumika katika kipindi cha nusu ya

kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 4015: Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa daraja pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66 ambapo ujenzi umefikia asilimia 63. Jumla ya shilingi bilioni 93.09 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(viii) Mradi Na. 4191: Daraja Jipya la Selander (Tanzanite Dar es Salaam)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa barabara unganishi zenye urefu wa km 5.2. Jumla ya shilingi bilioni 1.74 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

### 2.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 2.3.2.1. Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma

#### A. Reli

**(i) Mradi Na. 4213: Mfuko wa Reli**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria kwa ajili ya reli ya MGR; kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa kumi (10) ya mizigo na behewa moja (1) la abiria na kuanza kutoa huduma; kukamilika kwa uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na umeme katika njia ya reli ya MGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza; na kuendelea na uundaji wa vichwa viwili (2) vya treni vya njia kuu aina ya 88U na vichwa saba (7) vya sogeza aina ya 64XX ambapo utekelezaji umefikia asilimia 43. Jumla ya shilingi bilioni 187.33 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

#### B. Barabara na Madaraja

**Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi**

**(a) Mradi Na. 4147: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kipande cha Kidatu – Ifakara (km 68) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 71.3. Jumla ya shilingi bilioni 5.66 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235**)
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 29; Tarime – Mugumu (km 86) sehemu ya Mogabiri – Nyamongo asilimia 8; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Natta – Mugumu (km 45). Jumla ya shilingi bilioni 12.69 zimetumika katika

nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha Lusitu – Mawengi (km 50); na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 2. Jumla ya shilingi bilioni 15.26 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4193: Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro - Singida (Km 460)**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Handeni – kiberashi (km 50) sehemu ya Handeni - Mafuleta (km 20) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 11 na sehemu ya Mafuleta – Kileguru (km 30) taratibu za manunuzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 2.41 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4188: Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni - Mkiwa (km 528)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9) kwa kiwango cha lami sehemu ya Noranga – Itigi (Mlongaji – km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 7.5; na sehemu ya Mlongaji - Mkiwa (km 31.9). taratibu za manunuzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 2.91 zimetumika katika nusu ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 4112: Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kipande cha Chagu – Kazilambwa (km 36) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 74.4; na kuendelea kwa ujenzi wa kipande cha Uvinza – Malagarasi (km 51.1) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 22. Jumla ya shilingi bilioni 26.16 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 4041: Barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) na Daraja la Mnywamaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) sehemu ya Amanimakoro – Ruanda (km 35) na ujenzi wa daraja la Mnywamaji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 22; na sehemu ya Luanda – Ndumbi Port (km 50) taratibu za manunuzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 5.99 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 4174: Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa kipande cha Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji ambapo utekelezaji

umefikia asilimia 96. Jumla ya shilingi bilioni 5.68 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kipande cha Nanganga – Ruangwa (km 53.2) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 59. Aidha, taratibu za manunuzi zinaendelea kwa sehemu ya Ruangwa – Nachingwea (km 57.6). Jumla ya shilingi bilioni 7.87 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kipande cha Tanga - Pangani (km 50) kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 62 na barabara ya Pangani – Mkange (km 214.5); sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) utekelezaji umefikia asilimia 15. Aidha, ujenzi wa daraja la Pangani (m 525) na barabara unganishi (km 25.6) unaendelea. Jumla ya Shilingi bilioni 11.64 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 152)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200) sehemu ya Ntendo – Muze (km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 12. Jumla ya shilingi bilioni 4.43 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(l) Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi sehemu ya Moronga – Makete (km 53.5) kwa kiwango cha lami; kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) Sehemu ya Kitulo– Iniho (km 36). Jumla ya shilingi bilioni 6.61 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(m) Mradi Na. 4123: Barabara ya Dumila – Kilosa (km 141)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93. Jumla ya Shilingi bilioni 1.26 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**(a) Mradi Na. 4124: Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami sehemu ya Matai – Tatanda (km 25) ambapo utekelezaji

umefikia asilimia 10 na sehemu ya Tatanda – Kasesya (km 25) taratibu za manunuzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 5.97 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 271)**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 46. Jumla ya shilingi 14.69 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya Mpanda – Mishamo – Uvinza Sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 2 na sehemu ya Luhafwe – Mishamo Jct (Bulamata) – km 37.25 taratibu za manunuzi zinaendelea; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Sitalike (km 71) sehemu ya Kibaoni – Mlele Jct (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 4 na sehemu ya Mlele Jct – Sitalike (km 21) taratibu za manunuzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 12.14 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4141: Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha Kisorya - Bulamba (km 51) kwa kiwango cha lami; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda - Bulamba (km 56.4) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88. Jumla ya shilingi bilioni 17.96 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4162: Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 121)**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Maswa (km 11), ambapo utekelezaji umefikia asilimia 72. Jumla ya shilingi bilioni 3.96 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25**)

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu za Kanyani *Junction* – Mvugwe (km 70.5) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52.71, Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35) asilimia 59.19, Kibondo *Junction* – Kabingo (km 62.5) asilimia 71.32 na Nduta Junction – Kibondo (km 25.9) asilimia 57.3. Jumla ya shilingi bilioni 8.29 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kumunazi –Bugene - Kasulo kwa kiwango cha lami sehemu za Kyaka – Mutukula na Bugene – Burigi *Chato National Park* (km 60) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10. Jumla ya shilingi bilioni 14.06 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Barabara za Mikoa na Kupunguza Msongamano**

**(a) Mradi Na. 4138: Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6) ambapo ujenzi wa km 1 umekamilika; na kuendelea kwa usanifu kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1). Jumla ya shilingi bilioni 1.52 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4145: Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68)**
Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu Mjini (spur roads) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45.05. Jumla ya shilingi milioni 329.97 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4132: Barabara za Mikoa (km 770.50)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa km 23.11 kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 22.4; kukamilika kwa ukarabati wa km 253.67 za barabara za mikoa kwa kiwango cha changarawe sawa na asilimia 24.33 ya lengo; na ujenzi wa madaraja 14 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52. Jumla ya shilingi bilioni 27.43 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(d) Mradi Na. 4285 Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Dar es Salaam)**
**Awamu ya Pili**
Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa *Lot 1* inayohusisha barabara zenye urefu wa km 20.3 (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu) – Kariakoo, Barabara ya Kawawa – barabara ya Morogoro (Magomeni), Barabara ya Chang'ombe – Barabara ya Kilwa) ambapo ujenzi umefikia asilimia 82. Jumla ya shilingi bilioni 179.89 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Awamu ya Tatu**
Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere hadi Gongo la Mboto zenye jumla ya kilomita 23.6 na kituo kikuu cha mabasi Kariakoo; Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA

umeanza ambapo utekelezaji umefikia asilimia 2. Jumla ya shilingi bilioni 34.75 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4146: Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma**

Hatua iliyofikiwa: Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya mzunguko (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot 1 & 2 km 112.3), sehemu za barabara ya Nala – Veyula – Mtumba – *Ihumwa Dry Port* (km 52.3) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 19; Ihumwa - Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60) asilimia 14; Kikombo Jctn – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) asilimia 5. Jumla ya shilingi bilioni 18.65 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Barabara za Vijijini na Mijini**

**Mradi Na. 4170: Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa matengenezo ya barabara yenye urefu wa km 8,446.78 kati ya hizo km 5251.23 ni matengenezo ya kawaida, km 1,906.12 matengenezo sehemu korofi na km 1,289.44 ni matengenezo ya muda maalum; kukamilika kwa ujenzi wa bararaba kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 180 na barabara za changarawe zenye urefu wa km 4,785, ujenzi wa madaraja makubwa na boksi kalvati 2,368 na mifereji wa maji ya mvua yenye urefu wa km 97.61. Jumla ya shilingi bilioni 343.18 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Ujenzi wa Nyumba za Serikali na Madaraja**

**(a) Mradi Na. 4126: Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Kiyegeya (Morogoro), daraja la Ruhuhu (Ruvuma), daraja la Msingi (Singida); kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi (km 18) katika daraja la Kitengule (Kagera) na daraja la Sibiti (Singida km 25); na kuanza ujenzi wa daraja la *Lower* Malagarasi. Jumla ya shilingi bilioni 3.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4020: Daraja Jipya la Wami (Pwani)**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Wami lenye urefu wa mita 510 na barabara unganishi (km 4.3). Jumla ya shilingi bilioni 14.85 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Serikali**

Hatua iliyofikiwa: Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Jijini Dodoma na kufanya maandalizi ya kuanza awamu ya II; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba 40 kati ya 66 zilizohamishiwa TBA kutoka CDA; kuendelea na ujenzi wa nyumba 150 za makazi ya watumishi wa umma katika eneo la Nzuguni Jijini Dodoma, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za majaji katika

mikoa ya Kilimanjaro moja (1), Tabora moja (1) Kagera moja (1) na kuendelea na ujenzi katika mikoa ya Shinyanga moja (1) asilimia 90 na Mtwara moja (1) asilimia 93; kuendelea na ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma eneo la *Area D* ambapo utekelezaji umefikia asilimia 18; kuendelea na ukarabati wa nyumba 30 za viongozi mikoani na matengenezo kinga ya majengo ya Magomeni Kota ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50; kuendelea na ukarabati wa nyumba zinazomilikiwa na TAMISEMI/NHC katika mikoa 20 zilizohamishiwa TBA umefikia asilimia 67.5; kuendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi Temeke Kota ambapo utekelezaji umefikia asilimia 7; na kuendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa makazi ya Watumishi katika eneo la Magomeni Kota *Block A* ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96 na *Block B* asilimia 15. Jumla ya shilingi bilioni 11.26 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**C. Usafiri Majini**

**(i) Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu umefikia asilimia 80; kuendelea na ukarabati wa meli ya MV Umoja umefikia asilimia 67; kuendelea na ukarabati wa meli ya MT Sangara umefikia asilimia 90.7; kuendelea na ununuzi wa wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya tatu (3) pamoja na chelezo ambapo meli mbili (2) zitajengwa katika Ziwa Tanganyika, meli moja (1) itajengwa katika Ziwa Victoria na Chelezo itajengwa Ziwa Tanganyika. Jumla ya shilingi bilioni 19.63 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4201: Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokozi katika maeneo ya Kanyara (Geita), Ukerewe na Musoma. Jumla ya shilingi milioni 205.51 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Vivuko**

**(a) Mradi Na. 4125*:* Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam; kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa maegesho katika vituo 6 (Magogoni – Kigamboni, Kilambo - Namoto, Utete-Mkongo, Iramba – Majita, Nyakaliro – Kome na Kasharu – Buganguzi); Ujenzi wa miundombinu ya majengo ya kusubiria abiria, ofisi na fensi katika vituo vya Bugolora – Ukara unaendelea, Mwigobelo (Musoma) umefikia asilimia 20 na vituo vya Nyakarilo – Kome na Kisorya – Rugezi vipo kwenye hatua za manunuzi; ujenzi wa maegesho ya Mayenzi – Kanyinya umefikia asilimia 30 ya utekelezaji na maegesho ya Muleba – Ikuza yapo kwenye hatua za manunuzi; ujenzi wa maegesho mapya ya Ijinga – Kahangala (Magu) na Bwiro – Bukondo (Ukerewe) yapo hatua za awali za ujenzi. Jumla ya shilingi milioni 696.17 zimetumika katika

nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4139: Ujenzi wa Vivuko Vipya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi ambapo ujenzi umefikia hatua ya kufunika *hull*; na kukamilika kwa taratibu za kumpata Makandarasi wa ujenzi wa vivuko vipya vya Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Bayugu - Mbalika, Nyakarilo – Kome na Nyamisati – Mafia. Aidha, ununuzi wa kivuko kipya cha Magogoni - Kigamboni upo kwenye hatua za mwisho za manunuzi. Jumla ya shilingi bilioni 9.41 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4144*:* Ukarabati wa Vivuko**

Hatua iliyofikiwa: Kukamilika kwa Ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Kazi, MV TEMESA na MV Tanga; na kuendelea na ukarabati wa vivuko vya MV Misungwi (50%), MV Nyerere (65%), MV Kilombero (65%) na MV Ujenzi (65%). Aidha, Ukarabati wa vivuko vya MV Kitunda, MV Magogoni na MV Kyanyabasa upo kwenye hatua za manunuzi. Jumla ya shilingi bilioni 3.83 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**D. Bandari**

**(a) Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam**

**(i) Bandari ya Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi ambapo shughuli zilizotekelezwa ni: Kuchimba na kupanua lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli hadi kufikia kina cha mita 15.5 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75. Jumla ya shilingi bilioni 30.22 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Bandari ya Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Uboreshaji wa Bandari ya Tanga upo katika awamu ya pili ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 91 unaohusisha uboreshaji wa gati namba 1 na 2. Jumla ya shilingi bilioni 173.7 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Bandari Kavu katika Eneo la Ruvu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa National Optic Fiber, Nyumba za Makazi, Ofisi na ufungaji wa umeme; kuendelea na ujenzi wa yadi na sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta tano (5) kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo ambapo umefikia asilimia 87; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Vigwaza/Kwala ambapo umefikia asilimia 98. Jumla ya shilingi bilioni 44.83 zimetumika katika kipindi

cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Bandari za Maziwa Makuu**

**(i) Ziwa Victoria**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa Bandari za Bukoba na Kemondo Bay; na kupatikana kwa Makandarasi kwa ajili ya uboreshaji wa bandari ya Mwanza North. Jumla ya shilingi bilioni 3.96 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Ziwa Tanganyika**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Gati katika Bandari mpya ya Karema; kuendelea na usanifu wa ujenzi wa *Passenger Lounge* na ukuta wa mizigo wa *Lighter Quay* katika Bandari ya Kibirizi na gati la Bandari ya Ujiji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 69; na kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi ya mkuu wa Bandari ya Kigoma. Jumla ya shilingi bilioni 17.5 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Ziwa Nyasa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa gati, ghala la mizigo, ghala la abiria, ofisi na sehemu ya kuegesha meli (ramp) katika Bandari ya Ndumbi. Jumla ya shilingi bilioni 7.27 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**E. Usafiri wa Anga**

**(a) Mradi Na. 6267: *Institutional Support***

**(i) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (JNIA TB III) na Kuboresha Huduma katika Viwanja vya Ndege**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa huduma katika Viwanja ikiwemo ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 39; kuendelea na manunuzi ya gari la Zimamoto; kuendelea na ufungaji wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; na kukamilisha ulipaji wa malipo ya fidia kwa wakazi waliopisha upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 17.07 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi wa Ununuzi na Ufungaji wa Rada Nne (4) za Kuongoza Ndege za Kiraia JNIA, KIA, Mwanza na Songwe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ufungwaji wa rada nne (4) za kuongoza ndege za kiraia katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Kilimanjaro, Songwe na Mwanza. Jumla ya shilingi milioni 23.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya

kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4290: Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa matengenezo ya rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa katika mikoa ya Mbeya na Kigoma; kuendelea na utengenezaji wa rada mbili (2) zitakazofungwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75; kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa vifaa mbalimbali vya hali ya hewa ikiwemo seti tano (5) za vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi vilivyofungwa Musoma, Mwanza, Bukoba, Tabora na Kibondo pamoja na vifaa vya kupima hali joto ilivyofungwa katika Kituo cha hali ya hewa kilichopo Singida; kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa kompyuta maalum "*Cluster Computer*" yenye uwezo mkubwa wa kuchakata taarifa za hali ya hewa iliyofungwa katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA); kukamilika kwa ukarabati wa ofisi ya hali ya hewa na nyumba tatu (3) za wafanyakazi zilizopo Mahenge; na kuendelea na ukarabati wa ofisi ya hali ya hewa katika Kiwanja cha Ndege cha Songea. Jumla ya shilingi bilioni 5.05 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6377: Kuboresha Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia**

**(i) Chuo cha Taifa cha Usafirishaji - NIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ununuzi wa vifaa maalum (Full Motion Cabin Crew Mock-up and Fixed Cabin Crew Mock-up) vya mafunzo kwa wahudumu ndani ya ndege; kuendelea na ujenzi wa majengo nane (8) kwa ajili ya madarasa, maabara, karakana na ofisi za watumishi ambapo majengo matano (5) yanajengwa katika kampasi ya Mabibo – Dar es salaam na majengo matatu (3) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro; kununuliwa kwa *Aircraft Engineering System Trainers (runnerable turbo jet engine na motorised cutway piston engine)* na *Virtual Maintenance Trainer (VMT) for Boeing 737-800* kwa ajili ya mafunzo ya wahandisi wa matengenezo ya ndege. Jumla ya shilingi bilioni 1.42 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Chuo cha Bahari Dar es Salaam - DMI**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na taratibu za malipo kwa ajili ya kununua mtambo (full motion simulator) wa kufundishia kwa ajili ya kuongeza ubora na umahiri katika kuhudumia mizigo kwenye meli na vyombo vingine vya usafirishaji. Jumla ya shilingi milioni 275.41 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4209: Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa maegesho ya ndege, uzio wa kiwanja, maegesho ya magari; na kukamilika kwa usanifu wa jengo la abiria. Jumla ya shilingi milioni 27.5 imetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4220: Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, kusimika taa za kuongozea ndege na ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na uzio wa usalama ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96. Jumla ya shilingi bilioni 6.05 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Songwe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilka kwa ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege, ufungaji wa taa za kuongozea ndege na ujenzi wa uzio wa usalama; kukamilika kwa ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege na usimikaji wa taa; na kuendelea kukamilisha jengo jipya la abiria pamoja na ufungaji wa mifumo na vifaa vyake ambapo utekelezaji umefikia asilimia 94.96. Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege, kusimikwa kwa taa na mfumo wa kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege katika kiwanja cha Ndege cha Geita na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha changarawe katika kiwanja cha Nachingwea; kuendelea na ukarabati wa njia ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami katika kiwanja cha ndege Lindi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Ndege vya Songea (asilimia 98), Iringa (asilimia 42) na Musoma (asilimia 43). Jumla ya shilingi bilioni 10.18 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na barabara za maungio na maegesho ya ndege ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10.2; kuanza kwa ujenzi wa majengo ya abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la zimamoto, jengo la huduma ya hali ya hewa na kituo cha kupoza umeme. Jumla ya shilingi bilioni 36.23 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

## F. Nishati

**Miradi ya Kufua umeme**

**(i) Mradi Na. 3164: Kinyerezi I *Extension* (MW 185)**

Hatua iliyofikiwa ni: Ufungaji wa mitambo umefikia asilimia 92 ambapo mitambo mitatu kati ya minne yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 135 imewashwa na umeme unaozalishwa kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Jumla ya shilingi bilioni 30.8 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 3169: Kufua Umeme wa Maji Rusumo (MW 80)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa bwawa, handaki la kupitishia maji, kituo cha kupoza na kuchochea umeme (switchyard), jengo la utawala na nyumba 24 za kudumu; kuendelea na ujenzi wa jengo la mitambo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.89 na ufungaji wa mitambo ya kufua umeme asilimia 56. Kwa ujumla mradi umefikia asilimia 98.3. Jumla ya shilingi bilioni 8.09 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

**(i) Mradi Na. 3111: Uimarishaji wa Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization)***

Hatua iliyofikiwa ni: Kuunganishwa kwa Mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Buhigwe) pamoja na Wilaya za Ngara na Biharamulo katika gridi ya Taifa kutokea kituo cha Nyakanazi; kuendelea na ujenzi wa njia ya msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi ambao umefikia asilimia 22; na jumla ya mikataba 26 ya kutekeleza miradi ya kuimarisha Gridi ya Taifa na mikataba 14 ya usambazaji wa umeme vijijini imesainiwa. Jumla ya shilingi bilioni 9.5 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi; kukamilika kwa usimikaji wa nguzo na uunganishaji wa nyaya za umeme; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilima 97.5. Jumla ya shilingi bilioni 3.3 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(iii) Mradi Na. 3175: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha – Namanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Singida hadi Arusha; kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Arusha hadi Namanga; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo mkoani Arusha. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 92. Jumla ya shilingi milioni 153.99 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 3179: Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Kinyerezi - Dodoma**

**Awamu ya kwanza (Rufiji - Chalinze)**: Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umefikia asilimia 83 na kituo cha kupoza umeme asilimia 48. Jumla ya shilingi bilioni 48.2 zimetumika Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Awamu ya pili (Chalinze – Dodoma na Chalinze - Kinyerezi)**: Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi kati ya Kinyerezi – Chalinze na Chalinze - Dodoma; na kukamilika kwa tathmini ya athari za mradi kwa mazingira na jamii (ESIA) pamoja na upembuzi yakinifu. Jumla ya shilingi shilingi bilioni 9.42 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 - North West Grid Extension (Iringa – Mbeya - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi)**

**Awamu ya Pili (Kigoma hadi Nyakanazi):**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa asilimia 90 ya ulipaji wa fidia katika eneo la Kidahwe na eneo la mkuza wa njia ya usafirishaji umeme; kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme; kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme; kuendelea na taratibu za kuwapata wakandarasi wa vituo vya kupoza umeme vya Nyakanazi na Kidahwe pamoja na njia za usambazaji umeme. Jumla ya shilingi milioni 947.32 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi Na. 3113: Usambazaji wa Nishati Vijijini**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuunganishwa kwa jumla ya vijiji 9,467 kati ya vijiji 12,318 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 76.7. Jumla ya shilingi bilioni 125.28 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**Miradi ya Usambazaji wa Gesi Asilia**
**(i) Mradi Na. 3162: Usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuunganishwa kwa nyumba 670 katika Mkoa wa Dar es Salaam; kuunganishwa kwa kiwanda cha *Raddy Fiber Manufacturing Tanzania Ltd* (Pwani); na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia majumbani yenye urefu wa kilomita 18.3 iliyounganisha nyumba 209 katika kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi. Hadi Desemba 2022, jumla ya nyumba 1,511, viwanda 53, taasisi tisa (9) na magari 2,000 yanatumia gesi asilia. Aidha, mtandao wa usambazaji wa gesi asilia umefikia km 143. Jumla ya shilingi milioni 469.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**2.3.2.2. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi**

**A. Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**

**(i) Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge**
Hatua iliyofikiwa ni kuanza ujenzi wa nyumba mbili (2) katika eneo la Kilimani; kukamilika kwa tathmini ya mahitaji ya mitambo kwa ajili ya ulinzi na usalama; na

kukamilika kwa ujenzi wa makazi ya Katibu wa Bunge (kilimani – Dodoma). Jumla ya shilingi milioni 565.65 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa majengo ya utawala, ukumbi wa Msekwa, ununuzi na ufungwaji wa vipuri vya mtambo wa kupooza hewa katika ukumbi wa Bunge; na kukamilika kwa ukarabati wa kumbi mbili za Bunge na uzio kwa ajili ya usalama. Jumla ya shilingi milioni 341.64 zimetumika katika kipindi cha nusu ya mwaka 2022/23.

**B. Kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Utumishi wa Umma**

**Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**(i) Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John P. Magufuli ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90. Jumla ya shilingi bilioni 3.51 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6284: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo wa e-HRP na uwekaji wa ujuzi wa kila Kada katika Mfumo; kuendelea na ujenzi wa Klabu ya Viongozi iliyopo Njedengwa Dodoma ambapo utekelezaji wa umefikia asilimia 41; kuendelea na uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ambapo hatua iliyofikiwa ni kukusanywa kwa mifumo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini inayotumika Serikalini; kukamilika kwa mafunzo kwa watumiaji 232 wa Mfumo wa HCMIS katika Taasisi za Umma; kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo wa *e*-Mrejesho, kubadili Mwongozo wa Malalamiko, kuandaliwa matangazo madogo madogo ya TV na Redio na kutoa mafunzo kwa Wakuu 150 wa Taasisi kuhusu matumizi ya mfumo; na kukamilika kwa ujenzi wa Mifumo ya Kielektroniki ya PEPMIS na PIPMIS. Jumla ya shilingi bilioni 1.54 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**C. Mfuko wa Mahakama**

**(i) Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama ya wilaya ya Manyoni; na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za wilaya za Liwale ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70, Kwimba (asilimia 89) na Ulanga (asilimia 40). Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu ambapo

utekelezaji umefikia asilimia 20; na ujenzi wa jengo la ghorofa sita kwa ajili ya makazi ya Majaji jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 68. Jumla ya shilingi billioni 2.6 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tisa (9) ambapo Mahakama ya Mwanzo Madale (Dar es Salaam) utekelezaji umefikia asilimia 85, Kinesi (Rorya) (asilimia 95), Mahenge (Kilolo) (asilimia 97), Luilo (Ludewa) (asilimia 60), Newala (Newala) (asilimia 60) na Usevya (Mlele) (asilimia 95); Nyakibimbili (Bukoba) - asilimia 80, Kabanga (Ngara) - asilimia 80 na Mlimba na Mang'ula (Morogoro) - asilimia 85). Jumla ya shilingi bilioni 2.4 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 6314: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu Tabora na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi. Jumla ya shilingi milioni 370 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6215: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Mahakama (Citizen Centric Judiciary Modernisation Project)**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama za wilaya 18 za Kyerwa na Misenyi (Kagera), Mbogwe na Nyang'wale (Geita), Itilima na Busega (Simiyu), Gairo, Mvomero na Kilombero (Morogoro), Kakonko, Buhingwe na Uvinza (Kigoma), Butiama na Rorya (Mara), Songwe (Songwe), Tanganyika (Katavi), Kaliua (Tabora) na Mkinga (Tanga). Jumla ya shilingi bilioni 14.1 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**D. Utawala Bora na Utawala wa Sheria**

**(a) Mradi Na. 5501: Kuimarisha Upatikanaji wa Haki za Binadamu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwajengea uwezo watumishi 45 kutoka katika Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu uratibu na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mikataba ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza haki za binadamu nchini; na kuandaa rasimu ya mpango kazi wa pili wa kitaifa wa kulinda haki za binadamu nchini kwa kupata maoni ya pande zote mbili za Muungano wa Tanzania. Jumla ya shilingi milioni 78 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 5502: Mpango Kazi Endelevu wa Kupambana na Rushwa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kusainiwa kwa Kanuni za Sheria ya Kuwalinda Mashahidi na Watoa Taarifa za Uhalifu ili zianze kutumika; kukamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Mashtaka, Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo na kuanza kupokea maoni ya Wadau; kutolewa elimu kwa wadau 400 kutoka taasisi za fedha kuhusu elimu ya kupambana na rushwa; kuanza kwa maandalizi ya awali ya

kuanzisha Kanzidata ya kudhibiti fedha haramu na kuandaa rasimu ya Mwongozo wa Utaifishaji wa Mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu. Jumla ya shilingi milioni 367.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 5507: Upatikanaji wa Haki za Wanawake na Watoto wa Kike**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukusanyaji wa maoni ya wananchi kuhusu maboresho ya Sheria ya Ndoa Sura 29 hususan umri wa mtoto wa kike kuolewa katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Tanga. Jumla ya hilingi milioni 123 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 5508: Upatikanaji wa Haki kwa Maendeleo Endelevu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa maandalizi ya mahitaji ya mfumo wa kubadilishana taarifa miongoni mwa Taasisi za Haki Jinai; na kukamilika kwa andiko la kutungwa kwa Sera ya Adhabu. Jumla ya shilingi milioni 967 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 6201: Haki Mtandao**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwajengea uwezo washiriki 65 ambao ni Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria, Wasaidizi wa Kisheria, Wasajili Wasaidizi, na Madawati ya Huduma za Kisheria kwenye Magereza na Polisi; na kukamilisha mpango wa mawasiliano ya huduma zinazotolewa na Wizara kwa wananchi. Jumla ya shilingi milioni 225 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 6207: Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza wigo wa kuifikia Haki**

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa ukaguzi kwa Taasisi 34 za Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kutoka wilaya 27 za mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara; Kufanya maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria Mkoa wa Kigoma ambapo wananchi 4,150 (wanaume 1,617, wanawake 2,416 na watoto 117) walipatiwa huduma ya msaada wa kisheria; na kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa mahabusu na wafungwa kwa njia ya huduma ya msadaa wa kisheria inayotolewa na mawakili bila malipo (Pro Bono) katika magereza ya Segerea na ukonga ambapo jumla ya wafungwa 56 walipatiwa huduma ikiwemo wanawake 23 na Watoto 33. Jumla ya shilingi milioni 400 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 6517: Haki ya Mtoto**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa mkutano wa Jukwaa la Haki Mtoto linalohusisha wadau kutoka taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kwa ajili ya kujadiliana utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Kitaifa wa Haki Mtoto; na kufanya usajili vizazi 548,253. Jumla ya shilingi milioni 585 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

**(i) Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa Ofisi Jumuishi katika mkoa Morogoro umefikia asilimia 53; Mkoa wa Kimashtaka Ilala (Kinyerezi) umefikia asilimia 66.5; Mkoa wa Pwani (asilimia 64.1); Mkoa wa Mbeya (asilimia 54.4); na ujenzi wa Ofisi Jumuishi za Huduma za Sheria katika mikoa ya Shinyanga, Manyara, Njombe, Katavi na Sumbawanga umefikia asilimia 15. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa Ofisi Jumuishi mkoani Mwanza umefikia asilimia 38. Jumla ya shilingi milioni 396 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Ujenzi wa Majengo ya Serikali Dodoma**

Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa majengo ya Serikali ni: Kuendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo ya Wizara katika mji wa Serikali Mtumba ambapo ujenzi wa majengo 24 umefikia wastani wa asilimia 60 na ujenzi wa jengo moja (1) la Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) umefikia asilimia 50. Jumla ya shilingi bilioni 93.83 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Jengo la makao makuu Jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asimilia 76. Jumla ya shilingi bilioni 15.7 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Ofisi na Makazi ya Viongozi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa majengo 49 ya muda mrefu ya Halmashauri ambapo 9 kati ya hayo yamekamilika; kuendelea na majengo 30 kwa Halmashauri zilizohamisha Makao Makuu ambapo jengo moja la Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika limekamilika; na kuendelea na ujenzi wa majengo 30 mapya ya utawala na ujenzi wa nyumba 46 za wakurugenzi na nyumba 78 za wakuu wa idara ambapo ujenzi wa nyumba. Jumla ya shilingi bilioni 78.54 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vi) Ofisi na Makazi ya Viongozi wa Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Ikulu Ndogo katika Mkoa wa Njombe ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; Kuendelea na ukamilishaji wa nyumba za Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mkoa wa Njombe (2); kuendelea na ukamilishaji wa nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya za Momba ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya za Ludewa na Siha; Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya Kibiti ambapo uko hatua ukamilishaji; kuanza ujenzi na ukarabati wa nyumba za wakuu wa wilaya za Iramba, Mbinga, Buhigwe, Mbinga na Momba; na kuanza ujenzi wa uzio wa nyumba ya

mkuu wa Wilaya ya Same; kukamilika kwa nyumba za Makatibu Tawala wa mikoa ya Katavi na Njombe na kuanza ujenzi wa nyumba za wahudumu na vibanda vya walinzi ambazo zipo hatua za manunuzi; na kuendelea na ujenzi wa nyumba za Makatibu Tawala wa Mikoa ya Ruvuma na Songwe; na kukamilika kwa nyumba za Wakuu wa Mikoa ya Njombe na Songwe.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni: kuanza ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Kakonko, Same, Hai, Gairo, Malinyi na Ulanga; kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani; kuendelea na ujenzi wa ofisi za wakuu wa Mikoa ya Geita na Songwe ambapo utekelezaji upo hatua ya ukamilishaji; ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa wa Dodoma, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Ruvuma na Rukwa; na upanuzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida na Kilimanjaro; kuendelea na ujenzi wa ofisi za Tarafa katika Mikoa ya Kilimanjaro (8), Arusha (2), Pwani (5), Mtwara (5), Songwe (4), Katavi (3), Dodoma (3), Mwanza (11), Morogoro (5), Ruvuma (2) na Kigoma (1); na kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la Soko la kisasa la Kariakoo ambapo utekelezaji uko hatua ya kumwaga zege kwenye ghorofa ya 4. Aidha, ukarabati wa jengo la zamani unaendelea ambapo utekelezaji uko asilimia 56. Jumla ya shilingi bilioni 21.64 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 6209: Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo kusaidia ujenzi wa vituo vya afya, vyumba vya madarasa, vyumba vya maabara na miundombinu ya maji na umeme. Jumla ya shilingi bilioni 15.99 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 6580: Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

Hatua iliyofikiwa ni: ukamilishaji wa ujenzi wa Barabara zenye urefu wa kilomita 5.3 kwa kiwango cha lami; ukamilishaji wa ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua kilomita 1.8; maandalizi ya mradi wa TACTIC; na maandalizi ya uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi. Jumla ya shilingi bilioni 10.43 zimetumika hadi Desemba, 2022.

**E. Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusajiliwa na kutambuliwa kwa watu 403,386 kati yao wageni 575 na wakimbizi 49 na kufanya jumla ya watu waliosajiliwa kufikia 23,630,813 katika Mikoa na wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar; kununuliwa kadi ghafi 2,667,293 za kuzalisha vitambulisho; kuchakatwa kwa maombi na kuzalishwa kwa namba za utambulisho wa Taifa (NIN) 394,374 nakufanya jumla namba za utambulisho wa Taifa (NIN) zilizozalishwa kufikia 19,885,966; kuzalishwa na kusambazwa kwa vitambulisho 312,870 kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa kufikia 11,201,666; kuunganishwa na kuboreshwa kwa mifumo na miundombinu ya mtandao wa mawasiliano kati ya Ofisi

za Usajili za Wilaya na Makao Makuu ambapo ofisi tatu (3) zimeunganishwa na kufanya jumla ya ofisi zilizounganishwa kufikia 141; na kuunganishwa kwa Taasisi 11 katika mfumo wa Usajili na Utambuzi na kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa na mfumo kufikia 72. Jumla ya shilingi billion 3.5 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**F. Usalama wa Raia**

**(i) Mradi Na. 6302: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania Bara**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Mkuu wa Kikosi cha kutuliza ghasia Singida; kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa kutenganisha eneo la Makao Makuu ya Polisi/CID na eneo la RPC Dodoma; kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja ”C” na ujenzi wa nyumba za makazi ya askari Ludewa utekelezaji umefikia asilimia 65, kituo cha Polisi Daraja “A” katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma (asilimia 70) na kituo cha Polisi Daraja “A” Kigamboni (asilimia 99); na kuendelea na ujenzi wa nyumba 3 za kuishi Makamishna wa Polisi Jijini Dodoma umefikia (asilimia 99). Jumla ya shilingi bilioni 1.30 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(ii) Mradi Na. 6303: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Zanzibar**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha Polisi Mkokotoni Zanzibar; kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Kizimkazi ambao utekelezaji umefikia asilimia 65; na ukamilika kwa majengo manne (4) ya kuishi familia nane (8) za askari Mfikiwa Kusini Pemba. Jumla ya shilingi milioni 739.3 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**G. Uhamiaji**

**Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kukabidhiwa kwa Ofisi ya uhamiaji ya Mkoa wa Geita; kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75, Lindi (asilimia 90) na Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Dodoma (asilimia 41); kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kambi ya Mafunzo ya Uhamiaji - Boma Kichakamiba wilayani Mkinga (Tanga) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 94; na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara asilimia 68. Jumla ya shilingi bilioni 1.25 zimetumika hadi nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**2.3.2.3. Mapinduzi ya TEHAMA**

**A. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**(i) Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi mpya wa Kilomita 1,600 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vituo 15 vya kutoleo huduma za

Mkongo; kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo wa ujenzi wa mkongo wa majini kiasi cha Kilomita 60 kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika; kuendelea na kazi za upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Data Zanzibar; kuwajengea uwezo wataalam 25 wa TEHAMA juu ya teknolojia mpya zinazoibukia na masuala ya usalama wa mtandao; kukamilika kwa utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Data Protection Act, 2022); na kutoa elimu kwa umma kuhusu usalama wa mtandao kwa wananchi 453, shule za sekondari 3 (wanafunzi 968), vyuo vikuu 8 (wanachuo 656) na wananchi takriban milioni 5.2 kupitia Vyombo vya Habari (TV-9, Redio-8, magazeti-7). Jumla ya shilingi Shilingi bilioni 39.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4234: Mfumo wa Anwani za Makazi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uboreshaji wa programu ya Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi; kukamilika kwa mapendekezo ya maboresho ya sheria nne (4) za kusimamia Anwani za Makazi; kukamilika kwa mapitio ya sheria ya EPOCA na kanuni zake; kukamilika kwa uhakiki wa taarifa za miundombinu ya Anwani za Makazi pamoja na taarifa za makazi zilizokusanywa katika Operesheni Anwani za Makazi kwenye Halmashauri 12, ambazo ni Majiji ya Dodoma, Arusha, Mbeya na Tanga, Manispaa za Mjini, Magharibi A, Magharibi B na Moshi pamoja na Halmashauri za Kaskazini A, Kaskazini B, Kusini na Kati; kutoa elimu kwa umma kuhusu Anuani za Makazi kwa wafanyabiashara 166 wa Mkoa wa Dodoma, watumishi 80 kutoka Wizara za Kisekta na watanzania takribani milioni 4.5 kwa kupitia vyombo vya habari; na kutungwa kwa Kanuni ndogo za Anwani za Makazi ambazo zimetumika katika kutekeleza mradi wa Anwani ya Makazi. Jumla ya shilingi bilioni 7.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusainiwa kwa mkataba na Mshauri Mwelekezi wa kusanifu na kusimamia ujenzi wa Taasisi ya TEHAMA na vituo vitano vya Ubunifu vya kikanda; kuboreshwa kwa miundombinu ya intaneti yenye kasi (broadband) na kuunganisha taasisi 18 kwenye mtandao wa Serikali; kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya vituo vya huduma pamoja utakaosaidia kurahisisha utendaji kazi wa vituo hivyo (Business Process re-engeering); kusainiwa kwa mkataba baina ya Wizara na Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya usanifu wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS); kuanza kwa taratibu za manunuzi kwa ajili ujenzi wa minara ya mawasiliano 388 kwenye Kata 388 ili kuwezesha huduma za mawasiliano nchini; kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanya mapitio ya sera na sheria zinazosimamia TEHAMA; na kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini kwa kuwapatia watalaam 17 mafunzo ya muda mfupi. Jumla ya shilingi bilioni 10.26 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 4279: Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania**

**(TBC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa studio za redio (TBC Taifa na TBC FM) na za ukombozi wa Nchi Kusini mwa Afrika katika jengo la utangazaji barabara ya Nyerere; kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya TBC Jijini Dodoma; kulipia haki za kuonesha mashindano ya kombe la dunia; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa michoro na mifumo kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la Kituo cha Taifa cha Televisheni (TVT) litakalotumika kwa ajili ya Chaneli ya Utalii ya Tanzania Safari. Jumla ya shilingi bilioni 1.95 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa na kurushwa kwa vipindi ishirini (20) vya Televisheni vinavyohusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1); kuratibu mikutano ya Taasisi za Serikali 37 katika kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli zake kwa umma kupitia vyombo vya habari; na kukamilika kwa malipo ya kifaa cha kurushia matangazo mubashara aina ya Live U. Jumla ya shilingi milioni 420.8 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha Kupiga Chapa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 79. Jumla ya shilingi bilioni 1.09 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa mtambo wa uchapaji ambapo jumla ya shilingi milioni 809.59 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(viii) Mradi Na. 6226: Kujenga Kituo Kikuu cha Kuendeleza Ubunifu wa TEHAMA na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Sekta ya TEHAMA Nchini**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi kwa ajili ya kufanya matengenezo na maboresho ya jengo la TEHAMA ziko katika hatua za ukamilishaji; kujenga uwezo kwa wabunifu na watengeneza bidhaa za TEHAMA 63 wa kanda ya Dar es Salaam juu ya namna bora ya kukuza bunifu zao ili ziweze kutoa ajira na kuchangia pato la Taifa; na kukamilika kwa matengenezo ya Portal ya wataalamu wa TEHAMA. Jumla ya shilingi milioni 500 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

### 2.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

#### 2.3.3.1.Uzalishaji Viwandani

**(i) Mradi Na. 6103: Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utafiti wa gari la Deraya (Armoured Personnel Carrier – APC) na *reverse engineering* ya vipuri vitano (5) vinavyotumika katika magari ya kuzima moto; kununuliwa kwa mashine za kupima ubora wa bidhaa za utafiti na uzalishaji; kukamilisha usimikaji wa mashine za *metal forming* za kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma zisizoshika kutu; kuendelea na ukarabati wa jengo litakalosimikwa vinu vya *metal galvanization* ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85; na kuwajengea uwezo wataalamu 43 katika fani za utafiti, ubunifu na utengenezaji wa magari na mitambo, mipango, ufundi stadi, masoko, TEHAMA, na ugavi. Jumla ya shilingi bilioni 8.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4486: Uzalishaji Viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na mapitio ya mikakati ya sekta ndogo za nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi; kuanza kwa uandishi wa mkakati wa bidhaa za nguo na mavazi; kuendelea kufanya tathmini ya uzalishaji wa magunia ya mkonge na biashara ya magunia ya jute; na kuendelea na ukamilishaji taratibu za umiliki wa ardhi yenye ukubwa wa ekari 62 iliyoko Kahama mkoani Shinyanga. Jumla ya shilingi milioni 633.08 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4948: Kuimarisha Uzalishaji Viwandani kupitia Uboreshaji wa Ubora na Tija - KAIZEN**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuongezeka kwa idadi ya waratibu wa KAIZEN viwandani kutoka 200 hadi kufikia 230 pamoja na idadi ya viwanda vilivyonufaika na huduma hii kutoka 135 ya hadi kufikia 150; kungezeka kwa idadi ya mikoa iliyofikiwa na huduma za KAIZEN kutoka 8 hadi 12 ambapo takribani viwanda 16 vimenufaika na mafunzo na kufanikisha kuongeza wakufunzi 36 wapya; na kufanyika kwa mafunzo kwa washiriki 20 kutoka Unguja na 70 kutoka Pemba.

**(iv) Mradi Na. 6260: *Institutional Support***

**(a) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uundaji wa mashine za kiwanda darasa cha kubangua Korosho (Manyoni) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; kukamilika kwa utafiti wa kubaini mahitaji ya zana za kilimo, mifugo, uvuvi na teknolojia za vijijini kwa wakulima wa Wilaya za Momba (Songwe) na Chemba (Dodoma); kuendelea na ukarabati wa majengo mawili (2) ya Utawala (Block A na Block B) na nyumba mbili (2) za watumishi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85; na kufanyika kwa

majaribio na kuthibitishwa kwa jumla ya aina 46 ya zana za kilimo na teknolojia vijijijni. Jumla ya shilingi milioni 873.8 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ununuzi na usimikaji wa mashine ya *overhead crane*; kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya tanuru ikiwemo *Induction furnace*; kukamilika kwa ujenzi wa msingi na kuendelea na usimikaji wa kinu cha kuyeyushia chuma (induction furnace) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; na kukamilika kwa ukarabati wa mfumo wa umeme. Jumla ya shilingi milioni 760.95 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO**

Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa Mita 400 (China boda road); na kukamilika kwa usimikaji wa bango ili kuzuia wavamizi. Jumla ya shilingi milioni 28.7 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi wa kuunganisha Matrekta ya URSUS**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kufanya mazungumzo na Serikali ya Poland kupitia Wawakilishi wa Timu Maalum ya Serikali ya Majadiliano (GNT); na kuendelea kufuatilia madeni kwa wakulima (716) waliokopa matreka hayo. Jumla ya shilingi milioni 200.00 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Kongane la Viwanda Nyanza**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa ghala Na. 1 na kuendelea na ukarabati wa ghala Na. 2 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10. Jumla ya shilingi milioni 84.1 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi wa kiwanda cha Viuadudu (TBPL)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa jaribio la pili la viwatilifu; kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya ndani (Viuatilifu Road) yenye urefu wa mita 230. Jumla ya shilingi bilioni 1.24 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji taarifa za tathmini ya viwanda na kuanisha fursa za Uwekezaji katika Kanda ya Kaskazini; kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala ili kutoa nafasi ya kuanzisha kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashari wa teknolojia na viatamizi kwa wabunifu wa teknolojia ambapo ujenzi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi milioni 406.13 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa unakiri na kufanya maboresho ya mchoro wa mtambo wa kuchakata mkonge uliopo Tanga; kuendelea na utafiti wa teknolojia ya kutengeneza matofali yanayohimili joto kali kwa awamu ya pili; kukamilika kwa mitambo midogo minne (4) ya sukari; kuendelea na usanifu wa kuendeleza teknolojia ya kuhifadhi maziwa wakati wa kukusanya na kusafirisha ili yasiharibike mapema na usanifu wa teknolojia ya kuhifadhi mazao ya mboga mboga kwenye ubaridi (cold rooms for small holder hortculture farmers); kuendelea na maboresho ya karakana ya kukata na kukunja vyuma kwa kuunganisha umeme mkubwa; kukamilika kwa utengenezaji wa vifaa tiba (vitanda drip stand, examination bed, delivery bed, theatre trolleys, hospital screens, bed side lockers, biomedical waste incinerators na milango ya kuzuia mionzi).

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuendelea na usanifu wa Mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospitali mahususi kwa kuchomea damu isiyofaa, mabaki ya wanyama na dawa zilizoharibika na kupitwa muda; kuendelea na utafiti na usanifu wa mtambo wa kukausha korosho pamoja na teknolojia ya mtambo wa kuchakata chikichi ili kuongeza thamani; kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wahandisi 15, mafundi sita (6) mafundi sanifu wawili (2) na watumishi nane (8) wasio kwenye kada za ufundi; kutoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vya KDT Company Ltd (Arusha), Twiga Cement Company Ltd (Dar es salaam) na Good will Company Ltd (Pwani). Jumla ya shilingi milioni 998.00 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(i) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo (SIDO)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa michoro ya majengo ya viwanda (industrial sheds) katika Mkoa wa Iringa na ukarabati katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Tabora na kumalizia jengo la Nyasa Mkoa wa Ruvuma; kuendelea na ujenzi wa majengo ya viwanda katika mikoa ya Tanga (1); Singida - Manyoni (1), Shinyanga – Kahama (2) na Geita - Chato (2); kuandaliwa kwa vipimo vya Mashine ya kukeleza vyuma, kukata na kukunja mabati, kuchomelea na kukata vyuma kwa ajili ya kuimarisha Kituo cha Uendelezaji Teknolojia (TDCs) katika mkoa wa Arusha; kuagizwa kwa mashine ya kukeleza vyuma, kukata na kukunja mabati, kuchomelea na kukata vyuma kwa ajili ya kuimarisha vituo vya Uendelezaji Teknolojia katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mbeya; kuzalishwa kwa mashine 228 na vipuli 1,374 za aina mbalimbali kupitia Vituo saba (7) vya kuendeleza Teknolojia (TDCs) kwa ajili ya viwanda vidogo; na kutolewa mafunzo kwa wafanyakazi wa SIDO kuhusu utumiaji wa mfumo wa ofisi mtandao. Jumla ya shilingi milioni 172.99 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(j) Mchango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Katika Uchumi wa Viwanda**

**Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd (KLICL)**
Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata ngozi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45, maabara na kantini (asilimia 99), Jengo la Jenereta (asilimia 99) na barabara za ndani na mitaro ya maji ya mvua (asilimia 50) ambapo utekelezaji wa jumla wa mradi umefikia asilimia 95; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo maji taka, barabara za ndani na uzio katika kiwanda cha ngozi. Jumla ya shilingi bilioni 122 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills Ranch - Morogoro**
Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa majengo, mifumo ya umeme na maji, majokofu ya upoozaji, uunganishaji wa umeme mkubwa na ufungaji wa mashine pamoja na majaribio ya mashine na mifumo ya uendeshaji. Jumla ya shilingi bilioni 20.35 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi cha ‘Mamba Ginger Factory Limited**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa majengo ya kiwanda; unganishaji wa umeme mkubwa na ufungaji wa mashine, majaribio ya mashine na mifumo ya uendeshaji. Jumla ya shilingi bilioni 1.782 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**Kiwanda cha Chai cha Mponde - Tanga**
Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa majengo, mitambo, mifumo ya umeme na maji pamoja na majaribio ya mitambo. Jumla ya shilingi milioni 500 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(v) Mradi Na. 4933: Uendelezaji wa Kanda Maalumu za Kiuchumi**

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Mtwara Free Port Zone**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara za ndani ya eneo la mradi zenye urefu wa km 1.06; na kukamilika kwa usanifu wa jengo la Kituo cha Pamoja cha Huduma (One Stop Center Building).

**2.3.3.2.Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II**

**A. Kilimo**

**(a) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II**

**(i) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa skimu mpya 14 zenye ukubwa wa hekta

34,284 Msesule (Kyela), Mkombozi LOT I (Iringa), Mkombozi LOT II (Iringa), Mkombozi LOT III (Iringa), Mkombozi LOT IV (Iringa), Membe (Chamwino), Kongogo (Bahi), Tlawi (Mbulu), Endagaw (Hanang'), Rudewa (Kilosa), Ulyanyama (Sikonge), Lyamalagwa (Nzega), Maguru Kenda – Sukuma (Buchosa) na Mahiga (Kwimba) zenye jumla ya hekta 34,284; kuanza kwa ukarabati wa skimu za umwagiliaji 15 zenye ukubwa wa hekta 16,646 za Mbaka (Busokelo), Uturo- Isenyela (Mbarali), Matebete (Mbarali), Gonakuvagogolo (Mbarali), Herman (Mbarali), Madibira (Mbarali), Mtula (Mafinga), Mgambalenga (Kilolo), Myamba (Same), Kirya (Mwanga), Mgongola (Mvomero), Idete (Kilombero), Idudumo (Nzega), Muhukuru (Nsimbo) na Idudumo (Nsimbo); Kuanza ujenzi wa mabwawa nane (8) yenye ujazo wa jumla ya mita za ujazo 113,170,000. Mabwawa yanayojengwa ni Ulyanyama (Tabora), Tlawi (Mbulu), Katunguru (Sengerema), Membe (Chamwino), Kasoli (Bariadi) na Nyida (Shinyanga). Jumla ya Wakandarasi 21 wameajiriwa katika miradi hiyo ambapo wakandarasi 19 sawa na asilimia 90.5 ni makampuni ya Tanzainia na Kampuni 3 sawa na asilimia 9.5 ni kampuni za nje ya nchi. Aidha, jumla ya ajira 1,650 zimezalishwa katika miradi hii. Jumla ya shilingi bilioni 26.7 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Kuwezesha Uanzishwaji wa Mashamba Makubwa ili kuwa Kitovu Cha Teknolojia Bora kwa Wakulima Wadogo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kubainisha mashamba makubwa (Block farms) yenye ukubwa wa ekari 183,012 kwa ajili ya vijana katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Kagera na Kigoma; kwa kushirikana na Halmashauri za Wilaya ya Chamwino na Bahi imekamilisha upimaji wa mashamba ya (ekari 11,453), Membe (ekari 8,000) na Ikumbulu Bahi (ekari 3,600); kupimwa kwa afya ya udongo wa mashamba hayo na kusafishwa kwa ekari 1,300 za shamba la Mlazo-Ndogowe; kusafishwa kwa Shamba la Chinangali lenye ukubwa wa ekari 400 kwa ajili ya uwekezaji; kusafishwa kwa shamba lenye hekta 30 la Kituo cha Mafunzo ya Wakulima Bihawana na kugawanywa katika vizimba (Blocks). Aidha, vijana 812 wamedahiriwa kwa ajili ya kupewa mafunzo katika vyuo vya kilimo kuanzia mwezi Machi, 2023 kabla ya kupewa ardhi ya kilimo. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Kuimarisha Vituo vya Utafiti na Utafiti wa Mbegu Bora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za TARI Makao Makuu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 18; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha TARI Kihinga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45; kuanza kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye jumla ya hekta 854 za vituo 16 vya utafiti; kujenga ghala tano (5) zenye vyumba vya ubaridi (cold rooms) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,075 za mbegu katika vituo vya TARI Selian, Hombolo, Tumbi, Naliendele na Dakawa; na kuanza ujenzi wa uzio katika eneo la kituo cha TARI Uyole lenye hekta 1,042; kununua vifaa na vitendanishi vya maabara ya udongo na bioteknolojia za TARI Mlingano na TARI Mikocheni; kufanya ugunduzi wa teknolojia mbalimbali kwa

kukamilisha mapendekezo ya kupitisha aina 15 za mbegu mpya kwa Kamati ya Kitaalam ya Mbegu ambapo 7 ni za maharage, 3 za mtama, 5 za zabibu, na 2 za zao la mgomba; kutunza vinasaba 33,332 vya mazao ya mpunga (729), mtama (416), uwele (105), ulezi (3), alizeti (39), zabibu (26), migomba (128), maharage (10), muhogo (20), korosho (30,000), pamba (328), mahindi (250), viazi vitamu (6), miwa (107), minazi (7), michikichi (3), mkonge (60), na kakao (17) kwa ajili ya utafiti na uhifadhi wa mbegu za asili; kukusanya aina 337 za mbegu za asili za mpunga na mboga (312 mpunga na 25 mboga), kusafisha na kuanza kuzalisha aina 20. Jumla ya shilingi bilioni 5.46 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(iv) Kuimarisha Huduma za Ugani, Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

**(a) Ukarabati wa Vyuo vya Kilimo na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

Hatua iliyofikiwa ni: Kudahiliwa kwa wanafunzi 3,115 wa mwaka wa kwanza na wa pili katika vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo; na kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya Kilimo Tumbi, Igurusi, Ilonga na NSI. Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Kuimarisha Huduma za Ugani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuboresha mazingira ya utoaji huduma kwa kununua na kusambaza pikipiki 3,500 kwa maafisa ugani katika mikoa 15; Kununua na kusambaza viti 1,020 na meza 23 katika Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) nane (8) katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu; Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 345 na wakulima 142 kuhusu matumizi ya vifaa vya kupima afya ya udongo; na kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 203 kuhusu kilimo biashara na matumizi ya mfumo wa M – Kilimo. Jumla ya shilingi bilioni 10.59 zimetumika hadi Machi, 2023.

**(c) Upatikanaji wa Mbegu Bora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuzalishwa na kusambazwa kwa bei ya ruzuku tani 1,004 za mbegu bora za Alizeti kwa wakulima katika wilaya 39 za mikoa ya Dodoma, Kagera, Mbeya, Mwanza na Singida. Kati ya kiasi hicho, tani 300 zimezalishwa na Sekta Binafsi; kuzalisha miche 90,000 ya parachichi na miche 94,908 ya chikichi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Kilimi (Nzega) lenye ukubwa wa hekta 400, Arusha (hekta 200) na Msimba (Kilosa) hekta 200 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25.0; kukamilika kwa upimaji wa maji (geological survey) na kutambua maeneo sita (6) ya kuchimba visima katika shamba la Arusha; kukamilika kwa uchimbaji wa visima virefu sita (6) katika shamba la mbegu la Msimba; kuongeza eneo jipya la hekta 1,300 kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora katika mashamba ya Kilimi - Nzega (hekta 300), Msimba - Kilosa (hekta 400), Mwele - Tanga (hekta 300) na Namtumbo - Ruvuma (hekta 300); kuendelea na ukarabati wa ghala la kuhifadhi mbegu la msimba ambao umefikia asilimia 90 na

usimikaji wa mtambo mpya wenye uwezo wa kuchakata tani 3 za mbegu kwa saa katika ghala hilo umefikia asilimia 85; ununuzi wa matrekta sita (6) na zana zake kwa ajili ya mashamba ya Msungura, Namtumbo, Msimba, Dabaga, Mbozi na Kilimi na ununuzi wa magari matatu (3) ya kusambaza mbegu. Jumla ya shilingi bilioni 15.4 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Upatikanaji wa Mbolea ya Ruzuku**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa ruzuku ya mbolea tani 297,599.18 kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini; kufanyika kwa usajili wa waingizaji wakubwa wa mbolea 28, mawakala wadogo 3,141 pamoja na wazalishaji wa ndani watatu (3) wa mbolea katika mfumo wa kielektroniki; na kufanyika kwa usajili wa wakulima kwenye mfumo wa kielektroniki 2,756,610.

**(e) Upatikanaji wa Viuatilifu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa viuatilifu lita 47,992 vya kudhibiti visumbufu vya milipuko ya viwavijeshi; na kutoa mafunzo ya matumizi salama na sahihi ya viuatilifu kwa wakulima, wafanyabiashara, maafisa ugani, na wanyunyiziaji katika Kanda ya ziwa (Mwanza na Mara), Kanda ya nyanda za juu kusini (Mbeya na Iringa), Kanda ya mashiriki ( Morogoro), Kanda ya kusini (Lindi na Mtwara) na Kanda ya kaskazini (Arusha). Jumla ya shilingi bilioni 2.97 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Kuimarisha Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa ghala tano (5) ambapo utekelezaji katika ghala la Litisha umefikia asilimia 97.67, Lipaya (asilimia 21.58), Liula (asilimia 36.62), Hangangadinda (asilimia 57.80) na Lilondo A (asilimia 33.32) katika halmashauri za Songea na Madaba; na kukamilika kwa ukarabati wa vihenge 22 na ghala tatu (3) katika mkoa wa Arusha. Jumla ya shilingi milioni 67.74 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA na Bodi ya Mazao Mchanganyiko kununua tani 18,294.314 za chakula (mahindi tani 17,257.857 na mtama tani 1,036.457); na kuendelea na maandalizi ya kuanzisha mnada wa chai kwa njia ya mtandao ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 90. Jumla ya shilingi bilioni 16.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Kuboresha Mifumo ya Kitaasisi, Bodi na Sheria**

**(a) Mifumo ya Kielektroniki ya kutoa huduma katika Sekta ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kutumika kwa Mfumo wa M-Kilimo kwa kutoa huduma ya ushauri wa kilimo bora cha mazao mbalimbali ikiwemo kujibu kero zinazohusu utoaji

wa mbolea ya ruzuku kwa wadau wa kilimo 4,548; kusajiliwa kwa wakulima 2,756,610 katika Mfumo wa Kielektroniki wa utoaji wa mbolea ya ruzuku; kuendelea na matumizi ya mfumo wa kutoa huduma za biashara ya mazao (Agriculture Trade Management Information System - ATMIS) ambapo jumla ya wakulima 500 wamesajiliwa na kupata huduma.

**(b) Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji katika Sekta ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupungua kwa riba ya mkopo kwa wakulima na kuwa chini ya asilimia 10; na kukamilika kwa mapitio ya sera ya mikopo katika mifuko ya pembejeo ambapo hatua za uidhinishwaji zinaendelea. Jumla ya shilingi milioni 17 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vi) Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Ushirika**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha TANECU (Newala) cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 za korosho kwa mwaka; na kusajiliwa kwa vyama viwili (2) vya ushirika katika vikundi vidogo vya wakulima 120 wa mazao ya mboga na matunda katika mikoa ya Arusha, Mbeya na Njombe. Jumla ya shilingi bilioni 6.3 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4499: Kudhibiti Sumukuvu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa ghala 14 katika mikoa 10 ya Kigoma, Mtwara, Dodoma, Mwanza, Ruvuma, Tabora, Manyara, Geita, Simiyu na Morogoro yenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,500 za mahindi na karanga ambapo utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 87; kuendelea na ujenzi wa Kituo Mahili cha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka (Postharvest Centre of Excellence for Grains) katika Wilaya ya Kongwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 48; kuendelea na ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Magonjwa ya Mimea (Biological Control Unit) Kibaha mkoani Pwani ambapo umefikia asilimia 98; kutoa mafunzo kwa vijana 420 kupitia Chuo cha Mafunzo ya Ufundistadi (VETA) kuhusu utengenezaji wa vihenge vya chuma kwa ajili ya kuhifadhi mazao vijijini; kutoa mafunzo kwa wakulima 60,000 na wafanyabiashara 500 kuhusu udhibiti wa Sumukuvu. Jumla ya shilingi Bilioni 29.528 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(c) Mradi Na. 4497: Kuongeza Uhifadhi wa Nafaka**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa vihenge (20) na maghala (4) katika wilaya za Babati, Mpanda na Sumbawanga; kuendelea na ujenzi wa vihenge 36 na ghala nne (4) kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kufikia tani 501,000 katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma ambapo umefikia wastani wa asilimia 85. Jumla ya shilingi milioni 649.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4427: Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - AFDP**

Hatua iliyofikiwa: kutolewa kwa mafunzo maalum ya kisayansi ya muda mfupi kwa watafiti 21 (breeders) kuhusu teknolojia ya mbegu kwenye mazao ya mahindi, maharage, alizeti na kunde; kukamilia kwa EIA katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya Msimba (Kilosa), Kilimi (Nzega), ujenzi wa maabara ya mbegu Morogoro na katika mashamba ya utafiti ya TARI; na kufanyika kwa usanifu wa ujenzi wa ofisi na ukumbi wa mafunzo, ghala za kuhifadhi mbegu, karakana na nyumba za wafanyakazi katika shamba la Kilimi (Nzega) na Msimba (Kilosa). Jumla ya shilingi Bilioni 1.15 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**B. Mifugo**

**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

**(i) Kuimarisha Afya ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa majosho 97 na kuendelea na ujenzi wa majosho 160 katika mikoa 25; kununuliwa kwa lita 52,560 za dawa ya kuogesha mifugo na kusambazwa katika mikoa 25 ya Tanzania Bara na mashamba ya Wizara na Taasisi zake; na kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 84,259,375 za chanjo dhidi ya magonjwa ya Mdondo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Homa ya Mapafu ya Mbuzi, Kimeta, Chambavu, Mchanganyiko wa Kimeta na chambavu na Kutupa Mimba. Jumla ya shilingi bilioni 8.23 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Kuimarisha Huduma za Ugani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa magari 13 kwa ajili ya uratibu wa ugani na pikipiki 1,200 kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 184; kupatiwa mafunzo rejea kwa maafisa ugani 487 wa sekta ya umma na 28 wa sekta binafsi; na kuendelea na taratibu za uanzishaji wa mashamba darasa ambapo tathmini ya uanzishwaji wa mashamba darasa ya ufugaji kuku imefanyika katika mikoa ya Ruvuma, Kilimanjaro, Shinyanga na Simiyu.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kutolewa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 580 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 119; kukamilika kwa ujenzi wa mabanda 24 kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo katika Vituo Atamizi vya Uwekezaji vya Vijana vya Mabuki (3); Buhuri Tanga (2); TALIRI Tanga (1) na Kikulula (2); kukamilika kwa ujenzi wa visima viwili (2) vya maji na miundombinu ambata katika Kituo cha TALIRI Tanga na Mabuki; kuandaliwa kwa shamba lenye ukubwa wa ekari 56 la malisho bora kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo katika Vituo Atamizi. Jumla ya shilingi bilioni 1.17 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Kuimarisha Huduma za Tafiti**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa vifaa shamba vikiwemo matrekta (4), *disc plough* (3), *harrow* (2), *bailer* (1) na *forage chopper* (1) kwa ajili ya kuwezesha utafiti wa mifugo hususan utafiti wa malisho na kusambazwa katika Vituo vya Utafiti vya TALIRI Tanga, Kongwa, Mabuki, Uyole na Mpwapwa; na kununuliwa kwa mbuzi majike 200 aina ya newala na madume 5 aina ya boer kwa ajili ya shughuli za kitafiti katika kituo cha utafiti Naliendele. Jumla ya shilingi milioni 411.75 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Uboreshaji wa Mbari kwa ajili ya Uzalishaji wa Maziwa na Nyama**

Hatua iliyofikiwa ni; na kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 84,259,375 za chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mifugo. Vilevile, jumla ya michovyo 668,000,278 ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe 398,227,019, mbuzi 138,000,211, kondoo 190,207,248 na punda 58,434,200; kununuliwa kwa hereni 150,000 kwa ajili ya kuwavalisha ng'ombe watakao himilishwa katika kambi; kununuliwa kwa mitamba 807 na kusambazwa katika Mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba ya Mabuki (500) na Sao Hill (307); kununuliwa kwa madume bora 200 ya ng'ombe na kusambazwa kwa wafugaji kupitia vikundi 100 vya Wafugaji katika Halmashauri nne (4) za Chamwino (50), Msalala (50), Maswa (50) na Chato (50); na kuzalishwa kwa mitamba 484 katika mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba. Jumla ya shilingi bilioni 2.36 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Mifugo na Mazao Yake**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa minada mitano (5) ya Msomera – Tanga (asilimia 85), Mkongeni – Morogoro (asilimia 30), Majimoto - Katavi (asilimia 10), Utengule – Mbeya (asilimia 15), Randa – Mara (asilimia 10); na kuendelea na ujenzi wa vituo 10 vya kukusanyia maziwa vya Kwemakame na Msomera – Tanga, Malimbika - Dar es Salaam, Magogoni – Morogoro, Lukani – Kilimanjaro, Ngaramtoni – Arusha, Komunge – Mara, Maswa – Simiyu, Karagwe – Kagera na Mkambako – Njombe ambapo wakandarasi wanaendelea na ujenzi.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa minada mitano (5) ya upili ya Weruweru – Kilimanjaro ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20, Mhunze – Shinyanga (asilimia 50), Meserani (asilimia 20), Wasso na Themi – Arusha (asilimia 35); kuendelea na ukarabati wa minada 13 ya awali kwa ajili ya kuipandisha hadhi kuwa minada ya upili ambapo utekelezaji katika mnada wa Nyanguge umefikia asilimia 85, Bungulwa – Mwanza (asilimia 70), Lugodalutale – Iringa (asilimia 10), Lupa – Mbeya (asilimia 90), Soya (asilimia 8) na Huzi (asilimia 5) – Dodoma, Kibinda – Simiyu (asilimia 70), Nzoka – Songwe (asilimia 90), Kilyamatundu – Rukwa (asilimia 30), Sikonge (asilimia 70) na Urambo (asilimia 80) – Tabora na Bukombe (asilimia 9) na Kasamwa - Geita. Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vi) Kuimarisha Unywaji wa Maziwa Shuleni**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa rasimu ya Mpango Mkakati wa Unywaji Maziwa Shuleni; na kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya mzabuni kwa ajili ya utengenezaji wa vituo nane (8) vya unywaji maziwa vya Morogoro (4) na Mbeya (4). Jumla ya shilingi milioni 35.7 fedha za nje zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vii) Kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa ya Kimambi na Matekwe – Lindi, na Mhanga (Singida); kukamilika kwa uchimbaji wa kisima cha Matanzi (Pwani), Makatapola (Iringa) na Lwami (Kilimanjaro); na kuandaliwa kwa jumla ya hekta 175 za shamba la mbegu za malisho na malisho.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mabwawa 11 ya Oloirieni ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10, Naalaram (asilimia 30) – Arusha, Kwekikwembe (asilimia 25) na Msomera (asilimia 35) – Tanga, Kongwa – Morogoro (asilimia 10), Vinyenze – Pwani (asilimia 10), Chang'ombe – Mbeya (asilimia 10), Kihumbo (asilimia 20) na Bukabwa (asilimia 10) – Mara, Kaiwang (asilimia 5), Leralumo (asilimia 5) – Manyara na Msaginia – Katavi (60%); kuendelea na uchimbaji wa kisima cha Muhukulu Lilai (Ruvuma) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70, Kitaraka – Singida (asilimia 5), Kapele - Kasinde – Songwe (asilimia 5) na Maswa – Simiyu (asilimia 5); shughuli za kuingiza umeme na ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji katika shamba la kuzalisha malisho na mbegu za malisho la Langwira umefikia asilima 80; kununuliwa kwa tani 8.555 (Rhodes na Buffel tani 6.105, J*uncao* tani 2.45) za mbegu za malisho na vipando vya miti malisho 18,025 kutoka mashamba ya Serikali na binafsi na kusambazwa kwa wafugaji walioandaa vikundi vya uanzishwaji wa mashamba darasa 100 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 44; na kusajiliwa kwa maeneo 156 ya kuzalisha vyakula vya mifugo (22), kuuzia (66), kuhifadhia (23), wauzaji nje ya nchi (23) na waingizaji wa rasilimali za vyakula vya mifugo (22) katika mikoa 20. Jumla ya shilingi milioni 411.3 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(viii) Kuboresha Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara zenye uwezo kuchukua wanafunzi 240 kila moja katika kampasi za Mpwapwa na Morogoro ambapo ujenzi umefikia asilimia 30. Jumla ya shilingi milioni 400 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

## C. Uvuvi

### (a) Mradi Na. 4701: Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth – SWIOFish)

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika kituo cha TAFIRI - Dar es Salaam; na kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala la ofisi ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu - Mafia ambapo ujenzi umefikia asilimia 90. Jumla ya shilingi bilioni 3.49 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II)**

**(i) Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa ofisi moja (1) ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi ya Busega (Simiyu); kuendelea na ujenzi wa ofisi mbili (2) za ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi za Nyakalilo (Sengerema) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60 na Sota – Rorya (asilimia 50); na kununuliwa kwa pikipiki 50 za maafisa ugani wa uvuvi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Jumla ya shilingi milioni 785.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23 .

**(ii) Kujenga na Kuimarisha Miundombinu ya Uvuvi (Mialo na Masoko)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi ya mialo miwili (2) ya Chifunfu/Kijiweni (Sengerema) na Igabiro (Bukoba) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 kwa kila mwalo.

**(iii) Kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati mdogo wa nyumba tatu (3) za wafanyakazi katika Kampasi ya Nyegezi (Mwanza) na Mbegani (Bagamoyo); kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara katika Kampasi ya Nyegezi (Mwanza) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75, ujenzi wa maabara umefikia asilimia 60 na ukarabati wa kitotoleshi katika Kampasi ya Gabimori – Mara (asilimia 15) na ujenzi wa maabara katika Kampasi ya Mikindani – Mtwara (asilimia 45).

**(iv) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utafiti wa uwingi, bioanuwai na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika ambapo jumla ya aina 7 za samaki na sampuli 639 zilikusanywa na kusafirishwa kwenda Uingereza; kufanya utafiti wa majaribio ya matumizi ya mitego/vyungu katika uvuvi wa pweza Tanzania ili kuwezesha uvuvi endelevu wa pweza. Jumla ya shilingi milioni 599.2 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II ) na Mradi Na. 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi**

**Kujenga na Kukarabati Miundombinu ya Ukuzaji Viumbe Maji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa mabwawa makubwa matatu (3) na madogo sita (6) kwa kuotesha nyasi na kujenga mifumo ya kuingiza na kutoa maji

katika Kituo cha Rubambagwe (Geita); kukamilika kwa matanki ya maabara (Lab tank), *nursery ponds, reservoir* na *tower* pamoja na kuendelea na ujenzi wa Kitotoleshi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60 katika kituo cha kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Bahari Ruvula – Mtwara; kuendelea na upanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji na ujenzi wa ghala moja (1) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; kuendelea na ujenzi wa Kitotoleshi cha vifaranga vya samaki na upanuzi wa kituo cha Ruhila (Songea) utekelezaji umefikia asilimia 22; kuendelea na ujenzi wa kitotoleshi, ukarabati na upanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Nyengedi – Lindi (asilimia 25); na kuendelea na ujenzi wa mashamba darasa sita (6) ya Ufugaji wa Samaki katika Halmashauri za wilaya za Kongwa, Iringa, Njombe, Songea, Tandahimba na Ruangwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15.

Kadhalika, Serikali imetoa mafunzo kwa vitendo yanayojulikana kama ATAMIZI kwa vijana 200 wanaojishughulisha na uvuvi pamoja na ukuzaji viumbe maji, ili kuzalisha vijana watakaoshiriki katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi na utoaji wa huduma za ugani. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana kujifunza kwa vitendo uvuvi na ukuzaji viumbe maji wenye tija unaoendana na mabadiliko ya teknolojia na uhitaji wa soko na kuongeza fursa za ajira kwa vijana. Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za ununuzi wa boti za uvuvi **118** ikiwa ni awamu ya kwanza ya ununuzi wa boti **160** zilizotarajiwa kununuliwa kwa ajili ya kukopesha wavuvi.

Jumla ya shilingi bilioni 1.12 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4703: Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa Jengo la Utawala la RAS MKWAVI (Block B); na kuandaa na kuhuisha *Bussiness Model* na Mpango wa Biashara wa miradi itakayotekelezwa na Shirika. Jumla ya shilingi milioni 29.1 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23**.**

#### 2.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia

**(i) Mradi Na. 1119: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (Sustainable Management of Mineral Resources Project - SMMRP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vitatu (3) vya umahiri vya Songea, Chunya na Mpanda; kununuliwa na kusimikwa (commissioning) kwa vifaa vya utafiti wa jiosayansi na vifaa vya maabara na uchunguzi kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania – GST; na kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba choronge *(core shed)* eneo la Kizota - Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 75. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kununuliwa kwa mawe mawili (2) makubwa ya

madini ya Tanzanite yenye jumla ya uzito wa kilo 5.22 na thamani ya shilingi bilioni 2.24 kutoka kwa mchimbaji mdogo.

**(ii) Mradi Na. 1120: Kituo cha Jemolojia Tanzania (Tanzania Geomological Centre)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwawezesha watumishi tisa (9) wa Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu kuhusu masuala ya uongezaji wa thamani madini. Jumla ya shilingi milioni 716.34 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

#### 2.3.3.4. Huduma

**A. Maliasili na Utalii**

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asimilia 57.7; kuongezeka kwa idadi ya watalii wa ndani kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 199.5; kuimarika kwa utalii wa urithi wa utamaduni na malikale; kupungua kwa ujangili na uvunaji haramu wa maliasili; na kuongezeka kwa udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu ambapo jumla ya vituo vya askari 16 zimejengwa.

**(a) Mradi Na. 5203: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)**

Hatua iliyofikiwa ni: ununuzi wa malori 44 kwa ajili ya doria na usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa; ununuzi wa mitambo minne (4) kwa ajili ya kuimarisha kingo za mito iliyopoteza mwelekeo wake wa asili katika Bonde la Usangu; uzinduzi wa Mkakati wa Kutangaza Utalii wa Ukanda wa Utalii wa Kusini mwa Tanzania; kukamilika kwa tafiti nne (4) zinazohusiana na wanyamapori katika maeneo ya kipaumbele ya hifadhi; kutoa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima 200 kutoka katika vyama nane (8) vya umwagiliaji; kutolewa kwa mafunzo ya usimamizi wa rasilimali za maji na uhifadhi wa mazingira kwa viongozi 28 wa jumuiya tatu (3) za watumia maji; kukamilika kwa ujenzi wa mfereji mkuu wa kilometa 2.9 na mfereji wa upili wa kilometa 6.9 katika Skimu ya Umwagiliaji ya Madibira; kusimikwa kwa vigingi 1,200 katika vijiji 8 na vigingi vingine 800 vimetengenezwa kwa ajili ya uwekaji mipaka wa vyanzo vya maji katika maeneo ya Mto Mbarali juu na chini kwa ajili ya kuimarisha kingo za mto huo; na kutoa mafunzo na kuvipatia fedha vikundi 150 vya Benki ya Hifadhi za Jamii (Community Conservation Bank-COCOBA) kwa ajili ya ununuzi wa mbegu bora za mazao. Jumla ya shilingi bilioni 22.3 zimetumika kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4812: Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya doria vikiwemo sare 100 (boots & combat), GPS 20, mahema 24, kompyuta 15 na kamera 15; kufanyika kwa mafunzo kwa waendesha mashtaka na wanasheria 70 kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na Jeshi la Uhifadhi; kufanya doria za ki-intelijensia na za ushirikiano za kupambana na ujangili katika Kanda 10 za ki-ikolojia za Kupambana na Ujangili; na kufanyika kwa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa Jumuiya ya Uhifadhi Wanyamapori wa Jamii (WMA) kwa viongozi 23 wa MBOMIPA. Jumla ya shilingi bilioni 12.0 zimetumika kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4647: Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

Hatua iliyofikiwa ni: kuandaa na kuwapatia mipango ya usimamizi wa mashamba wakulima 603; kutolewa kwa vifaa vya kupambana na majanga ya moto (fire beaters 393 na knapsack fire sprayers 36); kuanzishwa kwa Kamati za Vijiji za Usimamizi wa Moto zenye jumla ya watu 2,612 katika vijiji 80; kuanzishwa kwa vikosi vya kupambana na moto vyenye jumla ya watu 1,284; kutolewa kwa mafunzo ya ugani katika vijiji nane (8); kutoa mafunzo ya usimamizi na utunzaji wa mashamba kwa wakulima wa miti 13,246, viongozi 296 wa vijiji, wajasiliamali 202 na wakulima160; kutolewa kwa mbegu za miti zilizoboreshwa kwa vijiji 24; na kutoa mafunzo kwa wakufunzi saba (7) wa moto kuhusu tahadhari za moto na maafisa ugani 92 juu ya usimamizi wa biashara katika mnyororo wa thamani wa misitu. Jumla ya shilingi milioni 959.5 zimetumika kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4650: Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme - FORVAC)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ununuzi na usajili wa viwanda viwili (2) jongea (mobile sawmills) vya kuchakata mazao ya misitu kwa njia endelevu; kusimika mitambo ya kukausha mazao ya misitu kwa kutumia teknolojia ya mionzi ya jua katika wilaya za Liwale na Ruangwa; kununua na kusambaza mizinga 1,013 ya kisasa, jozi 12 za mavazi ya kurinia asali na vifaa vingine vya kuchakata asali katika vijiji 16 vya kongani ya Ruvuma, wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa kwa wanufaika vikundi 24; kuanzisha vikundi vitano (5) vya kukopa katika vijiji vya viwili (2) vya Wilaya ya Ruangwa; na kuwezesha vijiji 13 vya wilaya ya Liwale kupasua mbao zenye ukubwa wa mita za ujazo 452 na Wilaya ya Ruangwa jumla ya mita za ujazo 312.5. Jumla ya shilingi bilioni 4.6 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4651: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki - BEVAC**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa michoro ya usanifu na muundo kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanachuo wa kike lenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 200 katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) - Tabora; kuainisha maeneo ya misitu na hifadhi kwa ajili ya kuanzisha hifadhi za nyuki na manzuki pamoja na kanda maalum

za ufugaji nyuki katika mikoa ya Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Tabora, Katavi na Kigoma; kuainisha vituo vya kukusanyia na kuchakatia asali kwa lengo la kuviboresha na kuvijengea uwezo vile vinavyofanya vizuri; kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki na ushirika kwa maafisa nyuki 15, maafisa misitu wanne (4) na wataalam wengine wa mradi watano (5) pamoja na ununuzi wa pikipiki 20, kompyuta 8 na simu janja 37. Jumla ya shilingi bilioni 6.21 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 4816: Mradi wa Uendelezaji Utalii wa Mikutano na Matukio - MICE**

Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa hekta 19.2 za ardhi katika halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Utalii wa Mikutano na Matukio. Jumla ya shilingi milioni 7.59 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**B. Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**(i) Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo la iliyokuwa Makao Makuu ya Ofisi ya Kamati ya Ukombozi ya OAU ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; na kutoa elimu ya uzalendo wa kuenzi na kuhifadhi kumbukumbu za harakati za ukombozi wa Bara la Afrika kwa kuwafikia zaidi ya watu 2,000,000 Afrika kupitia mitandao ya kijamii, makongamano, matamasha, Makala jongefu na mijadala bayana. Jumla Shilingi milioni 515.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4353: Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa mkataba na nyaraka za ukarabati ya miundombinu ya taasisi na uendeshaji wa Tamasha la 41 la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo; na kuendelea na hatua za ununuzi wa Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa studio ya kisasa za kurekodi filamu na kituo cha redio na televisheni. Jumla ya shilingi milioni 216 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo kwa wasanii na wadau wa sanaa (45) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 ambao wamezalisha ajira za moja kwa moja 63 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 114; na kutolewa kwa mafunzo kwa wasanii 632 kuhusu elimu ya fedha, utunzaji kumbukumbu na urasimishaji. Jumla ya shilingi bilioni 1.07 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 6385: Ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Malya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 27; na kukamilika kwa michoro ya Kituo cha Kukuza na Kuendeleza

Vipaji (Sports Academy). Jumla ya shilingi milioni 389.27 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6523: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mshauri Elekezi wa ukarabati wa viwanja vya Benjamini na Uhuru na kuandaliwa kwa makadirio ya majenzi (BOQ) na michoro. Shughuli nyingine zilizofanyika ni tathmini ya awali ya mahitaji na gharama za ukarabati wa miundombinu ya michezo katika viwanja Saba (7) vya mpira wa miguu nchini.

**(vi) Mradi Na. 6521 - Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kushiriki na kutoa mada ya ubidhaishaji wa Kiswahili katika Kongamano la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) lililofanyika nchini Burundi na Kongamano la Chama cha ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) lililofanyika Chuo Kikuu cha HOWARD nchini Marekani; na kufanyika kwa maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Kiswahili Duniani. Jumla ya shilingi milioni 130 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 6527 - Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa Tathmini ya shule 56 za Sekondari zilizoteuliwa kuwa shule maalum za michezo ambapo hatua iliyofikiwa mi kukamilika kwa upembuzi yakinifu katika shule za sekondari saba (7) zilizopo mikoa ya Tabora, Tanga, Arusha, Pwani, Dodoma. Aidha, maandalizi ya makadirio ya majenzi (BOQ) yapo katika hatua za mwisho ili kutangaza zabuni na kumpata Mkandarasi.

**(viii) Mradi Na. 6504 - Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi Pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Sports Arena (Dar es Salaam na Dodoma)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mkandarasi wa ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzikia wananchi katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo mkandarasi yupo katika hatua za awali za kuandaa vifaa (*Mobilization Stage*); na kupatikana kwa eneo la ekari 12 kwa ajili ya ujenzi wa Arena ya Michezo Dar es Salaam lililopo Kawe, *Tanganyika Packers*. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**C. Sekta ya Fedha, Biashara na Masoko**

**(a) Mradi Na. 6244: Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na miradi 26 katika Halmashauri 23 ambapo miradi 19 ipo hatua ya ukamilishaji (miradi 12 imeanza kutoa huduma) na miradi saba (7)

ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Jumla ya shilingi bilioni 16.94 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Benki za Maendeleo**

**(i) Benki ya Maendeleo TIB**

Hadi kufikia Desemba 2022, Benki ya Maendeleo TIB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 370.23 ambayo ipo kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii zikiwemo kilimo miradi sita yenye thamani ya shilingi bilioni 87.47, ujenzi miradi minne (shilingi bilioni 29.99), elimu miradi miwili (shilingi bilioni 5.33), umeme miradi miwili (shilingi bilioni 8.70), Taasisi za fedha mradi mmoja (shilingi bilioni 0.31), Hoteli mradi mmoja (shilingi bilioni 0.08), uzalishaji miradi minne (shilingi bilioni 42.16), Madini miradi miwili (shilingi bilioni 96.76), Huduma nyingine miradi miwili (shilingi bilioni 2.87), Utalii miradi mitatu (shilingi bilioni 74.58), Mawasiliano na Usafirishaji mradi mmoja (shilingi bilioni 1.91), Mikopo binafsi minne (shilingi bilioni 6.91) na Maji miradi 65 (shilingi bilioni 13.16). Kati ya miradi hiyo, asilimia 89.34 ilitolewa kwenye miradi ya sekta binafsi na asilimia 10.66 kwenye miradi ya sekta ya Umma.

**(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo – TADB**

Hadi kufikia Desemba 2022 TADB ilikuwa na mtaji wa shilingi bilioni 454.351 ikiwa ni ongezeko la asilimia 26 kutoka shilingi bilioni 360.502 zilizokuwepo mwaka 2021. Aidha, hadi Desemba 2022, TADB ilitoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 161.7 kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya viwandani (Kahawa, Pamba na Mkonge); mazao ya mbogamboga na matunda (Parachichi, Vanilla, na Zabibu); uzalishaji wa mbegu za mafuta ya chakula (Alizeti na Chikichi); uzalishaji wa nafaka mbalimbali (Mahindi, Mpunga na Maharage) pamoja na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ng'ombe wa nyama, kuku na samaki. Vilevile, kufikia Desemba, 2022, TADB kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo (SCGS), ulitoa dhamana za jumla ya shilingi bilioni 48.471 kupitia benki kumi na tano (15) washirika katika mnyororo wa thamani wa mazao mbalimbali katika mikoa 24 ya Tanzania bara na kufanya kiasi cha dhamana kilichotolewa kwa wakulima wadogo kufikia shilingi bilioni 173.49 toka mfuko ulipoanza mwaka 2018.

**(c) Huduma za Bima**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandikishwa na kutolewa kwa leseni 1,195 zikijumuisha Kampuni za bima 31, Kampuni za bima mtawanyo (Reinsurance) 3, madalali wa bima mtawanyo watano (5), madalali wa bima 112, wakala wa bima 958 na benki wakala (bancansurance) 29, watoa huduma ya bima kidigitali wanne (4), watakwimu bima wanne (4), Wachunguzi binafsi wa bima (Private Insurance investigators) watatu (3) na wakadiriaji hasara wa bima 46; Kufanya ukaguzi kwa watoa huduma za bima ambao ni makampuni ya bima 18, matawi ya kampuni 18 za bima, madalali wa bima 8; benki wakala 8 na mawakala wa bima 68; kufanya ukaguzi wa bima kwa vyombo vya moto 33,160,000; na kupokea malalamiko 284 ambayo yalishughulikiwa

ambapo malalamiko 68 yalipatiwa ufumbuzi na kulipwa, 22 yalikataliwa, 11 yalipelekwa mahakamani, 18 yalipelekwa kwa Msuluhishi wa Migogoro ya Bima na 135 bado yanaendelea katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

**(d) Huduma Ndogo za Fedha**

Hadi Desemba 2022, jumla ya leseni 759 kwa watoa huduma za fedha daraja la tatu (*SACCOS*) zilitolewa na kusajiliwa watoa huduma za fedha daraja la nne (*CMGs*) wapatao 34,127. Aidha, Benki Kuu ilisajili watoa huduma 1,095 wa daraja la pili (*Non deposit taking money lenders).*

**(e) Huduma Jumuishi za Fedha**

Hatua iliyofikiwa ni: kuanzishwa kwa idara ya huduma jumuishi ndani ya Benki Kuu ili kuchochea mikakati itakayoongeza ujumuishaji wa kifedha na ufuatiliji wa masuala ya huduma jumuishi za fedha nchini na kutoa elimu ya fedha kwa umma kupitia semina kwa makundi mbalimbali na kupitia luninga na kuandaa rasimu ya Mpango wa Benki Kuu wa kumlinda mlaji wa Huduma za Fedha (*Bank of Tanzania Financial Consumer Protection Framework*).

**(f) Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uandaaji wa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation Guideline) kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na taasisi anazozisimamia; kukamilika kwa taarifa ya tathmini ya matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji (PEFA); kufunga na kuunganishwa kwa mfumo wa MUSE na mifumo sita (6) ambayo ni GePG, PlanRep–TR, PlanRep – LGA, ERMS na mifumo ya benki za biashara (CRDB na NMB); kuunganishwa na kufungamanishwa kwa Mfumo wa Ufuatiliaji na Uchambuzi wa Taarifa za Fedha na mifumo ya PlanRep - TR na MUSE; kuendelea na uundaji wa mfumo wa ukusanyaji wa gawio na fedha taslim kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma; kuendelea na ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya mtandao; kutolewa mafunzo kwa watumishi 2,696 kuhusu Usimamizi wa fedha za umma; kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi za Hazina Ndogo katika mikoa Kigoma, Kagera na Ruvuma. Jumla ya shilingi bilioni 14.7 zimetumika kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 6326: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi (Treasury Building)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli Mtumba ambapo utekelezaji umefikia asilimia 33.4 na ukarabati wa jengo la Wizara Dar es Salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60. Jumla ya shilingi bilioni 8.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 6573: Mpango Kabambe wa Takwimu Tanzania (TSMP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutoa mafunzo kwa makarani wa Sensa kwa mikoa yote katika ngazi ya wilaya, kata/shahiya; kufanya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi; kuchakata takwimu na kuandaa hesabu kuu za sensa; kuratibu vikao vya kamati ya sensa katika ngazi ya Taifa, mikoa na wilaya; usambazaji wa matokeo ya awali; kuendelea kufanya uchambuzi kwa matokeo zaidi; na kufanya mkutano wa kiufundi wa WASH. Jumla ya shilingi bilioni 303.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 6388: Uboreshaji wa Miundombinu ya TEHAMA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusimika Mfumo wa MUSE katika balozi kumi (10) za Tanzania za Nigeria, New-York, Washington, Canada, Abudhab, Oman, South Korea, Kuwait, Malaysia na Brazili pamoja na usimikaji wa mfumo wa usalama katika mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa fedha za umma. Jumla ya shilingi milioni 396.3 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**D. Masoko**

**(a) Soko la Bidhaa Tanzania – TMX**

Hatua iliyofikiwa ni: kutoa elimu, kuhamasisha wadau mbalimbali juu ya manufaa ya Soko la Bidhaa na kuuza Mazao. Soko liliuza Kahawa (Kagera) ambapo jumla ya tani 49,677 ziliuzwa kwa thamani ya shilingi bilioni 110.69. Ufuta uliuzwa tani 136.650 kwa shilingi bilioni 0.44, Kakao tani 878.570 kwa shilingi bilioni 4.12. Maandalizi ya kuuza Mifugo hai (ngómbe, mbuzi na kondoo) na ngozi zinazotokana na Wanyama hao yanaendelea. Aidha, timu ya wataalam ikijumuisha Soko la Bidhaa, Wizara ya Fedha na Mipango, Tume ya madini na Benki Kuu ya Tanzania ilikutana na kujadili namna Soko la Bidhaa litakavyoshiriki kuuza madini. Tume ya Madini itafanya utafiti wa aina ya madini yatakayouzwa Soko la Bidhaa na kuandaa mkataba wa makubaliano (MOU) kwa maeneo yote ya ushirikiano.

**2.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji**

**2.3.4.1.Huduma za Biashara na Masoko**

**(a) Uendelezaji wa Masoko ya Bidhaa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujengea uwezo wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa 12; na kuendelea na taratibu za awali za kumtafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 300.00 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Kuimarisha Maendeleo ya Soko la Ndani na Nje - TANTRADE**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuratibiwa kwa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yaliyohusisha washiriki 3,200 (kampuni za ndani 2,975 na kampuni za nje 225 kutoka Nchi 23); kutolewa kwa programu 10 za mafunzo kwa wafanyabiashara 285; kuzinduliwa kwa Mfumo wa *TanTrade Biashara Mobile App*

unaowezesha Wafanyabiashara kupata taarifa za masoko na kubaini fursa za kuweza kuuza bidhaa zao; na kuandaliwa kwa Mwongozo wa fursa za Uwekezaji baina ya Tanzania na Marekani. Jumla ya shilingi milioni 400.00 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Kuendeleza Biashara Kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

Hatua iliyofikiwa ni: kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa jengo la ghorofa 10 katika kampasi kuu ya Dar es salaam; kuendelea na taratibu za manunuzi ili kumpata Mshauri Mwelekezi wa mradi wa kumalizia ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (lecture theatre) kampasi ya Mwanza. Shughuli nyingine iliyofanyika ni kukamilika kwa ukarabati wa Kampasi ya Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 458.16 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**Kukuza Ushiriki wa Watanzania kwenye Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji**

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa tathmini ya ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati ambapo ajira 72,395 zimetolewa katika miradi ya Kimkakati.

**Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo na dhamana za mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 326.60 kwa wajasiriamali 903,763; kufanyika kwa tathmini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kuimairisha utendaji wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji; kuhuisha taarifa za mifuko na programu 72 za uwezeshaji.

**Kukuza Sekta Binafsi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa vikao na vyama mwavuli vya Sekta Binafsi ikiwemo Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) kwa lengo la kujadili jitihada za uendelezaji wa Sekta Binafsi nchini; kufanyika kwa utambuzi wa muundo wa Sekta Binafsi nchini ambapo jumla ya Kampuni 488 zenye ukomo wa ahadi (Limited by Guarantee) za Sekta Binafsi zimesajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Jumuiya za Biashara 22 zimesajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya nchini.

### 2.3.4.2. Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji

**A. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji Tanzania namba 10 ya mwaka 2022; kuendelea kuandaa kanuni za Utekezaji wa Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 2022; na kuandaliwa kwa mapendekezo ya maboresho ya sheria na kanuni zenye muingiliano ikiwemo maeneo ya tozo kero, adhabu, leseni na vibali kwenye sekta mbalimbali za biashara na uwekezaji; kuandaa na kushiriki

makongamao 10 ndani na Nje ya nchi; kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa jumla ya Hati za Makubaliano 50 zilizosainiwa; na kuendelea kuratibu maandalizi ya Kongani za Viwanda ikiwemo kongani ya viwanda ya Kwala Mkoani Pwani.

**B. Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi**

**(a) Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Centre - OSC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatiwa huduma kwa jumla ya wateja 13,836 katika kituo cha Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (OSC) ambapo jumla ya miradi 329 (127 wageni, 111 Watanzania 91 ubia kati ya wageni na Watanzania) ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,517 na inatarajiwa kutoa ajira kwa watanzania wapatao 53,632; kutolewa kwa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na OSC kwa njia ya "Documentary" na vyombo vya habari; na kutengenezwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji Mahali Pamoja (Tanzania Electronic Investment Window - TeIW) ambapo awamu ya kwanza inahusisha kuunganisha Mifumo kutoka Taasisi za NIDA, TRA, BRELA, TIC, Kazi, Uhamiaji na Ardhi.

**C. Mahusiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia**

**(a) Mradi Na. 6391: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Vitega Uchumi, Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa makazi ya balozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji) na nyumba ya mkuu wa utawala Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden); kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za ubalozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji); kuendelea na ukarabati wa makazi ya balozi wa Tanzania Stockholm (Sweden); kuanza kwa ukarabati wa jengo la zamani la ofisi Washington D.C, Marekani; kukamilika kwa ukarabati wa majengo matatu (3) ya makazi ya watumishi katika Ubalozi wa Tanzania Lilongwe (Malawi); kukamilika kwa ukarabati wa majengo nane (8) yanayojumuisha nyumba saba (7) zinazotumika kama kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Harare (Zimbabwe). Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika katika kipindi cha nusu mwaka ya mwaka 2022/23.

### 2.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu

#### 2.3.5.1. Afya

**(a) Mradi Na. 5487: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la kutoa huduma kwa wagonjwa binafsi na wagonjwa mashuhuri. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6364: Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila**

Shughuli zilizotekelezwa ni : Kuwezesha mafunzo kwa watumishi 82 ya ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali za kibingwa katika masomo ya uzamili; kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha upandikizaji viungo na sehemu ya kufulia nguo; na kukamilika kwa ukarabati wa wodi za watoto wachanga mahututi (NICU). Jumla ya shilingi bilioni 9.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(c) Mradi Na. 5491: Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba (vipandikizi (inplants revolving fund);. Jumla ya shilingi Milion 500 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5419: Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la Wagonjwa mahututi (ICU). Jumla ya shilingi milioni 500 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la (Oncology) la kusimika vifaa vya uchunguzi wa Saratani katika kituo cha Mbeya. Jumla ya shilingi Bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 5424: Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa Ambukizi – Kibong'oto (Kilimanjaro)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi na ukarabati mkubwa wa jengo la radiolojia kwa ajili ya kusimika CT Scan; kuendelea na ukarabati wa jengo la utawala; kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje na kukamilisha ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi. Jumla ya shilingi bilioni 3 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na 5425: Hopitali ya rufaa ya Afya ya Akili Mirembe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje. Jumla ya shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 5426: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa, Bugando**

Shughulili iliyotekelezwa ni kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa majengo ya wagonjwa mahututi - *Medical ICU*, *Surgical ICU*, na *Neonatal ICU*. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(i) Mradi Na. 5427: Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (Medical ICU na Surgical ICU); na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za tiba - mionzi kwa matibu ya magonjwa ya cancer (Radiotherapy)

ambapo utekelezaji umefikia asilimia 53. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 5422: Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**
Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), jengo la huduma za dharura (EMD) na chumba cha tiba mtandao; ununuzi wa vifaa tiba; na kuendelea na ujenzi wa jengo kwa ajili ya huduma za uzazi unaofanyika eneo la Meta ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99. Jumla ya shilingi Bilioni 12 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 5428: Hospitali ya Benjamini Mkapa**
Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa chumba cha kutolea tiba mtandao na jengo la huduma za CT - Scan; na kukamilika kwa upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU). Jumla ya shilingi bilioni 2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(l) Mradi Na. 5408: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Burigi**
Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa awamu ya tatu ya ujenzi wa nyumba 20 za watumishi, kuendelea na ujenzi wa uzio ambao umefikia asilimia 85, kukamilika kwa ujenzi wa njia za kupita wagonjwa na barabara za ndani ya eneo la Hospitali na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za uchunguzi kwa njia ya mionzi (Radiolojia). Jumla ya shilingi bilioni 29 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(m) Mradi Na. 5423 Hospital ya Rufaa ya Kanda ya Kusini - Mtwara**
Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), ujenzi wa nyumba ya mtumishi na ukarabati wa chumba cha tiba mtandao; na kuendelea na ujenzi wa Jengo la Huduma za Dharura (EMD) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80 na ujenzi wa jengo la OPD umefikia asilimia 61. Jumla ya shilingi bilioni 3.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(n) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni:

**(i) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe:** Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya OPD, afya ya uzazi, EMD, ICU, upasuaji, mifupa, wodi, sehemu ya kufulia, damu salama, kichomea taka na nyumba tano za watumishi. Aidha, ujenzi wa jengo la huduma za CT-Scan umefikia asilimia 99. Jumla ya shilingi bilioni 22 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Hospitali ya Mkoa Simiyu:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi, kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (asilimia

94), jengo la huduma za dharura (asilimia 94) na nyumba ya mtumishi (asilimia 98). Jumla ya shilingi bilioni 3.2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(iii) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita:** Kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Afya ya Uzazi na nyumba ya mtumishi, kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi umefikia asilimia 98 na jengo la huduma za dharura (asilimia 98). Jumla ya shilingi bilioni 3.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(iv) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songwe:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la OPD na jengo la huduma za afya ya uzazi; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na jengo la huduma za dharura (asilimia 89). Jumla ya shilingi bilioni 8.8. zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(v) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi:** Kukamilika kwa ujenzi nyumba ya mtumishi; kuendelea na ujenzi wa majengo ya uchunguzi na afya ya uzazi, miundombinu ya ICT, HVAC, Lift, Hewa Tiba, chumba cha tiba mtandao na jengo la OPD na Ujenzi jengo la huduma za CT-Scan umefikia Asilimia 97; na ujenzi wa jengo la huduma za dharura na jengo la wagonjwa mahututi umefikia asilimia 84. Jumla ya shilingi bilioni 12.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(vi) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida (RRH):** Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya mtumishi, ukarabati wa jengo la huduma za CT - Scan na chumba cha tiba mtandao; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za dharura na Jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90. Jumla ya shilingi bilioni 7.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(vii) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga:** Kukamilika kwa ujenzi ya nyumba ya mtumishi na jengo la huduma za CT-Scan; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 97 na jengo la huduma za dharura asilimia 99. Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(viii) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mara:** Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za watumishi; kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na jengo la huduma za dharura asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(ix) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Arusha (Mount Meru):** Kukamilika kwa ujenzi

wa nyumba ya mtumishi, ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, chumba cha tiba mtandao na jengo la huduma za CT - Scan. Jumla ya shilingi bilioni 3.1 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(x)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwanza (Sekou Toure):** Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la huduma za CT-Scan, chumba cha tiba mtandao na nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi milioni 500 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xi)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Mwananyamala):** Kuendelea na ujenzi wa jengo la Huduma za dharura ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98 na jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 90) na ukarabati wa jengo la huduma za CT-Scan (asilimia 99). Jumla ya shilingi bilioni 3.2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Temeke):** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la huduma za dharura; kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za CT - Scan ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi umefikia asilimia 96. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xiii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Pwani (Tumbi):** Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya mtumishi; kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za dharura na jengo la huduma za CT - Scan. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xiv)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kigoma (Maweni):** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kuhifadhi maiti, nyumba ya mtumishi na ukarabati wa chumba cha tiba mtandao; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za CT-Scan na huduma za dharura ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99 na jengo la OPD asilimia 95. Jumla ya shilingi bilioni 6.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xv)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro (Mawenzi):** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za dharura na ujenzi wa nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi milioni 240 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xvi)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Manyara:** Kukamilika kwa ukarabati wa chumba cha tiba mtandao na nyumba ya mtumishi; na kuendelea na ujenzi wa majengo ya huduma za CT - Scan (asilimia 92), wagonjwa mahututi (asilimia 82) na huduma za dharura (silimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 3.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xvii) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya:** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi na ujenzi wa nyumba ya mtumishi; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za CT-Sca ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87. Jumla ya shilingi bilioni 2.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xviii) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mtwara:** Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la huduma za CT - Scan. Jumla ya shilingi bilioni 3.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xix) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma:** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la huduma za dharura, ujenzi wa nyumba ya mtumishi, ujenzi wa jengo la huduma za CT-Scan na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xx) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za CT-Scan, ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi na ukarabati wa chumba cha tiba mtandao. Aidha, ukarabati na upanuzi wa jengo la huduma za dharura umefikia asilimia 99.4 na ujenzi wa nyumba ya mtumish umefikia asilimia 99. Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(xxi) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kagera**: Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya Mtumishi na jengo la wagonjwa mahututi; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za dharura (asilimia 99) na jengo la huduma za CT-Scan (asilimia 98). Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(o) Mradi Na 2208: Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMR)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kufanyika kwa tafiti za afya za magonjwa 113 ya binadamu; kufanyika kwa utafiti wa kufuatilia hali ya maambukizi ya malaria nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika mikoa 13 ya Tanzania bara (MSMT); kufanyika kwa jaribio nasibu la awamu ya tatu ya dawa ya Metformin kwa watu walioambukizwa VVU wanaokaribia kupata ugonjwa wa kisukari; na kufanyika kwa utafiti wa vyakula tiba kwa ajili ya afya ya uzazi na kutatua mahitaji muhimu ya virutubibisho na madini kabla na wakati wa ujauzito. Jumla ya shilingi bilioni 11.95 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(p) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na

vitendanishi ambapo kwa zahanati na vituo vya afya umefikia asilimia 45, hospitali za wilaya (asilimia 52), hospitali za rufaa za mikoa (asilimia 87) na Hospitali ya Taifa (asilimia 66); Kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba vya afya ya kinywa na macho kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri 71 zilizokamilika; na ununuzi wa vifaa tiba vya zahanati 300; na ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya Afya 159 vya tozo. Jumla ya shilingi bilioni 256.3 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(q) Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kutoa chanjo kwa watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja ambapo chanjo ya Penta3 kwa watoto 397,700 sawa na asilimia 107, chanjo ya Polio ya matone OPV3 asilimia 103, sindano (IPV) asilimia 107, Surua rubella 1 asilimia 109, Surua Rubella 2 asilimia 96, HPV1 asilimia 83 na HPV2 asilimia 62. Jumla ya shilingi bilioni 41 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(r) Mradi Na. 5492: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP)**

Hatua iliyofikiwa ni: kutoa huduma ya tiba na matunzo kwa watu wapatao 1,582,109; kutolewa kwa huduma za PMTCT, ambapo vituo 7,120 sawa na asilimia 95 ya vituo vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto vinatoa huduma za PMTCT; kupatiwa kwa huduma za upimaji VVU kwa wajawazito 1,793,204 kati ya wajawazito 1,818,147 wajawazito wote waliohudhuria hudhurio la kwanza kliniki. Kati yao, wajawazito 52,012 sawa na asilimia 2.9 walibainika kuwa wanaishi na maambukizo ya VVU. Wajawazito 49,953 sawa na asilimia 96 walianzishiwa dawa za ARV na kuzuia maambukizi kwenda kwa mtoto. Watoto 34,364 sawa na asilimia 88 ya Watoto waliozaliwa na akina mama wanaoishi na VVU walipimwa kipimo cha kwanza cha uchunguzi wa maambukizi ya VVU katika umri wa miezi miwili na asilimia 0.7 walibainika kuwa na maambukizi. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(s) Mradi Na.5498: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kununuliwa na kusimikwa kwa mashine za kisasa aina ya Truenut 30 kwenye vituo vya kutolea huduma za Kifua Kikuu; kutolewa kwa huduma za mkoba kliniki tembezi (Mobile Vans outreach services) ambapo jumla ya watu 8,298 walichunguzwa na kupimwa Kifua Kikuu; na kutekeleza shughuli ya tambua TB ambapo jumla ya wagonjwa 155 sawa na asilimia 35 wa Kifua Kikuu Sugu waliogundulika walianzishiwa matibabu. Jumla ya shilingi bilioni 9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(t) Mradi Na. 5406: Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya Kuambukiza**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa wodi mbili (2) kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na milipuko katika Hospitali ya Kisopwa ambapo utekelezaji wa umefikia asilimia 60; na kufanya tathmini ya huduma za mionzi nchini katika hospitali tano (5) - BMH, MBEYA, ORCI, KCMC na BUGANDO ili kuangalia

huduma zinazotolewa. Jumla ya shilingi bilioni 2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(u) Mradi Na. 2204: Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa wa jengo la wodi maalum (Private wards) katika Chuo cha *Tabora Clinical Officers Training Centre*; kukamilika kwa ukarabati wa majengo ya Chuo cha Ngudu (Ngudu School of Environmental Health Science), Chuo cha Kilosa Clinical Officers Training Centre, Kagemu Environmental Health Science, DIHAS na Chuo cha Tabora COHAS. Aidha, ujenzi katika Chuo cha Korogwe SON umefikia asilimia 95 , Mtwara COTC asilimia 95 na Nachingwea SON asilimia 48; na kutolewa kwa ufadhili wa masomo ya uzamili katika fani mbalimbali za afya kwa watumishi 373. Jumla ya shilingi bilioni 8.2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 5416: Mipango ya Afya na Uendeshaji**

Shughuli zilizotekelezwa: kuwekwa kwa mfumo wa tiba mtandao katika hospitali nne (4); na kununuliwa na kuanza kutumika kwa vifaa vya TEHAMA katika hospitali za kanda za Bugando na Benjamin Mkapa na hospitali tatu (3) za kibingwa (Muhimbili, MOI na JKCI) na hospitali maalum moja (1) (Ocean Road Cancer Institute). Jumla ya shilingi milioni 124 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(w) Mradi Na. 5401: Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Hospitali 59 za halmashauri na ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri ambapo utekelezaji wa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Jumla ya shilingi bilioni 57.15 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(x) Mradi Na. 5429: Huduma ya Afya ya Msingi**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukamilishaji wa zahanati 300 katika Halmashauri 184 ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali; na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa vituo vya afya 150, zahanati 300 na hospitali za Halmashauri 71. Jumla ya shilingi bilioni 59 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**2.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

**(i) Mradi Na. 6330: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa kumbi pacha za mihadhara (lecture theatre two in one) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1008, kuendelea na ujenzi wa bweni la wasichana la ghorofa nne (4) (asilimia 95); kukamilika kwa ukarabati wa jengo la utawala katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba; kuendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 (asilimia 90), ukumbi wa Mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 260 (asilimia 94) na mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 kila moja (asilimia 98) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha; kukamilika kwa ujenzi wa

Jengo la Utawala lenye vyumba vya ofisi 17 na kumbi mbili (2) ndogo za mikutano zenye uwezo wa kuchukua watu 40 kwa wakati mmoja katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale; na ujenzi wa hosteli ya ghorofa mbili yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6259: Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 463.84 kwa wanawake wajasiriamali; kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) na Mkakati wa utekelezaji wake (2005) ambayo ipo katika hatua ya uidhinishaji; kukamilika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na kuandaliwa kwa MTAKUWWA Awamu ya Pili; kukamilika kwa maandalizi ya Programu ya miaka mitano (2022 – 2026) ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kwenye Jukwaa la Kimataifa la Kizazi chenye Usawa; kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (Saint John University) na hivyo kufikisha idadi ya madawati 87 ya Jinsia yaliyoanzishwa mpaka sasa katika Vyuo Vya Elimu ya Juu na Kati; kufanyika kwa kampeni maalum ya kupinga ukatili dhidi ya watoto hususan ukeketaji katika mikoa yenye matukio mengi ya ukeketaji ya Manyara ambapo ukeketaji umefikia asilimia 58 na Mara (asilimia 31); na kuanzishwa kwa mfumo wa huduma kwa mteja ambao utatumika kutoa huduma zote za Wizara. Jumla ya shilingi bilioni 2.03 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuundwa kwa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto 1,393 katika shule za msingi na sekondari na Mabaraza ya Watoto 560 katika mikoa 8 (Rukwa, Arusha, Tanga, Dar es salaam, Pwani, Shinyanga, Dodoma na Geita); kutolewa kwa elimu ya uelewa katika jamii kuhusu Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22 - 2024/25) kwenye mikoa 10 ya Tabora, Lindi, Dar es saalam, Morogoro, Arusha, Manyara, Mbeya, Rukwa, Kagera na Dodoma; na kuendelea na maandalizi ya video fupi zenye ujumbe maalum ambazo zitatumika kwenye vyombo vya habari ikiwemo redio na Runinga kwa ajili ya kutoa tahadhari ya matumizi yasiyofaa ya mitandao ya kijamii kwa watoto, wazazi na jamii kwa ujumla. Jumla ya shilingi milioni 640.3 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 6290: Uchakataji wa Taarifa na Uandaaji Programu Programming and Data Processing)**

Hatua iliyofikia ni: Kufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli, Mlale, Ruaha, Uyole,

Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) na Makazi ya Wazee Kibirizi (Kigoma) na Kilima (Kagera). Jumla ya shilingi milioni 140 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

#### 2.3.5.3. Elimu

**(a) Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukarabatiwa kwa majengo yaliyoungua katika Chuo Kikuu Cha Dar es salaam Kampasi ya Zanzibar na ununuzi wa vifaa vya maabara; kuendelea na ujenzi wa Vyuo vitatu (3) vya Ualimu ambavyo ni Sumbawanga (asilimia 80), Dakawa (asilimia 80) na Mhonda (asilimia 80) na shule ya Mfano ya Sekondari Dodoma (asilimia 90); ujenzi wa shule mpya 40, madarasa 96, mabweni 4, nyumba za walimu 7 katika shule za msingi; ujenzi wa mabweni 62, madarasa 46, maabara 16, maktaba 4, nyumba za walimu 13, mabwalo 22 katika shule za sekondari; ujenzi wa ofisi tano (5) za wathibiti ubora wa shule katika halmashauri za Njombe, Tarime, Pangani, Bunda na Ubungo; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika vyuo vya ualimu Mamire (asilimia 90), Vikindu (asilimia 70), Songea (asilimia 5), Singachini (asilimia 5) na Katoke (asilimia 5); kuendelea na ukarabati wa Shule Kongwe 61 (msingi 45, Sekondari 16) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; na kununuliwa kwa mashine za uchapaji katika kiwanda cha Press A. Jumla ya shilingi bilioni 44.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4321: Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MMEM) LANES II**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa asilimia 40 ya tathmini ya ubora wa shule kwa shule 5812 Tanzania Bara; kuendelea kwa MEWAKA katika Halmashauri 144 zilizopo katika mikoa 26; kuchapishwa kwa nakala 372,773 ya vitabu vya uchambuzi wa mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi – CIRA – PSLE 2021; kuendelea na uchapaji wa nakala 53,510 za vitabu vya uchambuzi wa upimaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu - PIRA – SFNA na nakala 314,700 za vitabu vya uchambuzi wa upimaji wa darasa la IV – PIRA – SFNA ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa 128 ya mfano ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50. Jumla ya shilingi bilioni 17.64 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4319: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (Boost Primary Student Learning)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanya tathmini ya mahitaji ya miundombinu kwenye Shule za Msingi 17,182 zilizopo katika Halmashauri zote; Mafunzo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Elimu wa Mikoa, timu za utekelezaji wa mradi ngazi za Mkoa na Halmashauri ambapo jumla ya watendaji 2,888 wamepatiwa mafunzo; kutoa Mafunzo ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwenye shule za Msingi 2,952 kwenye Halmashauri 26 (Halmashauri 1 kila Mkoa) za majaribio; na

kukamilika kwa uaandaji wa miongozo ya utawala bora na kiongozi cha usimamizi wa shule pamoja na moduli 12 za mafunzo endelevu ya walimu kazini. Jumla ya shilingi bilioni 265.08 zimetumika hadi Januari, 2023.

**(d) Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanya ufuatiliaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 6,096, vifaa 1,655 vya kunawia mikono na matenki 238 ya kuhifadhia maji katika Shule za Msingi 235 zilizo katika Halmashauri 86; na kuandaa rasimu ya Mpango wa Kitaifa wa Ugharimiaji na Uwekezaji katika Huduma za Maji na Usafi na Mazingira Shuleni (National School WASH Costed Plan and Investment Case). Jumla ya shilingi bilioni 19.02 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa shule mpya 232 za Sekondari za kata zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 kila moja katika kata zisizokuwa na shule za Sekondari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75; ujenzi wa shule 10 maalumu za bweni (kidato cha 5 & 6) za wasichana kwa masomo ya Sayansi na upanuzi wa shule 11 umefikia asilimia 50; kukamilika kwa upanuzi wa shule kongwe 18 za sekondari na vituo nane (8) vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ili vitumike kutoa elimu kwa njia mbadala kwa wasichana walio nje ya mfumo rasmi; na kuwezesha na kutoa mafunzo kazini kwa walimu wapatao 736 wa masomo ya Sayansi na Hisabati kama wawezeshaji wa kitaifa. Jumla ya shilingi bilioni 39.72 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa ofisi za walimu katika shule mbili (2) za sekondari, maabara nne (4) na matundu 1,920 ya vyoo katika shule 80 za msingi na 22 za sekondari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na asilimia 89 mtawalia; kutolewa kwa mafunzo kwa wanufaika 5,981 kuhusu ujuzi katika nyanja za Kilimo, Kilimo uchumi, utalii na huduma za utalii, usafirishaji, Nishati na Teknolojia ya habari na mawasiliano; kutolewa kwa mafunzo ya ufundi stadi kwa wananchi 1,627 wanaotoka katika kaya maskini ikiwemo vijana, wanawake na walemavu; na kufikia asilimia 89 ya ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kuboresha miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule tisa (9) za msingi na shule moja (1) ya sekondari. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 fedha zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 6363: Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha - ATC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 428 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.46; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa nane (8) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 880 kwa wakati mmoja, maabara sita (6) zenye uwezo wa

kuhudumia wanafunzi 270 kwa wakati mmoja na ofisi 26 zenye uwezo wa kuhudumia watumishi 104 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.4; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa hospitali ya taaluma na tiba (polyclinic) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 94.43; na kuendelea na ujenzi wa kliniki itakayohudumia wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo jirani ambapo utekelezaji umefikia asilimia 24.43. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 4397: Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ufundi stadi vya mikoa ya Dodoma (asilimia 90), Mtwara (asilimia 94). Jumla ya shilingi bilioni 26.52 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 4323: Kuendeleza Elimu ya Ualimu - TESP**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi, maktaba na vyumba vya TEHAMA katika Vyuo saba (7) vya Butimba (asilimia 100), Morogoro (asilimia 90), Tukuyu (asilimia 92), Kasulu (asilimia 90), Patandi (asilimia 91), Mpwapwa (asilimia 70) na Dakawa (asilimia 70); kuendelea na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA ambapo kazi ya uunganishaji wa vyuo 35 vya ualimu katika Mkongo wa Taifa umefikia asilimia 40; ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo vya ualimu 35; ununuzi wa vifaa na madawa ya maabara katika vyuo 10 vya ualimu vya sayansi; na kuendelea na uundaji wa mfumo wa usahihishaji wa kielektroniki ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Jumla ya shilingi bilioni 12.35 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 657.0 kwa wanafunzi 196,982 (wanafunzi 73,031 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 123,951 ni wanaoendelea na masomo); kuwezesha ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ya shilingi bilioni 84.7 sawa na asilimia 86.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 97.5 katika kipindi cha nusu mwaka; kutoa udhamini wa wanafunzi 585 wenye ufaulu wa juu zaidi katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kupitia *Samia Scholarship*; na kuanzishwa kwa Kituo Mahsusi cha Wateja. Jumla ya shilingi bilioni 330.78 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 4392: Mradi wa Elimu wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi ya ESPJ**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati na ujenzi wa vyuo 14 vya maendeleo ya wananchi (FDCs) ambapo ujenzi umefikia asilimia 95, vyuo 25 vya Ufundi Stadi vya Wilaya (asilimia 96) na Chuo cha Ufundi cha Dodoma (asilimia 78); kutoa mafunzo ya ujuzi kwa vijana 2,373 walio katika mazingira magumu kupitia mpango wa *Bursary Scheme* na mafunzo kwa watanzania 5,030 kupitia programu ya mafunzo ya

Utarajali na Uanagenzi; na kuwajengea uwezo watumishi 2,400 wa VETA na FDCs kwa lengo la kuimarisha stadi za ujuzi. Jumla ya shilingi bilioni 27.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(l) Mradi Na. 4314: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maabara ya baiolojia ya viumbe hai ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88;na kuendelea na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya chuo (asilimia 75). Jumla ya shilingi milioni 210.2 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(m) Mradi Na. 6350 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Uchumi (asilimia 46) na maabara kuu ya kemikali kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani (asilimia 20); kuendelea na upanuzi wa hosteli ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongeza ghorofa mbili (2) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15; na kuanza utekelezaji wa mradi wa ubunifu wa utengenezaji wa vifaa vya maabara vya mashuleni (asilimia 50). Jumla ya shilingi bilioni 5.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(n) Mradi Na. 4385: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu ya maabara za sayansi katika shule ya sekondari ya mazoezi ya Chang'ombe ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; na kuendelea na ujenzi wa Jengo la Kitivo cha Insia na Sayansi za Jamii na Maabara za Sayansi. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(o) Mradi Na. 6353: Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa jengo la maktaba (wanafunzi 3,000) Kampasi Kuu na Zahanati Kampasi ya Mbeya; kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 5) na jengo la madarasa sita (6) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,129 Kampasi Kuu (asilimia 5); kuendelea na ukarabati wa eneo la mahafali (asilimia 70), viwanja vya michezo (asilimia 44) na madarasa 6 (asilimia 60) katika Kampasi Kuu, bwalo la chakula Kampasi ya Mbeya (asilimia 91); na kuendelea na uwekaji wa taa za barabarani Kampasi Kuu (asilimia 80). Jumla ya shilingi milioni 635.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(p) Mradi Na. 6354: Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa midahalo, madarasa, maabara, studio, karakana, jengo la shahada za juu na utafiti pamoja na mabweni; kuendelea na ukarabati wa karakana (asilimia 50), madarasa 15 (asilimia 50), ofisi 5 (asilimia 50), maabara 2 (asilimia 50), mabweni ya wanafunzi 3 (asilimia 50),

nyumba 10 za watumishi (asilimia 50) na miundombinu ya TEHAMA (asilimia 50). Jumla ya shilingi milioni 165.68 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(q) Mradi Na. 6365: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la maktaba (asilimia 5) na ukumbi wa mihadhara ambapo ujenzi umefikia asilimia 28; kuendelea na ukarabati na upanuzi wa jengo la Kurugenzi ya Shahada za Awali (asilimia 85) na miundombinu mbalimbali ya Chuo iliyopo Kampasi kuu ya Moshi (asilimia 20), na ofisi 174 za Chuo za mikoani (asilimia 5); na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la stoo na choo na ununuzi wa gari moja (1). Jumla ya shilingi milioni 303.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(r) Mradi Na. 6364: Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili - Kampasi ya Mloganzila**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ununuzi wa vifaa vinavyotumia umeme wa jua ili kukuza matumizi ya teknolojia ya kijani kibichi na kupunguza matumizi makubwa ya umeme (asilimia 85); kuendelea na ujenzi wa tanki kubwa la maji katika na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (asilimia 40); kuendelea na ukarabati wa Hosteli 4 za wanafunzi na ujenzi wa miundombinu (mihadhara, madarasa, ofisi za utawala na walimu) Kampasi Kuu ya Muhimbili - Upanga (asilimia 50.0); na ukarabati wa awamu ya pili wa miundombinu (nyumba moja ya utafiti na mifumo ya maji na umeme) ya kituo cha kufundishia cha Bagamoyo cha kampasi ya Muhimbili (asilimia 80.6); na ukarabati wa mabweni 6 ya Chole (asilimia 80). Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(s) Mradi Na. 4384: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaaam – DIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa matano (5) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200 na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 160 Kampasi ya Myunga ambapo ujenzi umefikia asilimia 95; kuanza ujenzi wa mabweni 2 Kampasi ya Mwanza yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 (asilimia 20); na kuratibu mafunzo kwa washiriki 71 katika TEHAMA, Sayansi ya Maabara na Teknolojia ya Ngozi. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(t) Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki - TAEC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa awamu ya Pili ya Ujenzi wa Maabara na Ofisi zilizopo Arusha na Dodoma; kuendelea na ujenzi wa ofisi na maabara Dar es Salaam (asilimia 63), ujenzi wa ofisi na maabara Mwanza (asilimia 84) na ujenzi wa maabara ya Zanzibar (asilimia 36); kuendelea na ujenzi wa jengo maalumu la kuhifadhi ya kilimo kwa kutumia teknolojia ya mionzi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 34.0; na kuendelea na ujenzi wa jengo maalumu kwa ajili ya kuhifadhi

mazao ya kilimo (asilimia 34). Jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(u) Mradi Na. 6333: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa hosteli mbili (2) zitakazosaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu (asilimia 44); kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya Chuo; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya maabara na karakana (asilimia 98); na kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) yatakayohudumia wanafunzi 800 (asilimia 48). Jumla ya shilingi milioni 84.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6361: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – SUA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendeleza shamba la miti la Ifinga, kwa kupanda hekta 1,364 za miti; kuendelea na ukarabati wa Hosteli katika Kampasi ya Edward Moringe (asilimia 70); na kununuliwa kwa kiwanda cha mbao katika Kampasi ya Mizengo Pinda; Jumla ya shilingi bilioni 7.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(w) Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majiko na gesi kwa ajili ya vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi (asilimia 93); kuendelea na ununuzi wa vifaa vya karakana katika vyuo 34 vya maendeleo ya wananchi (asilimia 82); na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo 14 vya maendeleo ya Wananchi (asilimia 90). Jumla ya shilingi bilioni 7.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(x) Mradi Na. 4381: Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) awamu ya pili yatakayohudumia wanafunzi 768 kila moja katika kampasi ya Karume – Zanzibar (asilimia 45) na ujenzi wa Jengo la Maktaba na ukumbi wa mihadhara (asilimia 12), kukamilika kwa uwanja wa mpira wa kikapu na ukarabati wa Jengo la Uhuru katika Kampasi ya Kivukoni na jengo la Utawala katika Kampasi ya Karume, vyoo vya wanafunzi katika jengo la utamaduni na ukarabati wa miundombinu na kuweka samani katika mabweni ya Azimio, Kizota, Kawawa na kijichi; na kuendelea na ujenzi wa kumbi za mihadhara za Garden Hall 3 na Garden Hall 4 katika Kampasi ya Kivukoni (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 2.3 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(y) Mradi Na. 4306: Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa moja (1) lenye ofisi kumi (10) na kumbi nne (4) za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 (asilimia 70); na ujenzi wa kumbi za mihadhara katika kampasi ya Bagamoyo (asilimia 5). Jumla ya shilingi milioni 378.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya

mwaka 2022/23.

**(z) Mradi Na. 6345: Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ugharamiaji wa miradi 173 ( ubunifu 123, utafiti 39 na miundombinu ya utafiti 11; kutoa mafunzo ya awali ya ubunifu kwa watoa ruzuku 14 wa MAKISATU na washindi 13 wa MAKISATU; kufanya mafunzo ya kuongeza uelewa juu ya Miongozo ya kutambua, kukuza ubunifu, uvumbuzi na maarifa asilia kwa Halmashauri 23; kuandaa mfumo wa uhawilishaji wa teknolojia (technology transfer system) pamoja na mapitio ya teknolojia zinazoibuka (Inventory of emerging technologies); na kuendelea na uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu na mfumo wa TEHAMA wa Menejimenti ya Utafiti na Ubunifu ili kuongeza ufanisi na upatikanaji wa taarifa za watafiti na wabunifu. Jumla ya shilingi bilioni 2.4 fedha za ndani zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(aa) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukamilishaji wa: maboma ya madarasa ya shule za msingi 809; maboma ya vyumba vya maabara za Sayansi 271 katika Shule za sekondari; maboma ya mabwalo ya chakula manne (4) katika shule za msingi na mabwalo 74 katika shule za sekondari; maboma ya mabweni 64 katika shule za msingi zenye mahitaji maalum na mabweni 115 kwa shule za sekondari; nyumba za walimu 113 katika shule za msingi; madarasa ya shule kongwe 1,072; uzio shule maalamu 35; vyoo shule shikizi 2,726; kukamilika kwa ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari katika mikoa yote 26; na ujenzi wa shule 6 mpya za Msingi. Jumla ya shilingi bilioni 233 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/233.

**(bb) Mradi Na. 4322 na 4393: Elimumsingi Bila Ada**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutoa elimu msingi bila ada ikijumuisha ruzuku ya uendeshaji wa shule, posho ya madaraka kwa walimu wakuu 21,335 na maafisa elimu kata 3,921, fidia ya ada kwa shule za bweni kwa wanafunzi 204,439 na kutwa 2,341,438 na kugharamia chakula cha wanafunzi 226,723 wa shule za bweni na wanafunzi wenye mahitaji maalum 45,366 wa shule za msingi za kutwa. Jumla ya shilingi bilioni 176.10 zimetumika Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(cc) Mradi Na. 4309: Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki (EASTRIP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Miundombinu (Karakana, Mabweni, Kumbi za Mihadhara na Nyumba za Watumishi) katika kituo cha Umahili cha Kikuletwa; kuendelea na ujenzi wa majengo nane (8) kwa ajili ya madarasa, maabara, karakana na ofisi za watumishi ambapo majengo matano (5) yanajengwa katika Kampasi ya Mabibo – Dar es salaam na majengo Matatu (3) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro; na ununuzi wa vifaa maalum vya mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege (Fixed Cabin Crew Mock – Ups). Jumla ya shilingi

5.3 bilioni zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(dd) Mradi Na. 6321: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA)**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala Kampasi ya Babati ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ee) Mradi Na. 6322: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa madarasa, jengo la utawala, bwalo la chakula pamoja na ukumbi wa shughuli mbalimbali (multipurpose hall) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Aidha, ujenzi wa bweni, nyumba za wafanyakazi, maktaba na maabara za kompyuta umefikia asilimia 50. Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ff) Mradi Na. 6323: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, madarasa na maktaba katika Kampasi ya Nyang'homango, Misungwi - Mwanza ambapo utekelezji umefikia asilimia 65. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(gg) Mradi Na. 6206: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara awamu ya pili katika Kampasi Kuu Dodoma (asilimia 65); ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa - Magu Mwanza (asilimia 60); na kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa bweni la wanafunzi awamu ya III katika eneo la Miyuji Kampasi Kuu Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 3.32 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**2.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**(a) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi kwa ajili ya uwekezaji na makazi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji ambapo hati za kumiliki ardhi 98,191 sawa na asilimia 28 ya Hati 350,000 na hatimiliki za kimila 27,895 zimetolewa sawa na asilimia 5.4 ya 520,000; na Mashamba 81 yamepimwa. Jumla ya shilingi bilioni 1.57 zimetumika kwa kipindi cha nusu mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 2324: Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutekelezwa kwa kazi ya kupima na kujenga alama za mpaka kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya. Jumla ya kilomita 110 zimeimarishwa kutoka

Ziwa Natroni hadi Namanga na hivyo kufanya kipande cha mpaka kilichoimarishwa kuwa kilometa 348 kati ya kilometa 758 za mpaka wa nchi kavu wa Tanzania na Kenya. Jumla ya shilingi Milioni 36.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(c) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo**

Hatua iliyofikiwa ni: Ukarabati na ununuzi wa samani za ofisi katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya matatu (3) Busega, Kishapu na Kyerwa; Kuendelea na ukamilishaji wa jengo la Maktaba katika Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA). Jumla ya shilingi milioni 155.6 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(d) Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya za Tanganyika (Katavi), Uvinza (Kigoma) na Nzega (Tabora); kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 141 vilivyopo katika wilaya 27; kujengea uwezo timu 288 kutoka halmashauri za wilaya 36 na wajumbe 1,936 kutoka Kamati za uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 242 kuhusu uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji; kujengea uwezo halmashauri ya wilaya ya Nzega kuhusu matumizi ya mfumo wa uandaaji wa hati za hakimiliki za kimila (CCROs); kuandaliwa kwa mipango kina ya vitovu vya vijiji na mashamba katika vijiji vitano (5); na kuwezesha upimaji wa viwanja 5,269 na mashamba 2,740 katika wilaya za Nzega, Chalinze na Handeni. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 zimetumika katika nusu ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4953: Uboreshaji wa Milki za Ardhi**

Hatua zilizofikiwa ni: Kuwajengea uwezo viongozi 44 na watumishi 45 katika jiji la Dodoma kuhusu utekelezaji wa mradi kwa upande wa mjini; na kuwajengea uwezo Halmashauri tatu (3) za Chamwino, Longido na Maswa kupitia majaribio ya mradi kwa upande wa vijijini. Jumla ya shilingi bilioni 4.02 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Katika Vijiji 975**

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kutatuliwa kwa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 nchini; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi za Taifa, na kufanya tathmini na uthamini kwa wananchi watakaopisha shughuli za uhifadhi kwenye Hifadhi ya Taifa Ruaha na Serengeti (Pori Tengefu - Ghuba ya Speke). Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**2.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira**

**(a) Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira**

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa

asilimia 72.3 mwezi Juni 2021 hadi wastani wa asilimia 77.0 Desemba, 2022. Aidha, kwa upande wa mijini hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi imeongezeka kutoka asilimia 86.5 hadi asilimia 88.0.

**(b) Mradi Na. 3436: Ufuatiliaji na Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP - II)**

Hatua iliyofikiwa ni: ukarabati wa mabweni matatu (3) katika chuo cha maji; ununuzi wa eneo la ekari 41.5 katika Manispaa ya Singida kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Singida ya Chuo cha Maji; kugharamia wataalamu washauri wanne (4) kutoa huduma katika maeneo ya usimamizi wa fedha na ununuzi wa mradi wa WSSP II; na kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) ambayo yamefikia wastani wa asilimia 90. Jumla ya shilingi bilioni 1.75 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6545: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukaratabati na ujenzi wa vituo 8 vya kukusanya takwimu za rasilimali za maji; kuanzishwa kwa jumuiya 11 za watumiaji wa maji; kupima na kuweka mipaka katika vyanzo 43 kwa lengo la kuvilinda na kuvitangaza; na kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa ofisi za mabonde ya Ziwa Nyasa katika Miji ya Njombe, Bonde la Wami Ruvu, Ziwa Rukwa, na ofisi za Bonde la Ruvuma katika miji ya Lindi na Mtwara. Jumla ya shilingi bilioni 11.56 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 3435: Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia**

Hatua iliyofikiwa: kufuatilia, kukusanya na kuchunguza ubora wa maji kwenye jumla ya sampuli 3,117 za maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani (2378), umwagiliaji (19), ujenzi (42), viwandani (203) na sampuli 475 za ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji; na kuendelea kuboresha maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia vitendea kazi ikiwemo vifaa vya usalama mahala pa kazi (89), vifaa vya kupima ubora wa maji (*Mult-parameters Kits* (8), *Fluocullator* (8), *Turbidimete*r (8)) pamoja na Kompyuta (30). Jumla ya shilingi milioni 340.47 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 3280: Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa miradi 382 na kunufaisha wananchi wapatao 2,064,023. Jumla ya shilingi bilioni 93.29 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 3306: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa mtandao wa majisafi katika maeneo ya Ndachi – Mnadani katika jiji la Dodoma na Manispaa ya Bukoba; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira Arusha ambapo utekelezaji

umefikia asilimia 89.47; kuendelea na ujenzi wa choteo jipya katika mradi wa maji na usafi wa mazingira mji wa Kigoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99; kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika mji wa Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji ya Musoma ambao umefikia asilimia 5. Jumla ya shilingi bilioni 69.81 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Wanging'ombe; na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Mugango – Kiabakari - Butiama ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 71. Jumla ya shilingi bilioni 35.64 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 3342: Mradi wa Maji wa Tabora – Igunga - Nzega**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na upanuzi wa mradi wa Tabora – Nzega – Igunga kupeleka maji katika miji ya Tinde na Shelui ambapo utekelezaji umefikia asilimia **99** na upo katika hatua za matazamio; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika miji ya Nzega, Uyui, Tabora, Igunga, tinde na Shelui. Jumla ya shilingi bilioni 1.52 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 3403: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na Miji Mingine**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa zoezi la kulipa fidia, usanifu wa bomba kuu na kuhamisha makaburi 78 kwenye eneo la mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mkoa wa Simiyu; na kuendelea na usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji katika miji na vijiji 147 kandokando ya bomba kuu, mabwawa ya kumwagilia. Jumla ya shilingi bilioni 2.38 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 3437: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji eneo la DAWASA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usambazaji wa maji katika maeneo ya Mshikamano, zegereni na Chalinze III; na kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi wa kutoa maji kutoka kwenye tanki la Chuo Kikuu Ardhi na kupeleka Bagamoyo. Jumla ya shilingi bilioni 6.14 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 3439: Mradi wa Maji wa Mpera na Kimbiji**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji ujazo wa lita milioni 15 katika eneo la Kisarawe II; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika maeneo ya Kigamboni. Jumla ya shilingi bilioni 1.94 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23

**(l) Mradi Na. 3438: Mradi wa Bwawa la Kidunda**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda na Mkataba umesainiwa mwezi Novemba, 2022 ambapo Mkandarasi anaendelea na maandalizi *ya* vifaa (*mobilization stage)* na wataalamu kwa ajili ya kuanza ujenzi. Jumla ya shilingi bilioni 49.4 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

#### 2.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

**(a) Programu Na. 5301: Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**(i) Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vidogo viwili (2) vya kutengeneza bidhaa za ngozi katika Halmashauri za Simanjiro na Kishapu; kukamilika kwa ujenzi wa majosho mawili (2), mabirika mawili (2) ya kunyweshea mifugo katika Halmashauri za Mpwapwa na Simanjiro; kuanzishwa kwa kitalu cha Mkonge (Ekari 20) katika Halmashauri ya Kishapu; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za nyuki (Manzuki) 16 katika Halmashauri ya Kishapu; kutengeneza na kusambaza mizinga 400 ya ufugaji nyuki katika Halmashauri za Kishapu (200) na Simanjiro (200); na kukamilika kwa uchimbaji wa visima virefu vitatu (3) na utengenezaji wa majiko banifu kwa kaya 90 katika Halmashauri ya Mpwapwa. Jumla ya shilingi milioni 230.9 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania**

Hatua Iliyofikiwa ni: kuanzisha mashamba darasa 127 kwa ajili ya kusambaza teknolojia na mbinu bora za kilimo cha mazao ya mahindi, mpunga, mtama, mihogo, alizeti, mwani na migomba; kukamilika kwa ukarabati wa tuta lenye urefu wa mita 850, ujenzi wa *spill ways* mbili na kukarabati *spill way* moja katika eneo la Bonde la Ukele - Pemba; upandaji wa miti 1,336,860 katika maeneo ya vijiji na shehia za Micheweni (1,322,410), Nzega (8850), Mkalama (3,000), Kondoa (1,100) na Magu (1,500); na kutengeneza na kutundika Mizinga ya Nyuki 3,665 kwa wilaya za Nzega (1,072), Mkalama (1,520), Kondoa (600), Magu (241) na Micheweni (222). Jumla ya shilingi milioni 230.9 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria (ACC - LVB Project)**

Hatua iliyofikiwa ni: Ufungaji wa pampu nne (4) za kusukuma maji zinazotumia umeme wa nguvu ya jua kwenye visima vinne (4) virefu katika vitongoji vya Mbiti (2), Busalanga (1), na Sekoture (1); kurinwa kwa lita 160 za asali na kufungashwa; kuanzisha vitalu vya miti ya matunda, mbao na kivuli katika shule za msingi Busalanga na Ng'haya ambapo miche takribani 40,000 imeoteshwa; kuendelea na ujenzi wa vibanda vinne (4) vya mitambo ya kuzalisha umeme; ujenzi wa uzio wa usalama kwenye mitambo ya kuzalisha umeme wa jua; na kutandaza mtandao wa

bomba za maji wenye urefu wa mita 800; na ujenzi wa mfereji mkubwa wa shughuli za umwagiliaji wenye mita 300. Jumla ya shilingi milioni 16.25 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu**

Hatua iliyofikiwa ni: Ununuzi wa vifaa kwa ofisi za Wizara za kisekta za Tanzania Bara na Zanzibar ambazo zinatekeleza Mradi; na kuwezesha ushiriki wa Tanzania Katika Mkutano wa 26 (COP 26) wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Glasgow Uskochi; kuandaa mwongozo wa biashara ya Hewa Ukaa na kanuni zake.

**(v) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bioanuai**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezesha Tathmini ya Athari za Utekelezaji wa Shughuli za Mradi kwa Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Safeguard);* kutoa mafunzo ya kuhuisha masuala ya urejeshaji katika mipango, sera na mikakati ya kisekta kwa kikosi kazi cha taifa cha kuhamasisha masuala ya urejeshaji endelevu wa mazingira; na kuandaa mikakati ya mawasiliano, usimamizi wa maarifa, pamoja na wavuti ya mradi. Jumla ya shilingi bilioni 1.53 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

**(i) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa**

Hatua iliyofikiwa ni: Ukusanyaji wa taarifa kuhusu mbinu bora za kilimo cha asili; kufanya tathmini ya Sera na shughuli za maendeleo katika eneo la mradi; kufanya tathmini na kuendeleza utekelezaji wa mipango shirikishi ya usimamizi wa misitu; kuendeleza juhudi za uzalishaji endelevu wa mkaa mbadala na uhamasishaji wa majiko banifu kwa Halmashauri za Wilaya za Kyela, Ludewa, na Makete; kuwezesha usimamizi endelevu wa rasilimali za maji katika bonde la ziwa Nyasa; kuwezesha makundi kumi (10) ya wanawake na makundi kumi (10) ya vijana kufanya shughuli mbadala za kiuchumi zikiwemo kilimo, ufugaji wa nyuki na uvuvi. Jumla ya shilingi milioni 87 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

Hatua iliyofikiwa ni: kuandaa na kuchapisha Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Usimamizi wa Taka; kuandaa kanzidata ya Sheria, Kanuni, Sheria ndogo na Miongozo ya Usimamizi wa mazingira; kuboresha mfumo mtandao wa utoaji vibali vya mazingira; na kuandaa Mipango Kazi ya Usimamizi wa Mazingira kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Jiji la Dodoma.

**(c) Mradi Na. 5305: Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika**

**Mazingira kwa Muda Mrefu**

Hatua iliyofikiwa ni: kutoa elimu kwa umma kuhusu uhifadhi wa taka ngumu ikiwemo kuonesha mifano katika masoko na shule za Dodoma; kutoa mafunzo kwa Manispaa za Kigamboni na Ubungo kuhusu namna ya kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Taka; kufanya tathmini ya hali ya urejelezaji wa taka ngumu nchini; kuchukua sampuli za mafuta ya Transfoma yanayosadikika kuwa na kemikali aina ya PCBs katika vituo vya kupoza umeme Zanzibar kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kimaabara; na kukamilisha rasimu ya kanuni za usimamizi wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu. Jumla ya shilingi milioni 23.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 5304: Kudhibiti Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuratibu na kushiriki kwenye maadhimisho ya siku ya Ozoni Duniani; kutolewa kwa mafunzo kwa maafisa forodha (40) na wasimamizi wa sheria (20) kuhusu njia za kudhibiti uingizwaji nchini wa kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni; mafunzo kwa mafundi mchundo (60) wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna ya kuhudumia vifaa hivyo pasipo kuharibu mazingira; na kuandaa Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni za mwaka 2022 kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN No.581 na GN No. 582); Jumla ya shilingi milioni 61 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 6309: Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

Hatua iliyofikiwa ni: Kulipa fidia kwa wananchi jirani na makazi ya Makamu wa Rais, Tunguu; na kuendelea na ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais, Kilimani Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 596.99 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**2.3.5.7. Usimamizi wa Maafa Nchini**

**(i) Mradi Na. 6575: Kuimarisha Uwezo wa Kujiandaa na Kukabili Maafa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutoa mafunzo kwa Kamati mbili (2) za Usimamizi wa Maafa na waratibu wa maafa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara; kuandaa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa pamoja na mikakati ya kupunguza madhara katika Halmashauri sita (6); na kutoa misaada ya kibinadamu katika Halmashauri nne (4) zilizoripotiwa matukio ya maafa. Jumla ya shilingi bilioni 1.73 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

**Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa maghala mawili (2) ya kuhifadhi vifaa vya misaada ya kibinadamu wakati wa maafa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 63.

Jumla ya shilingi milioni 490.24 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

### 2.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu

#### 2.3.6.1. Ujuzi na Uwezeshaji

**(a) Mradi Na. 6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kufanyika kwa mafunzo ya uanagenzi yanayohusu ujenzi na kulima kwa kutumia vitalu nyumba kwa vijana 7,760 katika mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Tabora, Pwani na Singida; kuwezesha mafunzo 11 ya kuboresha Tija na Ubunifu kwaajili ya kujenga uwezo kuhusu dhana, kanuni na viwango vinavyoibuka katika tija, ubunifu na ufanisi; kuwezesha mafunzo kwa washiriki 198 kutoka taasisi mbalimbali binafsi na za umma; kutolewa kwa mafunzo ya ujuzi wa teknolojia ya uchumi wa buluu katika sekta ya uvuvi kwa vijana 500; kuundwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Soko la Ajira kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA); na kukamilika kwa moduli ya kuwaunganisha watafutakazi na waajiri. Jumla ya shilingi bilioni 3 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo kwa vikundi 50 vya uzalishaji mali na kampuni 35 za vijana; kutoa mafunzo kwa wakopaji na wasimamizi wa Mfuko katika mikoa minne (4) ya Dodoma (481); Kigoma (716); Shinyanga (100) na Lindi (200); na kukamilisha maandalizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Jumla ya shilingi bilioni 1.88 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6205: Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha**

Shughuli zilizofanyika ni: kuendelea na Mapitio ya Programu ya Kukuza Kazi za Staha; kuendelea maandalizi ya upembuzi wa Asasi na Mitandao inayojihusisha na masuala ya maendeleo ya vijana katika mikoa 26; Kuandaliwa kwa Rasimu ya pili ya Mfumo wa mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule kwa lugha ya Kiingereza. Jumla ya shilingi milioni 137.79 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4954: Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vya madarasa (13), mabweni ya wanafunzi nane (8), nyumba za watumishi (17), karakana sita (6) na majengo ya mabwalo ya chakula matatu (3), majengo ya utawala mawili (2) katika vyuo vya ufundi stadi na marekebisho vya Mtapika (Masasi – Mtwara), Luanzali (Tabora), Sabasaba (Singida) na Yombo (Dar es Salaam). Jumla ya shilingi bilioni

3.46 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 202/23.

### 2.3.7. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma

Hatua iliyofikiwa ni: kuchangiwa kwa jumla ya shilingi bilioni 425.3 katika Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 135 ikiwa ni ongezeko la asilimia 35 ya lengo lilokusudiwa la kukusanya shilingi bilioni 314.9 kwa kipindi husika. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa makusanyo ya mtaji wa ziada, ulipwaji wa madeni kwa wakati, michango ya asilimia 15 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na mapato yatokanayo na simu zinazopigwa nje ya nchi. Vile vile, uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma umeongezeka kutoka shilingi trilioni 67.06 mwaka wa fedha 2020/21 hadi kufikia shilingi trilioni 69.91 mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 4.

### 2.3.8. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

**Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

Serikali imeendelea na uratibu wa utekelezaji wa miradi ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (Public Private Partnership - PPP) inayoibuliwa na Mamlaka za Serikali kwa kuzingatia Sheria ya PPP, Sura 103 na Kanuni zake za mwaka 2020. Katika kutekeleza miradi ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi, hatua iliyofikiwa ni:

(i) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa kipande cha barabara ya Kibaha – Chalinze (km 78.9) na kuendelea na taratibu za kumpata mbia;

(ii) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa miradi ya barabara ya tozo kutoka Chalinze - Morogoro (126km); barabara ya tozo Mbeya By-pass (Uyole – Sogwe 48.9km) na mradi wa ukaguzi wa lazima kwa vyombo vya moto;

(iii) Kuendelea na maandalizi ya upembuzi yakinifu wa awali wa mradi wa ujenzi wa kituo cha mazoezi tiba Mbweni Dar es Salaam chini ya Taasisi ya Mifupa ya MOI na ununuzi wa mtoa huduma wa mradi wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Tatu na ya Nne;

(iv) Kukamilika kwa mapitio ya taarifa ya upembuzi yakinifu ya miradi ya ujenzi wa viwanda vya dawa muhimu na vifaa tiba itakayotekelezwa chini ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya na kuendelea na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya taratibu za ununuzi wa mbia;

(v) Kuandaliwa kwa mkataba wa ubia na taratibu za kusaini mkataba kati ya mzabuni anayependekezwa ambaye ni mtoa huduma wa kudumu na Mamlaka ya Serikali (Wakala - DART) kwenye mradi wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza;

(vi) Kuendelea na hatua za kumpata mbia wa miradi ya ujenzi wa hoteli ya nyota nne na jengo la biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; na

(vii) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi wa kuimarisha huduma za saratani nchini kwa kujenga kituo cha ubingwa bobezi wa tiba ya saratani eneo la Mloganzila (Ultra- Modern Oncology Centre - UMOC) na Kituo cha Saratani Mbeya (Mbeya Cancer Centre - MCC) eneo la Iwambi- Mbeya chini

ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI).

Aidha, utekelezaji wa ujumla wa miradi ya PPP umegharimu jumla ya shilingi bilioni 10.49 ambapo kiasi cha shilingi milioni 134.5 zimetolewa kutoka kwenye mfuko wa PPP na shilingi bilioni 10.35 zimetoka katika sekta zinazotekeleza miradi husika.

| Jina la Mradi | Kiasi cha Fedha Kilichotumika |
|---|---|
| Mradi wa Barabara ya Chalize - Kibaha - Morogoro (km 205) | 8,940,696,000 |
| Miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba - MSD | 1,010,222,537 |
| mradi wa ujenzi wa kituo cha mazoezi tiba Mbweni Dar es Salaam chini ya Taasisi ya Mifupa ya MOI | 171,236,000 |
| PPP Facilitation Fund (mradi wa ukaguzi wa lazima kwa vyombo vya moto) | 134,500,000 |
| Ocean Road Cancer Institute | 230,000,000 |
| **JUMLA** | **10,486,654,537** |

### 2.4. Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo

Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo ili kuongeza tija, ufanisi na uwajibikaji katika uratibu na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Aidha, katika kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi nchini, Serikali imeendelea kuongeza na kuboresha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ikiwemo Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS). Aidha, Serikali huzingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 katika utekelezaji wa shuguli za ufuatiliaji na tathmini.

#### 2.4.1. Ufuatiliaji wa Miradi katika kipindi cha Mwaka 2022/23

Hadi kufikia Desemba, 2022, jumla ya miradi 112 ilifuatiliwa na kufanyiwa tathmini ambapo miradi nane (8) ni ya kielelezo na miradi 104 ni ya kimkakati. Miradi ya kielelezo iliyofuatiliwa ni: ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR); kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (MW 2,115); uboreshaji wa shirika la ndege Tanzania; ujenzi wa madaraja ya juu katika jiji la Dar es Salaam (Uhasibu, Chang’ombe na daraja la bandari); ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi; ujenzi wa Kiwanda na Uendelezaji wa Shamba la Miwa Mkulazi – Mbigiri Estate; ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP); ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa; na eneo maalum la uwekezaji Bagamoyo. Miradi ya kimkakati iliyofuatiliwa inatekelezwa katika sekta za kukuza uchumi, huduma za jamii na utawala bora, uwajibikaji na utoaji haki. Kwa upande wa sekta za kukuza uchumi, miradi iliyofuatiliwa ni ya viwanda (17), biashara (1), ujenzi (7), uvuvi (1), uchukuzi (4), kilimo (5), madini (1) na nishati (4). Sekta za Huduma ya Jamii zilizofuatiliwa ni afya

(7), elimu (9), na maji (41). Kwa upande wa utawala bora, uwajibikaji na utoaji haki inayojumuisha sheria, mambo ya ndani, habari na mawasiliano, na utawala jumla ya miradi nane (8) ilifuatiliwa.

### 2.4.2. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23

Katika zoezi la ufuatiliaji na tathmini changamoto mbalimbali zilijitokeza katika utekelezaji wa Mpango. Changamoto hizo zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni changamoto za jumla na changamoto mahsusi za miradi.

**Changamoto za Jumla**

(i) Ongezeko la bei za mafuta kutokana na ongezeko la mahitaji lililosababishwa na chumi za nchi nyingi kuanza kurejea katika hali ya kawaida baada ya kuanza kulegeza vikwazo vilivyowekwa kutokana na UVIKO-19 na vita baina ya nchi za Urusi na Ukraine. Ongezeko la bei za mafuta limesababisha kuongezeka kwa gharama na kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi;

(ii) Ongezeko la bei za bidhaa muhimu kwa ajili ya uzalishaji pamoja na usalama wa chakula nchini ikiwemo mbolea, ngano na kemikali muhimu zinazotumika viwandani kutokana na vita baina ya nchi za Urusi na Ukraine;

(iii) Kuchelewa kukamilika kwa miradi kutokana na kutokufika kwa wakati kwa vifaa na bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kulikosababishwa na kuathirika kwa mnyororo wa ugavi duniani (global supply chain disruptions) kutokana na UVIKO-19 na vita baina ya nchi za Urusi na Ukraine;

(iv) Kukosekana kwa wabia wa kutekeleza miradi iliyoandaliwa na kutangazwa kwa ajili ya kutekelezwa kwa utaratibu wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi;

(v) Wigo mdogo wa kodi unaotokana na baadhi ya biashara kutokuwa rasmi na hivyo kupunguza mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango; na

(vi) Baadhi ya wafanyabiashara kukwepa kodi hususan kupitia njia za magendo, kutokutoa stakabadhi za kielektroniki (EFD receipt) wakati wa mauzo.

**Changamoto Mahsusi**

(i) Upungufu wa rasilimali watu hususan wahandisi wa kusimamia utekelezaji wa miradi pamoja na wataalamu wa uendeshaji wa mitambo na vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa;

(ii) Watekelezaji wa miradi kuchelewa kukamilisha taratibu za utoaji wa Cheti cha Msamaha wa Kodi hali inayosababisha kuongezeka kwa gharama za mradi (madai ya riba) na kuchelewa kwa kutekeleza mradi;

(iii) Usanifu duni wa mradi hali inayosababisha kuongezeka kwa mawanda, gharama na muda wa utekelezaji wa miradi;

(iv) Usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa mikataba na mipango kazi kwa baadhi ya watekelezaji wa miradi;

(v) Kuchelewa kwa malipo ya makandarasi kunakosababishwa na

kutowasilishwa kwa nyaraka muhimu za kuwezesha kufanyika kwa malipo kwa wakati hali inayosababisha malimbikizo ya riba na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi;

(vi) Usimamizi na uratibu kwa baadhi ya taasisi kufanyika katika ngazi ya makao makuu bila kushirikisha wasimamizi waliopo katika eneo la mradi hali inayosababisha miradi kuchelewa, kuongeza gharama na kupunguza ufanisi katika malengo ya mradi;

(vii) Ushirikishwaji mdogo wa wadau muhimu wa mradi katika kipindi cha maandalizi hali inayosababisha kubadilika kwa mawanda ya kazi wakati wa utekelezaji; na

(viii) Kuchelewa kwa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi.

### 2.4.3. Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto

(i) Kuendelea na hatua za kukabiliana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa ruzuku, kupunguza viwango na idadi ya tozo na kuogeza jitihada za kuongeza uwezo wa Akiba ya Kimkakati ya Hifadhi ya Mafuta (National Strategic Petroleum Reserves)

(ii) Kuendelea na hatua za kukabiliana na ongezeko la bei za bidhaa muhimu kwa ajili ya uzalishaji pamoja na usalama wa chakula nchini ikiwemo kupitia sera za kibajeti mfano; kupunguza tozo na kodi, utoaji ruzuku (mbolea na mafuta) kwa bidhaa muhimu na kuchukua hatua za kuongeza uzalishaji wa bidhaa husika nchini (mfano ngano na mbolea);

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuongeza mapato ya ndani na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia Mpango;

(iv) Kuendelea kupanga maeneo ya kipaumbele kwa kuzingatia rasilimali fedha zilizopo;

(v) Kuendelea kuhakikisha kuwa malipo ya hati za madai yanafanyika ndani ya muda uliokubalika kimkataba;

(vi) Kuchukua hatua za kisera na kiutawala ili kuendelea kupambana na athari za mgogoro katika mnyororo wa ugavi duniani ikiwemo kutumia zaidi malighafi, vifaa na wataalamu wa ndani kwa maeneo yote ambayo hakuna ulazima wa huduma hizo kutoka nje ya nchi na usimamizi madhubuti wa uagizaji na uhifadhi wa malighafi na vifaa vinavyoagizwa kutoka nje (appropriate investory management);

(vii) Kuendelea kujenga uwezo wa Mafungu ili kuyawezesha kuandaa miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ili ijumuishwe katika Mpango;

(viii) Kuendelea kuajiri wahandisi na wataalamu watakaosimamia utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo;

(ix) Kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya ndani, kubuni vyanzo vipya vya mapato na kutafuta masoko ya bidhaa nje ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia Mpango na Bajeti. Aidha, Serikali

inaendelea na kufuatilia mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Taasisi mbalimbali ili kuweza kutekeleza miradi ya kipaumbele;

(x) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki; na

(xi) Kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji wa vifaa vya ujenzi ili kukidhi mahitaji ya soko yaliyoongezeka.

# SURA YA TATU

# MIRADI YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2023/24

## 3.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea miradi ya kipaumbele itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Uandaaji wa Mapendekezo ya Serikali ya Mpango umezingatia hatua za kimkakati zilizoainishwa katika Mpango Kazi wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26. Hivyo, utekelezaji madhubuti wa hatua hizo utafanikisha kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

## 3.2. Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

### 3.2.1. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022;

(ii) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya asilimia 3.0 hadi asilimia 7.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 11.5 mwaka 2022/23;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 3.2.2. Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2023/24

Misingi itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli kiuchumi;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili;

(iii) Kuendelea kuhimili athari za kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la ndani na nje;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa hali ya utoshelevu wa chakula nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

## 3.3. Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2023/24

### 3.3.1. Miradi ya Kielelezo

**(i) Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa reli ya Standard Gauge kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) na Morogoro - Makutupora (km 422); kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341); Makutupora – Tabora (km 368); Tabora - Isaka (Km 165); na kuanza ujenzi wa kipande cha Tabora - Kigoma (Km 506) na Uvinza (Tanzania) – Musongati – Gitega (Burundi) (Km 282); ununuzi wa injini, mabehewa na mitambo kwa ajili ya matengenezo ya njia; kugharamia uendeshaji wa reli ya *Standard Gauge*; kuendelea na ugharamiaji wa mafunzo ya wataalamu wa uendeshaji na usimamizi wa treni ya *Standard Gauge;* kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli kwa sehemu za Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) na sehemu ya Uvinza – Malagarasi km 156); Isaka - Rusumo – Kigali (km 495) sehemu ya Isaka – Rusumo (km 371); *na* ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa reli kipande cha Tabora - Kigoma. Jumla ya shilingi bilioni 1,196 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa bwawa (main dam); ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels); ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (Power House); ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard); na ujenzi wa nyumba za makazi na ofisi. Jumla ya shilingi trilioni 1.6 fedha za ndani zimetengwa

**(iii) Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege tano (5) mpya ambapo ndege moja (1) ni aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, ndege mbili (2) aina ya *Boeing 737-9*, ndege moja (1) ya mizigo aina ya *Boeing 767-300F* na ndege moja (1) aina ya *De Havilland Dash 8 Q400*; ukarabati na ununuzi wa vifaa vya karakana za matengenezo ya ndege (Hangar) za JNIA na KIA; kukamilisha ujenzi wa hanga jipya la kisasa katika kiwanja cha JNIA; kugharamia mahitaji ya awali ya uendeshaji wa ndege tano (5) ambazo ni Boeing 787 – 8, Boeing 737- 9 mbili (2), Boeing 767 - 300F na Dash 8 Q400 (1); ununuzi wa vifaa vya kuhudumia ndege na abiria viwanjani; ukarabati wa majengo ya ofisi ya ATCL makao makuu na lililopo kiwanja cha ndege cha JNIA Terminal I; ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA pamoja na ujenzi wa eneo la mafunzo ya awali kwa wanaanga; ununuzi wa ndege aina ya *Boeing Business Jet 737 – 7*; na ujenzi na ukarabati wa majengo kwa ajili ya kuhifadhi mizigo katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Songwe. Jumla ya shilingi bilioni 603.25 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 4015: Daraja la JPM - Kigongo – Busisi (Mwanza)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa daraja pamoja na barabara

unganishi (km 1.66). Jumla ya shilingi bilioni 10 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ikiwemo kuhamisha makaburi zaidi ya 400 kukamilisha ujenzi wa nyumba za fidia kwa wananchi; kuanza ujenzi wa bomba; kuendelea na ujenzi wa kambi za wafanyakazi; kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha mabomba; kuanza ujenzi wa bandari na matenki; kuanza ujenzi wa gati na kuendelea kuchangia hisa za kampuni. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi;**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha malipo ya fidia ya kuamisha makaburi katika eneo la mradi; kujenga uwezo wa namna ya kutekeleza shughuli zilizopangwa; kufanya maandalizi ya kuomba leseni na kufanya *Pre-FEED study* katika eneo la mradi. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa

**(vii) Mradi Na. 3171: Makaa ya Mawe (Mchuchuma - Njombe)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi (PAP); na kuanza kuzalisha makaa ya mawe. Jumla ya shilingi bilioni 3.03 fedha za ndani zimetengwa.

**(viii) Mradi Na. 1122: Magadi Soda Engaruka**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi (PAP), kuendelea na hatua za kutafuta mwekezaji wa mradi; Kufanya uhakiki wa taarifa zilipo katika tafiti zilizofanyika (Brine Resource appraisal and Techno-economic study review); na kulipa leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi bilioni 2.47 fedha za ndani zimetengwa.

**(ix) Mradi Na. 3165: Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) – Njombe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 62.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi Na. 3167: Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222) - Njombe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 57.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(xi) Mradi Na. 3115: Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia Eyasi – Wembere:** Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuchakata na kutafsiri taarifa za mfumo wa 2D; kuandaa moduli ya mfumo wa 3D kwa kutumia taarifa za kijiofizikia; na kukusanya taarifa na kufanya tathmini ya kijiokemia juu ya uwepo wa viashiria vya miamba inayozalisha mafuta (hydrocarbon seep detection). Jumla ya shilingi bilioni 3.1 fedha za ndani zimetengwa.

**Mnazi Bay Kaskazini:** Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya tathmini ya kina ya *data* za mitetemo za mfumo wa 2D na hali ya sakafu ya bahari; kukamilisha Mpango wa Kina wa Uchorongaji visima (Detailed Drilling Plan); kumpata Mkandarasi atakayechoronga kisima pamoja na watoa huduma nyingine wezeshi; na kufanya tathmini za kijiolojia na kijiofizikia kwa sampuli zitakazokusanywa kutoka kwenye visima vitakavyochorongwa. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(xii) Mradi Na. 4702: Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi – Kilwa Masoko**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko ambapo jumla ya shilingi bilioni 200.62 fedha za ndani zimetengwa.

**(xiii) Mradi Na. 4429: Ununuzi wa Meli za Uvuvi**

Shughuli itakayotekelezwa ni ununuzi wa meli mbili (2) zitakazovua katika ukanda wa uchumi wa Bahari (EEZ) ambapo jumla ya shilingi bilioni 11.9 fedha za nje zimetengwa.

**(xiv) Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha matayarisho ya shamba na kupanda miwa katika eneo lililobaki lenye ukubwa wa hekta 626 ili kukamilisha hekta 3,600 zinazotakiwa kulimwa; kuweka mfumo wa umwagiliaji katika shamba lenye ukubwa wa hekta 845; ujenzi wa bwawa la umwagiliaji lenye ukubwa wa mita za ujazo 3,500; kukamilisha ujenzi wa kiwanda kipya cha sukari; na ununuzi wa vifaa vya kupakia na kusafirisha miwa kwenda kiwandani. Jumla ya shilingi bilioni 60.80 fedha za ndani zimetengwa.

**(xv) Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

**Mradi Na. 4920: Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara katika eneo lenye viwanda. kukamilisha malipo ya fidia na kufanya usanifu wa kina wa miundombinu wezeshi ya ndani. Jumla ya shilingi bilioni 9.7 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 3.3.2.1. Kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji

**Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma**

**A. Reli**

(i) **Mradi Na. 4216: Ukarabati wa Njia Kuu za Reli**

Shughuli zitakazotekelezwa katika awamu ya pili ni: Kukamilisha ukarabati wa maeneo yaliyobaki katika vipande vya Makutupora - Manyoni na Kitaraka – Malongwe - Igalula; na kuboresha vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka. Jumla ya shilingi bilioni 7.08 fedha za nje zimetengwa.

(ii) **Mradi Na. 4213: Mfuko wa Reli**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uundaji wa vichwa viwili (2) vya treni vya njia kuu aina ya 88U na vichwa saba (7) vya sogeza aina ya 64XX; kuanza ukarabati wa njia ya reli ya Tabora - Kigoma (Km 411), Kaliua - Mpanda (Km 210), Tabora – Isaka - Mwanza (Km 385), Tanga - Arusha (Km 470) na Kilosa – Gulwe; ujenzi wa madaraja katika kipande cha Godegode - Gulwe; ufufuaji wa njia za reli zilizofungwa za Kilosa - Kidatu (Km 108) na Manyoni-Singida (Km 115); ukarabati wa mabehewa 120 ya mizigo na 12 ya abiria; ununuzi wa mabehewa ya mizigo 245, mabehewa ya abiria 22 na injini nane (8); kupima na kuweka alama katika maeneo ya reli nchini; na ufufuaji wa mgodi wa kuzalisha kokoto wa Pangani (Tanga) na Tumbi (Tabora) na Mgodi wa Tura. Jumla ya shilingi bilioni 294.80 fedha za ndani zimetengwa.

(iii) **Uboreshaji wa Reli ya TAZARA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa vifaa na mitambo (Tamping Machine moja, Excavator moja) kwa mgodi wa kokoto wa Kongolo (Mbeya), Mataruma ya Mbao vipande 20,000, *Railway Scanner* moja, *Railway Weighbridge* moja na Ujenzi wa njia mbili (2) za reli katika stesheni ya Tunduma. Jumla ya shilingi bilioni 13.96 fedha za ndani zimetengwa.

**B. Barabara na Madaraja**

**Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi**

**(a) Mradi Na. 4147: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 68). Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4113: Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena (km 220)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa barabara za Ifakara – Kihansi (km 124) sehemu ya Ifakara – Mbingu (km 50) na Kibena - Lupembe - Madeke (km 50). Jumla ya shilingi bilioni 6.31 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.82 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na.4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235***)*

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Sanzate – Natta (km 40), Natta – Mugumu (km 45) na Tarime – Mugumu (km 50) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 3.52 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 100)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Itoni – Lusitu (km 50) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.01 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4193: Handeni – Kibaya – Singida (Km 460)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Handeni – Kiberashi (km 50) vipande vya Handeni – Mafuleta (km 20) na Mafuleta – Kiberashi (km 30) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4195: Barabara ya Dodoma – Iringa (km 273.3)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass - km 7.3) kwa kiwango cha lami; na kuendelea kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma (km 266). Jumla ya shilingi bilioni 1.45 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4196: Barabara ya Dodoma – Babati (km 310)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Dongobeshi – Dareda (km 60); na kukamilisha usanifu wa kina wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass - km 15.5). Jumla ya shilingi bilioni 2.53 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4188: Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni (km 489.9)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Noranga – Itigi Mkiwa (km 56.9), Makongolosi – Rungwa – Noranga (km 356) Sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 50) na barabara za mji wa Itigi kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.74 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4112: Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265.1)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kazilambwa – Chagu (km 36); na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Uvinza – Malagarasi (km

51.1) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi milioni 840 fedha za ndani na shilingi bilioni 19.27 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4002: Barabara ya Mtwara – Newala - Masasi (km 225)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mnivata – Tandahimba - Masasi (km 160) sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100) na Mitesa – Masasi (km 60). Jumla ya shilingi bilioni 1.01 fedha za ndani na shilingi bilioni 11 fedha za nje zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 4003: Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Likuyufusi – Mkenda sehemu ya Likuyufusi – Mhukuru (km 60) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 7.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 4107: Barabara za Kuelekea kwenye Mradi wa Kufua Umeme wa Maji katika Mto Rufiji (km 406)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) kwa kiwango cha lami; ukarabati kwa kiwango cha changarawe barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Striggler’s Gorge; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178), sehemu ya Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4). Jumla ya shilingi bilioni 9.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 4174: Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (Km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100), sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.20) na Nachingwea – Ruangwa (km 57.6). Jumla ya shilingi bilioni 8.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(o) Mradi Na. 4041: Barabara ya Kitahi – Lituhi na Daraja la Mnywamaji (km 85)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kitahi – Lituhi na Daraja la Mnywamaji ambapo Lot 1 itahusisha sehemu ya Amanimakolo – Ruanda na Ruanda – Ndumbi Port. Jumla ya shilingi bilioni 9.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani (km 50) kwa kiwango cha lami; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Pangani/Tungamaa – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami pamoja na Daraja la Pangani na barabara unganishi. Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 27.56 fedha za nje zimetengwa.

**(q) Mradi Na. 4152: Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 1.02 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.0 fedha za nje zimetengwa.

**(r) Mradi Na. 4199: Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (Mbeya Bypass) (km 273.5)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa sehemu ya Uyole - Ifisi (km 29) kuwa njia mbili na mchepuo wa Mbeya (Uyole – Songwe (km 40). Jumla ya shilingi bilioni 13.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(s) Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3) na barabara kuelekea hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe (km 4) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.72 fedha za ndani zimetengwa.

**(t) Mradi Na. 4194: Barabara ya Makambako – Songea (Songea Bypass) (km 381)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukarabati barabara ya Makambako – Songea sehemu ya Lutikila – Songea (km 95.18) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 1.1 fedha za ndani na shilingi bilioni 21.42 fedha za nje zimetengwa.

**(u) Mradi Na. 4123: Barabara ya Dumila – Kilosa Road (km 141)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami; na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Rudewa – Kilosa (km 24). Jumla ya shilingi bilioni 1.32 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 4023: Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza ujenzi wa barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 8.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(w) Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza ujenzi wa barabara sehemu za Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152), Kizungu – Muze (km 12) kwa kiwango cha lami na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25). Jumla ya shilingi bilioni 7.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Kamunazi – Kasulo – Bugene na Kyaka – Mutukula (km 133), sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60), na Kagera Sugar Jct – Kakunyu sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25). Jumla ya shilingi bilioni 9.51 fedha za ndani zimetengwa.

**Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**(a) Mradi Na. 4124: Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.51 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 84.8)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16), Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8); Sanya Juu – Kamwanga sehemu ya Alerai – Kamwanga (km 26). Jumla ya shilingi bilioni 7.33 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4129: Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 242.2)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ukarabati wa barabara sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 150); na ujenzi wa barabara ya Nyakasanza – Kobero (km 58). Jumla ya shilingi milioni 560 fedha za ndani na shilingi bilioni 16.72 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4111: Nyakahura – Kumubuga –Rulenge – Kabanga Nickel – Murugarama (km 141)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza ujenzi wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Mpanda – Mishamo – Uvinza sehemu ya Vikonge - Luhafwe (km 25); na Luhafwe – Mishamo (km 25); sehemu ya Kibaoni – Sitalike (km 71) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 21.24 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4155: Barabara ya Nyanguge – Musoma/Kisesa Bypass (Km 214.25)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4). Jumla ya shilingi milioni 530 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4162: Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 121)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa mchepuo wa barabara ya Maswa (km 11). Jumla ya shilingi bilioni 2.02 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 379.25**)

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara za Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Junction (59.35), Kibondo Junction – Kabingo (62.5), na Nduta Junction – Kibondo (25.9); na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 48) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 7.22 fedha za ndani na shilingi bilioni 48.76 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4027: Barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.10);**

Shughuli itakayotekelezwa ni kujenga barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.10) sehemu ya Ngana – Ileje (km 52) na barabara za Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4103: Barabara ya Geita - Bulyanhulu - Kahama (km 170)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara ya Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa na shilingi bilioni 5.0 fedha za nje zimetengwa.

**Barabara za Mikoa na Kupunguza Msongamano**

**(a) Mradi Na. 4138: Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6); barabara ya Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km

14.66) sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 4). Jumla ya shilingi bilioni 8.79 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4132: Barabara za Mikoa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukarabati kilometa 693.68 kwa kiwango cha changarawe; kujenga kilometa 72.2 kwa kiwango cha lami; na kujenga madaraja 34 katika Mikoa 26 nchini. Jumla ya shilingi bilioni 67.64 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4285: Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka**

**Awamu ya Kwanza**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuboresha miundombinu ya mabasi yaendayo haraka iliyojengwa katika awamu ya kwanza katika eneo la Jangwani. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani na bilioni 12 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Pili**

(i) Ujenzi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa *Lot 1* inayohusisha barabara yenye urefu wa km 20.3 (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu), Bendera Tatu – Kariakoo, Sokoine – Zanaki, Kawawa Road – Morogoro Road (Magomeni), Chang’ombe Road – Kilwa Road). Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani na bilioni 5.0 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Tatu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka awamu ya Tatu inayohusisha barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere hadi Gongo la Mboto zenye jumla ya kilometa 23.3 na kituo kikuu cha mabasi Kariakoo, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA. Jumla ya shilingi milioni 1.0 fedha za ndani na bilioni 12.0 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Nne na Tano**

Awamu ya Nne itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi, Bagamoyo - Tegeta na barabara ya Sam Nujoma (Ubungo - Mwenge) zenye jumla ya km 30.12. Jumla ya shilingi bilioni 1.275 fedha za ndani na shilingi bilioni 11.63 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4161: Ujenzi wa Barabara za Juu (*Flyover*) Jijini Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa *flyovers* katika makutano ya barabara ya Magomeni, Mwenge,Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire na Makutano ya Barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct); na kuendelea na ununuzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Jumla ya shilingi milioni 320 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.1 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4146: Barabara za Mzunguko Katika Jiji la Dodoma**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60), Upanuzi wa barabara za mzunguko ndani ya jiji: Bahi R/About - Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3); na Ujenzi wa barabara ya Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) Road (km 18). Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 35.09 fedha za nje zimetengwa.

**Barabara za Vijijini na Mijini**

**(a) Mradi Na. 4170: Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa barabara zenye kiwango cha lami km 344.6, barabara za changarawe km 8,529.83; madaraja makubwa 239, kalvati 246 na mifereji ya maji yenye urefu wa km 28.13 na matengenezo ya barabara km 21,109. Jumla ya shilingi bilioni 710.31 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4169: Mradi wa Uboreshaji wa Barabara maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (Agri-Connect Programme)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza matengenezo ya barabara za lami zenye urefu wa km 63.9 kwa ajili ya uboreshaji wa barabara katika maeneo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo (Agri-Connect Programme) cha Kahawa na Mbogamboga katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Jumla ya shilingi bilioni 42.0 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6370: Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania (Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness-TACTIC)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu Msingi ya Mijini katika Halmashauri 12 ambazo ni Halmashauri za Majiji ya Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya; Halmashauri za Manispaa za Kigoma, Ilemela, Kahama, Morogoro, Sumbawanga, Songea na Tabora na Halmashauri ya Mji Geita. Jumla ya shilingi bilioni 74.10 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4021: Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 400 katika wilaya sita (6) za Iringa, Mufindi, Ruangwa, Mbogwe, Handeni na Kilolo. Jumla ya shilingi bilioni 96.8 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6209: Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuchochea maendeleo ya wananchi kwa

kuchangia fedha katika miradi inayotekelezwa katika majimbo kupitia mfuko wa maendeleo ya Jimbo. Jumla ya shilingi bilioni 15.99 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 6244: Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha miradi inayotekelezwa na kuanza ujenzi wa miradi ambayo haijaanza utekelezaji. Jumla ya shilingi bilioni 40.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Uboreshaji wa Bonde la Mto Msimbazi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa miundombinu ya kupunguza mafuriko katika Bonde la Msimbazi ambapo jumla ya shilingi bilioni 106.7 fedha za nje zimetengwa.

**Ujenzi wa Nyumba za Serikali na Madaraja**

**(a) Mradi Na. 4126: Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi (km 25) katika daraja la Sibiti (Singida) na kuanza ukarabati wa madaraja ya Kirumi (Mara) na Sukuma (Mwanza); kuanza ujenzi wa madaraja ya Mirumba (Katavi), Simiyu (Mwanza), Sanza (Singida), Mkenda (Ruvuma), Mpiji Chini (Dar es Salaam); na Mtera, Godegode (Dodoma), Mitomoni (Ruvuma), Malagarasi Juu (Kilelema–Kigoma). Jumla ya shilingi bilioni 13.93 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Serikali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa nyumba 20 za viongozi na nyumba 100 za watumishi jijini Dodoma, nyumba za makazi za watumishi katika eneo la Temeke Kota Dar Es Salaam, nyumba za makazi za watumishi katika eneo la Magomeni Kota; kuendelea na ukarabati wa nyumba za Viongozi pamoja na watumishi wa umma maeneo mbalimbali nchini; ukarabati wa karakana za TBA kwa ajili kutengeneza samani katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dar Es Salaam na Mbeya pamoja na karakana 12 za TEMESA zilizopo Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Dodoma, Pwani na Vingunguti; kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; na kuendelea na ujenzi wa karakana mpya ya kisasa ya magari jijini Dodoma pamoja na kuanzisha karakana za wilaya katika wilaya za Simanjiro, Masasi, Ukerewe, Chato, Mafia na Kyela. Jumla ya shilingi bilioni 47.55 fedha za ndani zimetengwa.

### C. Usafiri Majini

**Meli**

(i) **Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu; kukamilisha ukarabati wa meli za MV Umoja na MT. Sangara; kuanza ujenzi wa meli mpya (Wagon ferry) yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria na meli mpya (Barge/Cargo ship) ya kubeba shehena ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 2,800 na meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika; kuanza ujenzi wa chelezo ya kubeba meli wakati wa matengenezo katika Ziwa Tanganyika; kuanza ukarabati wa Meli ya MV Liemba, MV Sengerema, MT. Ukerewe na MT. Nyangumi; na ukarabati wa boti moja (1) ya mwendokasi (Sea Warrios) katika Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kusaidia kazi za uokozi sambamba na usafirishaji wa watalii wanaotembelea kisiwa cha Gombe. Jumla ya shilingi bilioni 284.59 fedha za ndani zimetengwa.

(ii) **Mradi Na. 4201: Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa kituo cha Kanda cha uokozi Mwanza; uboreshaji wa vituo vitatu (3) vya Kitaifa vya Utafutaji na Uokozi vya MRCC-Musoma, Ukerewe na Kanyala; uboreshaji wa Mfumo wa Simu za Dharura; uboreshaji wa vituo vya utafutaji na uokozi; na kuendelea na ununuzi wa vifaa ikiwemo ununuzi wa boti, kamera, samani, X-Band rada, *maritime radio* - VHF/MHF na HF, GMDSS, LRIT, navigation dividers, vishikwambi na darubini kwa ajili ya vituo na ofisi zilizoanzishwa. Jumla ya shilingi bilioni 12.26 fedha za nje zimetengwa.

**Vivuko**
(i) **Mradi Na. 4125: Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na upanuzi wa maegesho 11 katika vivuko vya Magogoni - Kigamboni upande wa Kigamboni, Kilambo - Namoto, Utete - Mkongo, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome, Irunda - Luchelele, Kisorya - Rugezi, Ilagala - Kajeje, Rusumo - Nyakiziba, Musoma - Kinesi, na Kasharu – Buganguzi; kujenga na kuimarisha miundombinu ya vivuko pamoja na majengo ya abiria katika vivuko sita (6) vya Kahunda - Maisome, Msanga Mkuu - Msemo, Kisorya - Rugezi, Bezi - Bukimwi, Nyakarilo - Kome na Bugolora – Ukara; kujenga maegesho katika vivuko vya Kayenze – Kanyinya, Muleba – Ikuza, Ijinga - Kahangala (Magu), Bwiro - Bukondo(Ukerewe) na Chato – Nkome katika Kivuko cha Zumacheli; kusimika na kuimarisha mifumo ya kukatia tiketi katika vivuko vya Magogoni - Kigamboni; Kigongo - Busisi, Kisorya - Rugezi, Pangani - Bweni na Ilagala – Kajeje; na kufanya ukarabati wa vivuko 6 na kujenga maegesho katika maeneo ya Buyagu, Mbalika, Ilunda, Luchelele, Bukimwi, Kisorya, Rugezi, kahunda and Maisome. Jumla ya shilingi bilioni 3.003 fedha za ndani zimetengwa.

(ii) **Mradi Na. 4139: Ujenzi wa Vivuko Vipya**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia, Magogoni – Kigamboni, Buyagu - Mbalika na kufanya manunuzi ya vitendea kazi vya karakana za TEMESA. Jumla ya shilingi bilioni 6.78 fedha za ndani zimetengwa.

(iii) **Mradi Na. 4144: Ukarabati wa Vivuko**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukarabati wa vivuko MV Musoma, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kyanyabasa, MV Tanga, MV Kitunda, MV Kazi, MV Magogoni na MV Kilombero II. Jumla ya Shilingi bilioni 6.59 fedha za ndani zimetengwa.

**Bandari**

**(i) Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam**

**(a) Bandari ya Dar es Salaam.**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea uchimbaji wa kina na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli na uboreshaji wa Gati Na. 8 – 11; na kuendelea na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati Na. 12 -15. Jumla ya shilingi bilioni 157.06 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Bandari ya Tanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Tanga na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya gati la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani (Tanga). Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Bandari ya Mtwara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na maboresho ya maeneo ya kuhudumia shehena za mizigo ambapo jumla ya shilingi bilioni 5.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Bandari ya Bagamoyo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa bandari ambapo jumla ya shilingi bilioni 30.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Bandari Kavu katika Eneo la Ruvu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa yadi na sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta tano (5) na barabara ya Vigwaza – Kwala (km 15.5). Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Ziwa Victoria**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na uboreshaji wa Bandari za Bukoba, Kemondo Bay na Mwanza North. Jumla ya shilingi bilioni 1.44 fedha za ndani

zimetengwa.

**(g) Ziwa Tanganyika**
**Bandari ya Kigoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa *Access Road, Cargo Shed, Passenger Wharf and Lounge*); na kuendelea na ujenzi wa *Passenger Lounge* na ukuta wa mizigo wa *Lighter Quay* katika Bandari ya Kibirizi na gati la Bandari ya Ujiji. Jumla ya shilingi bilioni 12.7 fedha za ndani zimetengwa.

**D. Usafiri wa Anga**

**(a) Mradi Na.6267 : *Institutional Support***

(i) **Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (JNIA-TB III) na Kuboresha Huduma katika Viwanja Vingine vya Ndege**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu katika jengo la tatu la abiria (JNIA TB III) unaojumuisha matengenezo ya mitambo na mifumo mbalimbali ikiwemo lifti 14, eskaleta saba (7), *travelators* mbili (2) za abiria, mashine 20 za ukaguzi wa abiria na mizigo, mifumo ya tiketi za abiria na mifumo ya TEHAMA; usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Arusha; ununuzi wa gari moja (1) la Zimamoto na Uokoaji; kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mwanza; kuanza kwa ujenzi wa mnara wa kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege Bukoba; na kuanza ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha ndege Mtwara. Jumla ya shilingi bilioni 21.0 fedha za ndani zimetengwa.

(ii) **Chuo cha Bahari Dar es Salaam - DMI**

Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha malipo ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia (*full motion simulator)*. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

(iii) **Mradi wa Ununuzi mitambo katika viwanja vya ndege**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua mitambo ya kisasa (Doppler Very High Frequency Omnidirectional Radio Range (DVOR), Distance Measuring Equipment (DME) na Instrument Landing Systems (ILS)) ili kuwasaidia marubani kutua kwa usalama katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, AAKIA, Mwanza na Songwe. Jumla ya shilingi bilioni 78.16 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4209: Kiwanja cha Ndege Mwanza**

Shughuli itakayotekelezwa ni: Ujenzi na upanuzi wa Maegesho ya Ndege na ujenzi wa jengo jipya la abiria. Jumla ya shilingi bilioni 5.83 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4220: Kiwanja cha Ndege Mtwara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege; na ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari; Jumla ya shilingi bilioni 5.55 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4156: Kiwanja cha Ndege Kigoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga jengo la abiria na ukarabati wa miundombinu (upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani); kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege; na kujenga uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Jumla ya shilingi bilioni 5.06 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.34 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4221: Kiwanja cha Ndege Sumbawanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari; na kufunga taa na mitambo ya kuongozea ndege. Jumla ya shilingi milioni 726.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.34 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4222: Kiwanja cha Ndege Shinyanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari; kufunga taa na mitambo ya kuongozea ndege; na ujenzi wa uzio wa usalama. Jumla ya shilingi milioni 726.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.34 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Songwe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa jengo la abiria na mifumo ya ulinzi; kukamilisha kufunga taa za kuongozea ndege; kukarabati tabaka la juu la lami katika barabara ya kutua na kurukia Ndege, barabara ya kiungio, ujenzi wa uzio wa usalama na ujenzi wa maeneo ya usalama (RESA) Jumla ya shilingi bilioni 11.12 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita, Iringa, Ruvuma (Songea), Simiyu, *Lake* Manyara, Tanga, Moshi, Lindi na Mara (Musoma); kujenga uzio wa usalama na barabara ya ukaguzi katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; na kujenga barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami katika kiwanja cha ndege cha Nachingwea. Jumla ya shilingi bilioni 28.36 fedha za ndani na shilingi milioni 544.50 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Msalato Jijini Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 2.11 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.37 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4158: Kiwanja cha Ndege Mpanda**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza usanifu wa jengo la abiria. Jumla ya shilingi milioni 13.31 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 4159: Kiwanja cha Ndege Tabora**

Shughuli itakayotekelezwa ni ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa uwanja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Jumla ya shilingi milioni 728.66 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.34 fedha za nje zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 4210: Kiwanja cha Ndege Arusha**

Shughuli itakayotekelezwa ni kujenga uzio wa usalama. Jumla ya shilingi milioni 266.22 fedha za ndani zimetengwa.

**E. Hali ya Hewa**

**(a) Mradi Na. 4290: Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa vifaa na mitambo ya kisasa kwa ajili ya utabiri wa hali ya hewa ikijumuisha rada mbili (2) za kwenye maji zitakazofungwa Tanga na Pemba kwa ajili upatikanaji wa taarifa ya hali ya hewa katika Bahari ya Hindi, mitambo ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe (AWS) na vifaa vya kupima mgandamizo wa hali ya hewa, kiasi cha joto na unyevunyevu; kukamilisha malipo ya rada mbili (2) za hali ya hewa pamoja na ufungaji wake; kuendelea na ujenzi wa kituo cha kanda ya mashariki (Dar es Salaam) na kituo cha kutoa tahadhari ya matukio ya *Tsunami*; kuendelea na ujenzi wa maabara ya uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa; kuanza kwa ujenzi wa ofisi za makao makuu Jijini Dodoma; uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Hali ya hewa; na ukarabati wa vituo vitatu (3) vya hali ya hewa. Jumla ya shilingi bilioni 31.5 fedha za ndani zimetengwa.

**F. Miundombinu ya kujifunzia**

**(b) Mradi Na.6377 Ujenzi wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia**

**(i) Chuo cha Taifa cha Usafirishaji – NIT**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukamilishaji wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo kwa

kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) lenye Maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 450, madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,653 pamoja na ofisi za watumishi katika kampasi ya Mabibo – Dar-es-Salaam; kuanza ujenzi wa awamu ya kwanza ya miundombinu ya Kituo Atamizi cha Mafunzo ya kuandaa mafundi mahiri wa teknolojia ya usafiri kwa njia ya Reli Tabora; ununuzi wa vifaa vya kufundishia kwa ajili ya mafunzo ya ufundi na teknolojia ya mafuta na gesi baharini; ujenzi wa jengo la kitaaluma la ghorofa nne (4) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,500 kwa wakati mmoja katika Kampasi ya Mabibo Dar es Salaam; ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uanzishwaji wa mafunzo na Kituo Atamizi cha kuandaa mafundi mahiri wenye ujuzi kwenye sekta ya usafiri wa majini, mafuta na gesi Kikwetu Lindi; na ununuzi wa vifaa vya mafunzo ya usafiri kwa njia ya maji. Jumla ya shilingi bilioni 1.86 fedha za ndani zimetengwa.

## G. Nishati

### Miradi ya Kufua Umeme

**(i) Mradi Na. 3168: Kufua Umeme wa Maji Kikonge (MW 300)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha upembuzi yakinifu; kufanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii, uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi na ulipaji wa fidia; kukamilisha usanifu wa mradi; na kuwapata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani.

**(ii) Mradi Na. 3169: Kufua Umeme wa Maji Malagarasi (MW 49.5)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kuendelea na ujenzi wa bwawa na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 54.5 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe – Kigoma. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 13.97 fedha za nje zimetengwa.

### Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme

**(i) Mradi Na. 3111: Uimarishaji wa Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization)**
Shughuli zitakazotekelezwa: Kujenga njia za kusafirisha umeme wenye msongo wa Kv 132 Ilala – Kurasini, Gongo la Mboto – Mbagala, Tabora – Shinyanga, Kasinga – Lushoto, Mkata – Kilindi, Tabora – Urambo, Ubungo – Chalinze – Hale na Kiyungi – Rombo; kujenga njia ya kusafirisha umeme wenye msongo wa Kv 220 Tunduru – Masasi, Kinyerezi – Mabibo – Ilala, Kinyerezi – kivule na Ibadakuli – Shinyanga; ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Makata (Tanga), Zegereni Mpanda (Rukwa), Imalilo Bariadi (Simiyu), Nguruka (Kigoma), Urambo (Tabora), Ilala, Ukerewe na Bunda Kibara; na kuongeza uwezo wa mashine umba katika vituo vya Dege Kigamboni, na Gongo la mboto; ulipaji wa fidia na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme wenye msongo wa kV 132 ambazo ni

Nyamongo – Serengeti, Musoma – Rorya, Nyakato-Sabasaba, Msamvu – Mvomero na msongo wa kV 220 ambazo ni Mwakibete-Chunya, Dundani-Pembamnazi, Pembamnazi-Dege, Kurasini-Dege, Bulyanhulu-Mbogwe, Buzwagi-Bukombe, Tagamenda-Kilolo, Songea-Mbinga na kituo cha kupoza umeme cha Manyoni; na upanuzi na ukarabati wa vituo vya Ubungo, Nyakato, Msamvu, Kunduchi, Mtwara, Mahumbika, Majani Mapana na Lusu. Jumla ya shilingi bilioni 400 fedha za ndani zimetengwa

**(ii) Mradi Na. 3179: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi.**

**Rufiji – Chalinze Kv 40**: Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme Chalinze. Jumla ya Shilingi bilioni 20 fedha za ndani zimetengwa.
**Kinyerezi - Chalinze kV 400:** Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha ulipaji fidia wananchi watakaopisha mradi na kuanza utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 40.0 fedha za ndani zimetengwa.

**Chalinze - Dodoma kV 400:** Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ulipaji fidia wananchi watakaopisha mradi kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme. Jumla ya shilingi bilioni 50.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 – North – West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi)**

**Awamu ya Kwanza: Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga:**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ulipaji fidia kwa wananchi waliopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo (Iringa, Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga) vya kupoza umeme; na kufanya upembuzi yakinifu kuhusu uwezo wa Mfumo wa Kusafirisha Umeme kwa ajili ya kuwezesha biashara ya umeme kati ya Tanzania na nchi jirani (SADC). Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 33.7 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Pili: Kigoma – Nyakanazi:** Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme; kujenga vituo vya kupoza umeme vya Nyakanazi na Kidahwe pamoja na njia za usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Jumla ya shilingi bilioni 7.2 fedha za nje zimetengwa

**(iv) Mradi Na. 3111: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Benaco - Kyaka**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 30.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 70.35 fedha za nje zimetengwa.

**(v) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi na kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi. Jumla ya shilingi bilioni 3.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Mradi Na. 3175: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme; na kituo cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo mkoani Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 7.64 fedha za nje zimetengwa.

**(vii) Mradi Na. 3113: Usambazaji wa Nishati Vijijini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuunganisha vijiji vilivyo salia ambavyo havijafikiwa na huduma ya umeme; kusambaza gesi ya kupikia katika maeneo ya vijiji vya mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani; kuwezesha ujenzi wa vituo vidogo 40 vya mafuta vijijini; na kupeleka umeme katika visiwa na maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa. Jumla ya shilingi bilioni 323.11 fedha za ndani na Shilingi bilioni 15.28 fedha za nje zimetengwa

**(viii) Mradi Na. 3180: Usambazaji wa Umeme Katika Vitongoji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa miundombinu ya usambazji wa umeme kwenye vitongoji vilivyosalia nchini ambapo jumla ya shilingi bilioni 40 fedha za ndani zimetengwa

**Miradi ya Gesi Asilia na Mafuta**

**(i) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)**

Shughuli itakayotekelezwa ni: kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study); na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii. Jumla ya shilingi milioni 938 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Uwezeshaji wa program ya nishati safi ya kupikia (Clean Cooking Energy)**

Shughuli zitakayotekelezwa ni: kuandaa mkakati wa nishati safi ya kupikia; na kutoa elimu kwa umma kuhusu nishati safi ya kupikia. Jumla ya shilingi milioni 900 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 3162: Usambazaji wa Gesi Asilia kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa mradi wa bomba la usambazaji wa gesi asilia kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach; kuanza ujenzi wa mradi wa bomba la usambazaji wa gesi asilia kutoka matoleo ya bomba kuu (BVS3) hadi Mnazi Mmoja mkoani Lindi; kuingia mkataba na mkandarasi wa ujenzi wa vituo vya CNG pamoja

na kuanza ujenzi; kuingia mkataba na mkamdarasi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwenda DUCE na Mlimani City; kuanza ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Ntorya kwenda Madimba; kuanza ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa DANGOTE, SAPPHIRE, ANRIC, WU ZHOU na NEELKANTH; na kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa usambazaji gesi asilia majumbani kwa mikoa ya Pwani na Lindi. Jumla ya shilingi bilioni 72.93 ya fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

#### 3.3.2.2. Mapinduzi ya TEHAMA

**(i) Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Kilometa 1,600 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Vituo vipya 15 vya kutolea huduma za Mkongo; ujenzi wa Mikongo ya Mwisho (last mile connectivity) kwenye taasisi 200 za Kimkakati; kuendelea na ujenzi wa mkongo wa majini kiasi cha kilomita 60 ili kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika; ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kutunzia Data Zanzibar, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama; kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni, na kukamilisha maandalizi ya kanuni na kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022. Jumla ya shilingi bilioni 103.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 4234: Anwani za Makazi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhakiki taarifa na kuweka miundombinu ya Anwani za Makazi katika Halmashauri 80, maeneo ya makundi maalum ikiwemo vituo vya bodaboda, wamachinga na kwenye maeneo ya Kimkakati nchini; kuboresha programu tumizi kulingana na mahitaji ya watumiaji; kuboresha Sera ya Posta ya Mwaka 2003, na kutunga sheria mahsusi ya Anwani za Makazi; na kujenga uelewa kuhusu namna ya kusimamia na kuendeleza mfumo wa anwani za makazi. Jumla ya Shilingi bilioni 50 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mawasiliano kwa Wote**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuwezesha ujenzi wa miundombini ya huduma za mawasiliano ikiwemo minara 1,353 kwenye vijiji na maeneo yasiyokuwa na mawasiliano; na kujenga kituo cha Kikanda kitakachojumuisha maghala ya kuhifadhi na kushughulikia bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha Biashara Mtandao. Jumla ya shilingi bilioni 35.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanzishwa kwa Taasisi ya TEHAMA na vituo vya Ubunifu wa TEHAMA; kuanzishwa kwa vituo vitano (5) vya kanda vya kusaidia kukuza Taaluma ya TEHAMA; kuendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Anwani ya makazi na Postikodi; utengenezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa

za Takwimu za TEHAMA (NISMIS); kuunganisha Taasisi za Serikali kwenye mtandao mmoja (GoVNET); Usimikaji wa vituo 10 vya Huduma Pamoja Centers; kujenga maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza; kuboresha uwezo na Mifumo ya Vituo vya kuhifadhia Data; utekelezaji wa Mkakati wa mawasiliano wa Tanzania ya kidijitali; Elimu kwa Umma; na Kujenga uwezo kwa wataalamu wa TEHAMA 500 Serikalini. Jumla ya shilingi bilioni 88.04 fedha za nje zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 4279: Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kujenga na kufunga miundombinu ya utangazaji ya redio na televisheni katika vituo vya TBC1, TBC2 na Tanzania Safari; ununuzi wa magari maalumu mawili (2) ya kurushia matangazo mbashara (Radio na Televisheni); ununuzi wa magari 10 kwa ajili shughuli za utangazaji; kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya TBC Jijini Dodoma pamoja na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA; na ununuzi wa mitambo na vifaa vya utangazaji wa redio, Televisheni na Mitandao ya kijamii kuunganisha studio tano (5) za Mikocheni, Zanzibar, Barabara ya Nyerere, Dodoma na Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 35.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa makala maalumu, kukusanya na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za Serikali; ununuzi wa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji na uandaaji wa taarifa vikiwemo kamera na visaidizi vyake, vifaa vya Kurushia Matangazo Mubashara; na kuanzisha Chaneli ya Televisheni ya Serikali itakayokuwa inaonesha habari za Serikali ikijumuisha shughuli zinazotekelezwa na Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri. Jumla ya shilingi bilioni 11.2 fedha za ndani zimetengwa kutekeleza shughuli hizo.

**(vii) Mradi Na. 4383: Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendeleza watalaam wa Sekta na wa nje ya Sekta kwa kutoa mafunzo ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA na matumizi ya teknolojia mpya zinazoibukia kwenye sekta nyinginezo; na kuwajengea uwezo waandishi wa Habari na wahariri wa vyombo vya Habari, kuelimisha umma juu ya teknolojia mpya za kidijitali, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi salama na yenye tija ya TEHAMA huku wakilinda haki za watoto, wanawake, makundi maalum na vijana. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(viii) Mradi Na. 6226: Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kanda vya

watengeneza bidhaa za TEHAMA; kuendelea na ujenzi wa kituo cha kuwezesha uanzishwaji wa kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam (Soft center); kuendelea na programu ya mafunzo ya kuendeleza wataalam wa TEHAMA waliosajiliwa; kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA; na kufanya tafiti za TEHAMA. Jumla ya shilingi bilioni 10.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(ix) Mradi Na. 4292: Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga kituo cha Kitaifa cha kuendeleza watalaam, tafiti na ubunifu wa TEHAMA jijini Dodoma; kuanzisha vituo atamizi vya TEHAMA katika vyuo vikuu vya umma na maeneo maalum ya kiuchumi kote nchini; na kujenga uwezo kwa wataalam 40 watakaosimamia programu za anga juu. Jumla ya shilingi bilioni 100.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha uchapachaji; kukamilisha ufungaji wa mitambo ya kisasa ya uchapaji; na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari kwa ajili ya kuongeza uzalishaji. Jumla ya shilingi bilioni 10.47 fedha za ndani zimetengwa.

**3.3.2.3. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi**

**A. Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**

**(i) Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge:**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa nyumba mbili (2) za viongozi wa Bunge (Kilimani - Dodoma), Makumbusho ya Bunge, Matenki ya kuhifadhia maji kwa ajili ya Jengo la utawala (Annex) yenye ujazo wa lita 20,000 ( Tower) na lita 50,000 (underground) na tenki la maji kwa ajili ya mfumo wa kukabiliana na majanga ya moto lenye ujazo wa lita 500,000. kazi nyingine zitakazofanyika ni ununuzi na usimikaji wa mitambo ya usalama. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Bunge**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea ukarabati wa majengo ya utawala, miundombinu katika Ofisi ndogo ya Bunge - Dar es Salaam na Ukarabati wa Server na mfumo wa sauti( DCN); ununuzi na ufungaji wa mitambo ya vipozeo (chiller na AC) kwa ajili ya kumbi za Bunge ( ukumbi wa Bunge na Msekwa); ununuzi wa viti 118 kwa ajili kumbi za Bunge; na kuendelea na ujenzi wa mfumo wa kudhibiti janga la moto kwa njia ya gesi katika maeneo maalum katika jengo la Utawala. Jumla ya shilingi bilioni 3.9 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 6216: Kulijengea Bunge Uwezo Awamu ya Pili (LSP II):**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea kuwajengea uwezo Wabunge na watumishi katika maeneo ya usimamizi wa bajeti, utungaji wa sheria na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge; na kukamilisha Mwongozo wa Utungaji wa Sheria, Muswada Binafsi wa Sheria, Usikilizaji wa Maoni ya Wadau, Ziara za Kamati za Bunge, Hoja Binafsi na Uchambuzi wa Bajeti. Jumla ya shilingi milioni 670.14 fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**
Shughuli itakayotekelezwa ni kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge na watumishi katika masuala ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, masuala ya kodi, utafiti wa masuala ya uchumi pamoja na mapitio ya sheria zinazosimamia utekelezaji wa bajeti. Jumla ya shilingi milioni 758.13 fedha za nje zimetengwa.

**B. Maboresho ya Mahakama**

**(i) Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya 18 za Kibiti, Mbulu, Simanjiro, Nkasi,Tunduru, Kahama, Kilosa, Chamwino, Rufiji, Nyasa, Mkalama, Ikungi, Momba, Serengeti, Tarime, Masasi, Ulanga, na Nachingwea; kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Kigoma; na kuanza ujenzi wa majengo mapya ya Mahakama 10 za wilaya za Serengeti, Iramba, Pangani, Nzega, Kishapu, Muleba, Siha, Tarime, Rombo na Malinyi. Jumla ya shilingi bilioni 18.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo**
Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 13 za Kinusi (Mpwapwa), Haubi (Kondoa), Magubike (Morogoro), Kitumbeine (Longido), Machame (Kilimanjaro), Ilangala (Ukerewe), Usevya (Mlele), Mbalizi (Mbeya), Maore (Same), Mahenge (Kilolo), Nanjilinji (Mtwara), Madale (Dar es Salaam) na Luilo (Ludewa). Jumla ya shilingi bilioni 4.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali Nyumba za Majaji na Mahakimu**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu; ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) kwa ajili ya makazi ya Majaji jijini Dodoma; na kuanza ujenzi wa Nyumba ya Jaji Kiongozi jijini Dodoma. Jumla ya shilingi billioni 20 za fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 6215: Mradi wa uboreshaji wa huduma za Mahakama (Citizen Centic Judiciary Modernisation Project)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Vituo Jumuishi vya utoaji

haki tisa (9) katika Mikoa ya Pwani, Manyara, Simiyu, Singida, Songwe, Geita, Lindi, Manyara na Katavi; na Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 60. Jumla ya shilingi bilioni 40 fedha za nje zimetengwa.

**C. Utawala Bora na Utawala wa Sheria**

Kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora kwa kuboresha miundombinu na uwezo wa utendaji kazi wa vyombo vinavyosimamia utawala bora na utawala wa sheria.

**(a) Mradi Na. 5501: Awamu ya Pili ya Uimarishaji wa Upatikanaji wa Haki za Kisheria na Haki za Binadamu Tanzania**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha na kuanza kutekeleza Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu; kujenga uwezo kwa Taasisi za Serikali 25 na Asasi Zisizo za Serikali 12 kuhusu uzingatiwaji wa haki na ulinzi wa haki za binadamu; kujenga uwezo kwa Mawakili wa Serikali 58 kuhusu uendeshaji wa mashauri ya Jinai; kuendelea na tafsiri ya Sheria na Miongozo ya utoaji haki kutoka Lugha ya Kingereza kuwa Lugha ya Kiswahili; na kuandaa Sera na miongozo ya Msaada wa Kisheria; kuwajengea uwezo vyombo chunguzi katika kuratibu na kusimamia uchunguzi wa makosa ya Jinai. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 5502: Kujenga Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana na Rushwa Tanzania**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Kuwalinda Mashahidi na Watoa Taarifa za uhalifu; kuandaa rufaa za viashiria vya rushwa na kuviwasilisha TAKUKURU; kukamilisha kushughulikia Mashauri 15 ya Rushwa Kubwa katika Mahakama ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; na kufanya uratibu wa upatikanaji na urejeshwaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya Uhalifu. Jumla ya shilingi bilioni 2.5 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5507: Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Watoto wa Kike.**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya maboresho Sheria za Kimila ili kuimarisha haki za wanawake na Watoto wa Kike; kujenga uwezo kwa wadau wa Haki 50 kuhusu shughuli za mahakama na ulinzi wa haki za wanawake na watoto wa kike; kujenga uwezo wa Viongozi wa Serikali za Mitaa 45, jamii 1,000 na watoa huduma ya msaada wa kisheria 38 kuhusu haki za wanawake na watoto wa kike, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia; kuandaa Sera na Miongozo ya kuzingatia katika utoaji haki za watoto wa jinsi zote; kutoa mafunzo kwa wadau wa mahakama 52 kuhusu uendeshaji wa mashauri ya jinai kwa kuzingatia usawa wa kijinsia; kuendelea kuratibu mfumo wa utekelezaji wa masuala ya uzingatiwaji na utoaji wa taarifa zinazohusu viashiria vya usawa wa kijinsia. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.1 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5508: Program ya Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuboresha maboresho ya kisera na kisheria katika kulinda, kukuza na kuhifadhi haki za binadamu na watu za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimazingira; kuboresha Sheria za Uchaguzi na Demokrasia; kufanya kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia; kuandaa mwongozo wa kuwalinda mashahidi na wahanga wa uhalifu wa jinai; kuratibu vikao vya kuandaa Sera ya Adhabu; kuandaa kutafsiri Sheria kwa Lugha ya Kiswahili kwa awamu ya pili; kujenga uwezo wa wadau kuhusu kushugulikia viashiria vya Maafa ya Kimbali; kuandaa miongozo ya Kisera ya upatikanaji haki; kuwajengea uwezo Watumuishi wa Wizara kuhusu kusimamia mfumo wa upatikanaji haki nchini; na kuandaa kituo cha kushughulia viashiria vya mauaji ya kimbali. Jumla ya shilingi bilioni 10.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6201: Haki Mtandao**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya mapitio ya Mifumo inayotumika na taasisi za haki Jinai na kuandaa mapendekezo ya kuonanisha ili iweze kusomana; kuanzisha mifumo ya kielektroniki kwa taasisi za Haki Jinai; ununuzi wa vifaa na maboresho ya Mifumo ya TEHAMA kwa Wizara na Taasisi za haki Jinai; kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na Tathmini wa Majukumu ya Wizara; kuwajengea uwezo watumishi 105 wa Wizara kuhusu mifumo iliyopo Wizarani; na kutoa elimu kwa umma kuhusu mifumo inayotumiwa na Wizara na Taasisi za haki Jinai katika utoaji wa huduma kimtandao. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 6207: Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza Wigo wa Upatikanaji wa Haki**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendesha mashauri 58 ya Jinai yanayowahusu Watoto Wanaokinzana na Sheria (pro bono services); kutoa mafunzo kwa kamati za Msaada wa Kisheria Katika Ngazi za Wilaya 85; kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria na kanuni zake; na kutoa mafunzo kwa viongozi wa kimila 32 na kidini 25 kuhusu haki za watoto, wanawake na Watu Wenye Mahitaji Maalum; na kufanya utafiti na tathmini ya hali ya Upatikanaji wa Msaada wa Kisheria na mchango wa afua za Mradi kwa miaka minne. Jumla ya shilingi bilioni 2.2 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 6517: Kuimarisha Haki za Mtoto**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza programu ya Pili ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu Tanzania; na kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Haki ya Mtoto wa mwaka 2020/21-2024/25. Jumla ya Shilingi bilioni 2.3 fedha za nje zimetengwa.

**(h) Program ya Usimamizi wa Utajiri Asilia na Maliasilia za Nchi Kijamii na Kiuchumi Tanzania**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wadau 55 kuhusu Majadiliano ya Mikataba na Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala; kuanzisha mfumo jumuishi wa uangalizi wa utajiri na maliasilia za nchi; kuanzisha kituo cha Kitaifa cha Utatuzi wa Migogoro; na kuandaa na kusambaza mwongozo wa usimamizi wa Utajiri na Maliasilia za nchi. Jumla ya Shilingi bilioni 1.8 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na usajili na utambuzi wa watu 1,063,763 katika Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar; kuzalisha na kugawa Vitambulisho vya Taifa milioni 13; kuunganisha taasisi 15 za Serikali na binafsi katika Mfumo (Kanzidata) na kuboresha huduma kwa wadau waliounganishwa katika Kanzidata; ununuzi wa kadighafi milioni tano (5) na malighafi za kuzalisha Vitambulisho vya Taifa; kuunganisha Ofisi 11 za Usajili za Wilaya na Makao Makuu na mkongo wa Taifa; kuunda mifumo (modules) 11 kwa ajili ya shughuli za usajili na utambuzi; na kufungamanisha kitambulisho cha Taifa na taarifa za mifumo mengine. Jumla ya shilingi bilioni 73.5 fedha za ndani na Shilingi bilioni 71.35 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

(i) **Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Dodoma**

Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania jijini Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 20 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Ofisi na Makazi ya Viongozi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa majengo 49 ya Halmashauri ya muda mrefu ambapo 9 kati ya hayo yamekamilika ikiwemo majengo ya utawala ya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze na Chemba; kuendelea na majengo 30 kwa Halmashauri zilizohamisha Makao Makuu ambapo jengo moja la Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika limekamilika; na kuendelea na ujenzi wa majengo mapya ya utawala 30. Aidha, kuendelea na ujenzi wa nyumba 46 za wakurugenzi na nyumba 78 za wakuu wa idara ambapo ujenzi wa nyumba hizo upo katika hatua mbalimbali. Jumla ya shilingi bilioni 78.54 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**(iii) Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Taasisi za Sheria**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa vituo 10 jumuishi vya Taasisi ya Sheria katika ngazi ya Mikoa na 20 katika ngazi ya Wilaya; na kuwajengea uwezo wataalamu 32 wa Wizara na Taasisi kuhusu mifumo ya utoaji Huduma katika vituo jumuishi. Jumla ya Shilingi bilioni 10.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mikoa mitatu (3) ya Arusha, Mtwara na Tanga. Jumla ya shilingi bilioni 10.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi ya Taifa ya mashtaka katika mikoa sita (6) ya Rukwa, Mwanza, Tanga, Dodoma, Shinyanga na Geita. Jumla ya shilingi bilioni 8.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Ujenzi wa Majengo ya Serikali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi; Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kudumu ya mawasiliano na majitaka; na kusimika kamera za ulinzi. Jumla ya shilingi bilioni 342 fedha za ndani zimetengwa.

**(vii)Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza Ujenzi wa majengo 25 ya Utawala kwenye Halmashauri zenye majengo chakavu na ya zamani; kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala 65; ununuzi wa samani kwa majengo ya utawala 42 yanayotarajiwa kukamilika; na ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi 33 na Wakuu wa Idara 116. Jumla ya shilingi bilioni 114.47 fedha za ndani zimetengwa.

**(viii) Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ofisi za wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa; Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Nyumba za wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Tarafa. Jumla ya shilingi bilioni 188.02 fedha za ndani zimetengwa.

**(ix) Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Ofisi za wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa; Ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Nyumba za wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Tarafa. Jumla ya shilingi bilioni 188.02 fedha za ndani zimetengwa.

**Usalama wa Raia**

**Mradi Na. 6302: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania Bara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa la kuishi familia za askari 12 Byakea Bukoba, Jengo la RPC Mtwara, vituo vinne (4) vya Polisi Daraja ‘B’ katika wilaya za Sikonge, Bariadi, Namtumbo na Mkuranga, Jengo la

RPC Rufiji, kituo cha Polisi Daraja C Kitangali Newala, Bweni la wanafunzi Chuo cha Marine Mwanza, Rest house Arusha, Bweni la wanafunzi Kidatu; na Kuanza ujenzi wa Jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Polisi Dodoma**,** nyumba 30 za askari Dodoma, uzio nyumba 3 za makamishna Dodoma, Rest house Tarime Rorya**;** Ofisi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia Tarime Rorya, Ofisi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia Geita, kituo cha Polisi Daraja ‘A’ Tarime, Kituo cha Polisi Daraja “B” Butiama, na nyumba ya OCD na Mkuu wa kituo Sikonge**;** na kuanza ukarabati wa nyumba 30 za kambi ya Kilwa Road. Jumla ya shilingi bilioni 13.86 fedha za ndani zimetengwa.

**Magereza**

**(a) Mradi Na. 6103: Mipango ya Ulinzi Magerezani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuweka miundombinu maalum ya usalama na upekuzi katika Magereza 10; kufunga mifumo ya kielektroniki ya kuimarisha usalama katika Magereza 15; na kuimarisha jukumu la kuwapeleka mahabusu mahakamani katika mikoa sita (6). Jumla ya shilingi bilioni 28.67 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 1201: Uimarishaji wa Viwanda vya Magereza**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha samani Msalato Dodoma; na kutolewa kwa mtaji wa uzalishaji. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6305: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa ukumbi Makao Makuu ya Magereza Msalato Dodoma na viwanja vya michezo Makao Makuu ya Magereza; kuendelea na ujenzi wa Gereza Igunga na Kwa Mturuki Bagamoyo; kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali ya Magereza Msalato Dodoma; kuanza ujenzi wa jengo la utawala Gereza Kalilankulukulu, majengo ya Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji na Chuo Kiwira na ujenzi wa magereza mapya katika wilaya za Kakonko, Kaliua, Karatu, Msalato, Kilosa, Gairo, Rorya, Mpimbwe, Sengerema, Kyerwa na Mlolo; kuanza ujenzi wa ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa ya Geita, Tanga, Songwe, Kagera na Rukwa; kuanza ujenzi wa jengo la kuhifadhia nyaraka za Serikali Makao Makuu ya Magereza na karakana Dodoma na Chuo cha Magereza Kiwira; na ununuzi wa vifaa na mitambo mbalimbali ya ujenzi. Jumla ya shilingi bilioni 25.47 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 6307: Ukamilishaji wa nyumba za watumishi wa Magereza**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa nyumba 11 za watumishi wa Makao Makuu ya Magereza, nyumba 12 za watumishi Gereza Kalilankulukulu - Mpanda na miundombinu ya majisafi na majitaka katika nyumba 39 za Makao makuu ya magereza; kuanza ujenzi wa nyumba 12 za maafisa waandamizi wa makao makuu ya magereza, nyumba za wakuu wa magereza mikoa ya Lindi na Rukwa, nyumba 12 (Gereza Kibiti (2), Chuo cha Magereza Kiwira (5) na magereza mkoa wa Mwanza (5), nyumba 12 katika Magereza ya Kibiti (2), Ngwala (2),

Matongo (2), King'ang'a (2), Kilombero (2) na Lushoto (2)); na ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Magereza Pwani, Gereza Kingolwira, Chuo cha Kiwira na Mtego wa Simba - Morogoro. Jumla ya shilingi bilioni 4.45 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6308: Ukarabati wa Magereza Makuu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukarabati mabweni ya Gereza Ukonga, Ushora, Bukoba, Mafia, Kitete, Segerea, Kingolwira, Isanga, Maweni, Mkuza, Lindi na Kondoa; na kukarabati miundombinu ya majisafi na majitaka katika Gereza Mbozi, Mpanda na Songwe. Jumla ya shilingi bilioni 1.98 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4428: Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba matano (5) ya Magereza ya Ushora, Kitete, Kalilankulukulu, Ilagala na Kilindi; kuanza ujenzi wa miundombinu ya ufugaji Gereza Ubena na Mugumu; kuanza ujenzi wa karakana nane (8), ghala nane (8) na ununuzi wa zana na mitambo; na kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za alizeti, mpunga, mbaazi, mahindi na ufuta katika magereza ya Ushora, Babati, Wami Kuu, Nachingwea, Ilagala na Kalilankulukulu. Jumla ya shilingi bilioni 16.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 2330: Upimaji wa Maeneo na Ulipaji Fidia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kupima na kutathmini wa ardhi katika Magereza 14 na Kambi 47; na Kulipa fidia ya maeneo manne (4) katika Wilaya za Misungwi - Mwanza, Kaliua – Tabora, Kilolo - Iringa na chamwino - Dodoma na viwanja viwili (2) magereza ya katika Mikoa ya Songwe na Ruvuma. jumla ya shilingi bilioni 2.40 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4491: Kuboresha upatikanaji wa Maji safi magerezani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuchimba visima 20 vya maji katika magereza 20; na kujenga karakana ya vifaa na mitambo ya ujenzi. Jumla ya shilingi bilioni 1.18 fedha za ndani zimetengwa.

**Huduma za Zimamoto na Uokoaji**

**(i) Mradi Na. 6582: Upanuzi wa Huduma za Zimamoto**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua magari (10) ya Kuzima moto na Maokozi nchini kwa ajili ya mikoa ya Simiyu, Manyara, Njombe, Songwe, Katavi,Geita, Kagera, Mara, Kilimanjaro na Mbeya; Magari mawili (2) ya kubeba wagonjwa kwa ajili ya mikoa ya Dodoma na Morogoro; Kujenga vituo (8) vya zimamoto na uokoaji katika mikoa ya Kigoma, Mbeya, Shinyanga, Singida, Rukwa, Iringa, Tabora, na Rukwa, nyumba mbili (2) za walimu na madarasa mawili (2) katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji Tanga; kujenga nyumba (15) na kukarabati nyumba 10 kwa ajili ya makazi ya Maafisa na Askari; na Kununua boti tano (5) za uokoaji, vifaa na mavazi maalum ya kuzima moto na Uokoaji. Jumla ya shilingi bilioni 43 (32)

fedha za ndani zimetengwa.

**Uhamiaji**

**Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Simiyu, Songwe, Katavi na Njombe, Ofisi za uhamiaji katika Wilaya za Simanjiro, Rorya, Mufindi na Kyerwa na ujenzi wa Ofisi za uhamiaji katika Vituo vya Mipakani vya Murusagamba na Kirongwe; kuanza ujenzi wa nyumba 2,304 za Maafisa, Wakaguzi na Askari wa Uhamiaji; kuanza ukarabati wa Ofisi za uhamiaji mikoa ya Kagera, Kilimanjaro na Morogoro, Ofisi ya wilaya Kahama na nyumba za makazi Tabora; na ununuzi wa mitambo katika kiwanda cha uchapaji nyaraka kijichi Dar es Salaam (KPU), Mtambo wa kuchapa Pasipoti Katika Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Dodoma na ununuzi wa magari 70, Pikipiki 125 na boti 3 kwaajili ya kuimarisha shughuli za misako na doria ya wahamiaji haramu. Jumla ya Shilingi bilioni 234.87 (217.5) fedha za ndani zimetengwa.

**D. Utumishi wa Umma**

**(i) Mradi Na. 6284: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuwezesha Taasisi za Umma 539 kutekeleza Mifumo ya Usimamizi wa Utendaji Kazi ya PEPMIS na PIPMIS; kuendelea na maboresho ya mifumo ya HR Assessment na e-HRP; kununua vitendea kazi (ikiwemo magari ya Viongozi Wakuu Wastaafu na kopyuta); kuanza kwa ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Mbeya; na kuendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya huduma za Serikali mtandao (e-Governance services). Jumla ya shilingi bilioni 1.565 fedha za ndani zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wastaafu wa Kitaifa (kukamilisha nyumba ya Rais wa Awamu ya Tano na kuanza nyumba ya Rais wa Awamu ya Sita); na kuendelea na ujenzi wa Klabu ya Viongozi. Jumla ya shilingi bilioni 6.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 6282: Mfumo Mpya wa Kielektroniki wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara - Home Grown HCMIS**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa mfumo na kuwajengea uwezo watumiaji; na kuongeza uwezo wa mfumo wa HCMIS kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya Serikali. Jumla ya shilingi milioni 600 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

#### 3.3.3.1. Uzalishaji Viwandani

**(a) Mradi Na. 1214: Kuendeleza Programu ya Maendeleo ya Viwanda - PCP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuratibu utekelezaji wa programu ya PCP chini ya UNIDO; kuwezesha uanzishaji wa mfuko wa pamoja (Backet fund) kwa ajili ya maendeleo ya viwanda; kuwezesha ukamilishaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda (SIDP); na kufanya tathmini ya kisekta ya mnyororo wa thamani kwa ajili ya ushindani wa viwanda katika chuma na bidhaa za chuma, soap na detergent. Jumla ya shilingi bilioni 2.13 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6103: Kuboresha Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania - TATC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ununuzi wa mashine na mitambo pamoja na kukarabati mashine, mitambo na majengo kwa ajili ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia; kuanzisha Karakana Kuu ya Kukalibu Chuma (Heavy Duty Foundry); kuanzisha kiwanda cha kuunda magari (Nyumbu Brand) na magari ya kuzima moto (Fire Fighting Vehicles) chenye uwezo wa kuunda magari sita (6) hadi kumi (10) kwa mwaka; kuendeleza wataalamu 37 katika fani za uhandisi wa magari na mitambo, mipango, ufundi stadi, masoko, TEHAMA, na ugavi; na kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia wa zana na vifaa mbalimbali, magari na mitambo. Jumla ya shilingi bilioni 25.37 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4486: Uzalishaji Viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya utafiti wa kina katika Sekta Ndogo za Pamba, Mafuta, Kahawa, Sukari, Korosho, vinywaji na Vifungashio; kubainisha na kufanya tathmini ya miundombinu ya masoko iliyopo nchini na matumizi yake; kuandaa kanzi data ya biashara za ndani, kikanda na biashara za kimataifa; na kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Masoko ya mazao, mifugo, samaki na bidhaa nyingine. Jumla ya shilingi bilioni 1.08 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4948: Kuendelea Kueneza Dhana ya KAIZEN Nchini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kueneza falsafa ya Kaizen kwenye mikoa saba (7) ambayo bado haijapata mafunzo; kuandaa mashindano ya Kaizen kuanzia kwenye mikoa hadi kimataifa kwa wenye viwanda; kushiriki kwenye mafunzo ya Kaizen ndani na nje ya nchi; kushiriki kwenye Maonesho mbalimbali kwa lengo la kueneza falsafa ya Kaizen kwa jamii; kutoa mafunzo kwa vitendo ya dhana ya Kaizen kwenye viwanda; na kuendelea kuvisimamia viwanda ambavyo vimeshapata mafunzo ya Kaizen ili kuendelea kutekeleza dhana hiyo. Jumla ya shilingi milioni 400.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6260: Miradi ya Kusaidia Taasisi**

**(i) Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua na kufanya ukarabati wa mashine; kufanya uzalishaji wa mashine na vipuri; na kufanya Ukarabati wa majengo matano (5). Jumla ya shilingi bilioni 2.60 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO – Eneo la viwanda**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kujenga km 2.8 za barabara; kujenga *Oxidation pond*; kujenga jengo la Kiwanda (Industrial shed). Jumla ya shilingi bilioni 12.07 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Eneo la Kongani ya Viwanda - Nyanza (Mwanza)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya ukarabati wa majengo ya *Nyanza Glass* ili kuvutia uwekezaji wa viwanda. Jumla ya shilingi milioni 200.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi wa Makaa ya Mawe Katewaka**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya majadiliano na mwekezaji na kusaini mkataba wa ubia (JV Agreement); na kulipa leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi milioni 320.69 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi wa Maganga Matitu *Sponge Iron***

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha majadiliano na mwekezaji na kusaini mkataba wa ubia (JV Agreement); na kulipa leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi milioni 238.41 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Mradi wa Makaa ya Mawe Mhukuru**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya utafiti wa kina wa kijiolojia (geological study); na kulipa leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi bilioni 1.17 fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Mradi wa Kiwanda cha Viuadudu (TBPL)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya ithibati ya bidhaa za viuadudu na Kiwanda (Pre-qualification); kufanya stadi ya uzalishaji wa mbolea za kibailojia (biofertilizer), na masoko ya viwatilifu vya kibailojia (biopesticides); kuandaa mpango biashara na kusaini mkataba wa manunuzi wa dawa za viuadudu (offtake agreement). Jumla ya shilingi bilioni 1.89 fedha za ndani zimetengwa.

**(viii) Kiwanda cha Mang'ula**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya Ukarabati wa majengo. Jumla ya shilingi milioni 456.49 fedha za ndani zimetengwa.

**(ix) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini - CAMARTEC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa mashine na mitambo ya Karakana na upanunuzi wa karakana iliyoko Makao Makuu (Arusha) na katika Tawi la Nzega

(Tabora); Ujenzi wa ghala na nyumba ya mtumishi na ununuzi wa mtambo wa kupaki korosho katika kiwanda darasa cha kubangua korosho kilichopo wilaya ya Manyoni; na kutengeneza mashine za kubangua korosho zitakazopelekwa wilayani Mtwara kwa lengo la kuongeza thamani katika zao la korosho. Jumla ya shilingi bilioni 2.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa maabara ya ngozi; kukamilisha ujenzi wa Jengo la Utawala ili kutoa nafasi ya kuanzisha Kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashari wa Teknolojia na Viatamizi kwa wabunifu wa teknolojia; na kuendelea kufanya tafiti mbalimbali kama za mazao ya kilimo na mimea ili kuongeza thamani. Jumla ya shilingi bilioni 6.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(xi) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kubuni na kuendeleza mtambo mkubwa wa kuchakata mkonge; kubuni na kuendeleza teknolojia ya kutengeneza matofali ya kuzuia joto kali (refractory bricks) kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa; kuendeleza na kuhawilisha teknolojia ya mtambo mdogo wa kuchakata miwa na kutengeneza sukari (sugar processing mini-plant); Kuboresha Karakana kwa kusimika mashine na vifaa vya kisasa (Heavy duty 6-axes CNC Machines). Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(xii) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo - SIDO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kujenga Majengo ya Viwanda katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Simiyu, Dodoma na Morogoro; kujenga Ofisi tatu za kutolea huduma katika mikoa ya Songwe, Dodoma na Mbeya; na kuimarisha miundombinu ya viwanda kwa kukarabati majengo, barabara, Mifumo ya maji, kujenga uzio katika Mitaa ya Viwanda ya mikoa ya Arusha, Mbeya, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Iringa, Mtwara, Mwanza na Ruvuma. Jumla ya shilingi bilioni 3.27 fedha za ndani zimetengwa.

**(xiii) Kuendeleza Biashara Kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la ghorofa kumi (10) la Vipimo na Viwango katika Kampasi ya Dar es Salaam; Ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa katika Kampasi ya Dodoma; na Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi wa kike na *Cafeteria* katika Kampasi ya Mbeya. Jumla ya shilingi bilioni 3.21 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4933: Uendelezaji wa Kanda Maalumu za Kiuchumi**

(i) **Eneo Maalum la Uwekezaji Tanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha malipo ya fidia, kupima na kuweka mipaka kwa ajili ya umilikishwaji; kufanya upembuzi yakinifu; kuandaa mpango

kabambe wa uendelezaji katika eneo lililolipiwa fidia la Tanga SEZ. Jumla ya shilingi milioni 750 fedha za ndani zimetengwa.

(ii) **Eneo la Maalum la Uwekezaji Kigoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya usanifu wa miundombinu, kuanza ujenzi wa miundombinu ya msingi; na kuendelea na programu za uhamasishaji wa kuvutia wawekezaji.

(iii) **Eneo Maalum la Uwekezaji Kahama**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupata hati miliki na kukamilisha ulipwaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi; kuanza maandalizi ya Upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe (Master Plan); kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira (SEA), usanifu wa miundombinu na kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi.

(iv) **Eneo Maalum la Uwekezaji Bunda**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa upembuzi yakinifu. Jumla ya shilingi milioni 100 fedha za ndani zimetengwa.

(v) **Eneo Maalum la Uwekezaji Songwe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na taratibu za kupata hati miliki; kuanza maandalizi ya Upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe (Master plan); na kufanya Tathmini ya kimkakati ya mazingira (SEA) na Usanifu wa Kina wa miundombinu wezeshi.

(vi) **Eneo Maalum la Uwekezaji Manyara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya Usanifu wa Kina wa miundombinu ya wezeshi.

(vii) **Eneo Maalum la Uwekezaji Mtwara Free Port Zone**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ili kuhamasisha uwekezaji katika eneo la Bandari huru (Free Port Zone) hususani kwa makampuni ya Mafuta na Gesi.

### 3.3.3.2. Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**A. Kilimo**

**(a) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II**

**(i) Kuimarisha miundombinu ya utafiti na kufanya tafiti zitakazozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo;**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji kwa vituo 17 vya utafiti vyenye jumla ya hekta 854 kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa mbegu; kusafisha na kuzalisha tani 250 za mbegu za asili na mbegu bora; kuwezesha vituo

6 vya utafiti vya TARI Ilonga, TARI Uyole, TARI Tumbi, TARI Naliendele, TARI Makutupora, na TARI Hombolo kuzalisha tani 450 za alizeti; ujenzi wa ofisi ya TARI Makao Makuu; ujenzi wa ofisi na nyumba nne (4) za watumishi kituo cha utafiti TARI Kihinga – Kigoma; kuimarisha maabara ya udongo ya TARI Mlingano, maabara za *tissue culture* na bayoteknolojia ya TARI Mikocheni; na Kujenga na kukarabati maghala Matano (5) ya mbegu. Jumla ya shilingi bilioni 40.73 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo kupitia mpango wa ruzuku (mbegu, mbolea, viuatilifu) na zana za kilimo**

**Upatikanaji wa mbegu bora**

ikiwemo Alizeti (tani 5,000), Ngano (tani 600), Soya (tani 400) na ukuzaji wa miche ya michikichi 500,000; miche ya parachichi 450,000; kujenga miundombinu ya umwagiliaji (Centre Pivot) kwenye hekta 1,020 kwenye mashamba 10 ya Kilimi (hekta 100), Msimba (hekta 100), Bugaga (hekta 100), Mbozi (hekta 100), Tengeru (hekta 20), Dabaga (hekta 100), Namtumbo (hekta 400) na Mwele (hekta 100); kuchimba visima 5 na kusimika miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu ya Bugaga (hekta 100), Mazizi (hekta 4.8) na Msungura (hekta 100); kununua matrekta sita (6), planta mbili (2) za kupandia mpunga na ndege mbili (2) zisizo na rubani zenye uwezo wa kubeba lita 20 za viuatilifu kwa ajili ya kunyunyuzia viuatilifu; kufungua maeneo mapya kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora katika mashamba ya Mwele (hekta 200) na Luhafwe (hekta 700); kujenga maghala matatu (3) ya kuhifadhi mbegu katika mikoa ya Ruvuma, Pwani na Katavi; kuendelea na ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya umwagiliaji yenye ujazo wa mita 45,000 katika shamba la mbegu la Mbozi, Namtumbo na Dabaga; ununuzi wa mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu kwa ajili ya mashamba ya mbegu Mbozi na Namtumbo; na kujenga bwawa lenye mita za ujazo 82,000. Jumla ya shilingi Bilioni 59.98 fedha za ndani zimetengwa. Jumla ya shilingi blioni 43.03 fedha za ndani zimetengwa.

**Upatikanaji wa mbolea**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea nchini kwa kutoa ruzuku ya mbolea tani 450,000 na kuimarisha mfumo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima nchini; Kuiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kununua na kusambaza tani 30,000 za mbolea na ardhi ya kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea; kukagua na kuthibiti ubora wa mbolea kwa wafanyabiashara na itatoa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea; na kusajili aina mpya za mbolea na visaidizi vyake 85 na kutoa leseni 2,100. Jumla ya shilingi Bilioni 165 fedha ndani zimetengwa.

**Upatikanaji wa Viuatilifu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa viuatilifu lita 118,500 vya kudhibiti visumbufu vya milipuko (lita 100,000 za kudhibiti viwavijeshi, lita 10,000 kwelea kwelea, lita 5,000 nzige, lita 3,000 nzi wa matunda na lita 500 panya); ujenzi na

ukarabati wa miundombinu ya maabara za uchambuzi wa viuatilifu na Afya ya Mimea katika ofisi za TPHPA- Arusha na Dar es salaam; ununuzi wa mashine za kisasa aina ya GC –MSMS, HPLC, HPLC – MSMS; Kukamilisha ununuzi wa ndege kwa ajili ya kuimarisha huduma za KILIMO ANGA; Kudhibiti ubora wa viuatilifu vinavyozalishwa nchini na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi; na kutoa mafunzo ya matumizi bora na sahihi ya viuatilifu. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kukamilisha Ujenzi wa Skimu 25 na ukarabati wa Skimu 30 zenye jumla ya hekta 95,005; Kukamilisha ujenzi wa Mabwawa 14 yenye mita za ujazo 131,535,000; Kujenga Skimu mpya 28 zenye ukubwa ya hekta 65,705 na ukarabati wa Skimu 70 zenye ukubwa hekta 85,500; Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Mabonde 22 ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 306,361; Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya pamoja (Block farms) 6 yenye jumla ya hekta 49,517.86 chini ya programu ya BBT; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu sita (6); kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu 42 zenye jumla ya hekta 91,357; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde ya kimkakati 19 yenye jumla ya hekta 283,461. Jumla ya shilingi bilioni 281 fedha za ndani zimetengwa..

**(iv) Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo**

**Kuimarisha Vyuo vya Mafunzo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukarabati na kujenga miundombinu ya MATI Uyole, KATRIN, MATI -Inyala, MATI - Ukiriguru, MATI - Igurusi, MATI - Mtwara, MATI - Mlingano, HORTI Tengeru na FTC (Bihawana Mkindo, Themi & Ichenga); na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mafunzo kwa Vyuo vya MATI Mlingano, HORTI Tengeru, MATI - Inyala, MATI - Maruku, MATI - Mubondo, MATI - Mtwara na FTC (Bihawana). Jumla ya shilingi bilioni 5.17 fedha za ndani zimetengwa.

**Huduma za ugani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ununuzi wa pikipiki 600; ununuzi wa magari 26 kwa Maafisa Kilimo, Sekretarieti za Mikoa; ununuzi wa vifaa vya kupima afya ya udongo *(Mobilie soil testing kit)* kwa ajili ya Halmashauri 45; kujenga na kukarabati vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) katika mikoa mitano (5); kuanzisha mashamba ya mfano 100 na mashamba darasa 56 katika Halmashauri 25 kwenye Mikoa ya Njombe, Rukwa, Kigoma, Songwe na Iringa; kuendelea kuimarisha matumizi ya Kituo cha Huduma kwa Wateja na Mfumo wa M-Kilimo; Kutoa mafunzo ya teknolojia iliyoboreshwa kuzingatia eneo la kilimo-ikolojia kwa Maafisa Ugani 1,200 kutoka mikoa 12; kutoa mafunzo ya matumizi ya huduma za kielektroniki (M-kilimo) kwa maafisa kilimo 600 katika mikoa mitano (5) (Pwani, Arusha, Mororgoro,

Ruvuma na Katavi) na maafisa ugani 3000 kutoka sekta binafsi; Jumla ya shilingi Bilioni 5.65 fedha za ndani zimetengwa.

**Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao ya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula na lishe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga ghala 100 zenye uwezo wa kuhifadhi kati ya tani 500 hadi 1,000 za mazao ya nafaka kila moja pamoja na kuweka vifaa vya pallets, vifaa vya zima moto, vipima unyevu na mizani katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Mbeya, Geita, Singida, Dodoma na Tabora; kukamilisha ujenzi na ukarabati wa ghala 38 katika Mikoa ya Ruvuma, Tabora, Shinyanga na Geita; kukamilisha ukarabati wa ghala 29 za kuhifadhi chakula katika Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga (13), Songea (8), Madaba (8); Kujenga visima vinne (4) katika ghala za Mbogokomtonga (1), Kigugu (1), Msolwa Ujamaa (1) na Njage (1) mkoani Morogoro; na kufanya tathimini ya hali ya upotevu wa mazao ya chakula katika mikoa 15 (Halmashauri 60) kwa lengo la kuwezesha kufanya maamuzi sahihi kuhusu kuimarisha usalama wa chakula nchini. Jumla ya shilingi bilioni 4.76 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Kuhamasisha na kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa (block farming) na kushirikisha vijana katika kilimo na kuimarisha upimaji wa afya ya udongo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni; Kutambua na kuweka mipaka ya mashamba mapya 30 yenye ukubwa wa hekta 200,000 kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo na vijana kupitia Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Njombe, Songwe na Tanga; kuwezesha upatikanaji wa fidia kwa ardhi ya kilimo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo katika mikoa tisa (9) (Singida, Manyara, Tabora, Pwani, Lindi, Mtwara, Rukwa, Ruvuma na Kigoma); kupima afya ya udongo katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji, kupima afya ya udongo katika maeneo ya umwagiliaji yaliyoathiriwa na tindikali na chumvi katika Mikoa ya Manyara, Morogoro, Pwani, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Arusha; na kuendeleza matumizi ya teknolojia za kurudisha na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika mashamba na mabonde yanayozunguka skimu 10 za umwagiliaji katika Mikoa ya Tabora, Pwani, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Singida. Jumla ya shilingi Bilioni 14.28 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga vituo viwili (2) jumuishi cha ukusanyaji, ufungishaji na uhifadhi wa mazao ya bustani katika Mikoa ya Iringa na Kilimanjaro; kujenga kiwanda kidogo kimoja (1) na kusimika mtambo wa kusindika zao la zabibu katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma; kukamilisha ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati yaliyokuwa chini ya mradi wa DASIP katika mikoa ya Shinyanga, Mara na Kagera; na ujenzi wa miundombinu wa masoko (market sheds) nane (8) katika

mikoa ya Kagera, Arusha, Tanga, Tabora, Lindi na Dodoma; Kuimarisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa uhifadhi na biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko; Kununua tani 113,435 za mazao ya mahindi, mpunga, alizeti na mtama mweupe kupitia CPB kwa ajili ya biashara; Kununua na kuhifadhi tani 100,000 za mahindi na mpunga kupitia NFRA; na Kuendelea kutoa taarifa za uzalishaji wa mazao ya chakula na upatikanaji wake sambamba na kubaini maeneo yenye upungufu wa chakula kwa lengo la kuchukua hatua stahiki. Jumla ya Shilingi bilioni 30 za fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Kuimarisha ushirika**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 238 kwa ajili ya kupewa mbinu za kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa Vyama vya Ushirika; uanzishwaji na usajili wa vyama vya ushirika 39 katika vikundi vidogo vya wakulima wa mazao ya mboga na matunda; uanzishwaji wa viwanda vidogo 25 na vikubwa 3 vya uongezaji thamani wa mazao yanayozalishwa na wanachama wa vyama vya ushirika; kuunganisha vyama 400 vya ushirika na masoko ya ndani na nje ya nchi; uanzishwaji wa mitaala ya ushirika katika Taasisi za elimu; na kuanzisha madawati ya Ushirika katika Wizara za kisekta. Jumla ya shilingi bilioni 5.79 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4499 Kudhibiti Sumukuvu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Kibaiolojia – Kibaha na Kituo Mahili Baada Mavuno (Post Harvest Centre of Excellence) Kongwa - Dodoma; Kukamilisha ujenzi wa ghala 14 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,500 katika Wilaya za Gairo, Chemba, Kiteto, Babati, Itilima, Buchosa, Bukombe, Kibondo, Kasulu, Nzega, Namtumbo, Nanyumbu, Unguja na Pemba; kuendelea na ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo; na kutoa mafunzo kuhusu uzalishaji na hifadhi bora wa mazao ya mahindi na karanga kwa viongozi, waandishi wa habari, wakulima na wasafirishaji wa mazao. Jumla ya shilingi milioni 500.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 29.05 fedha za nje zimetengwa

**(c) Mradi Na. 4497 Kuongeza Uhifadhi wa Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa vihenge 36 vya kisasa na ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 501,000 katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 48.72 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4427 Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 198 za mashamba ya Msimba na Kilimi; ujenzi wa ghala 1 la kuhifadhia mbegu, ofisi, jengo la kufundishia wakulima na nyumba 4 za watumishi katika shamba la Kilimi; ukarabati wa nyumba (5) za watumishi na karakana 1 katika shamba la

Msimba; ukarabati na ununuzi wa vifaa vya maabara ya mbegu Arusha; kutoa mafunzo kwa wakaguzi 50 wa mbegu katika ngazi ya wilaya; kuimarisha matumizi ya lebo za kielektroniki na ukaguzi ili kudhibiti uuzaji wa mbegu feki. Jumla ya shilingi bilioni 18 fedha za nje zimetengwa.

**B. Mifugo**

**(a) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

**(i) Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhimilisha ng'ombe 370,000; kuimarisha mashamba matano (5) ya kuzalisha mitamba kwa kuyapatia vitendea kazi (trekta 2 na magari 2, ng'ombe wazazi 500) na kuendeleza malisho; na kununua na kusambaza madume bora ya mbegu 400. Jumla ya shilingi bilioni 10.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga na kukarabati malambo 27; kuchimba visima virefu 10 kwenye maeneo yenye ukame; kuongeza uzalishaji wa mbegu katika mashamba mawili (2) ya Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya); na kuanzisha mashamba darasa ya malisho 150 ili kujenga uelewa wa wafugaji kuhusu kilimo cha malisho na aina ya malisho kulingana na ikolojia ya eneo husika. Jumla ya shilingi bilioni 5.48 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Kuimarisha Afya ya Mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga majosho 400; kununua dawa za kuogeshea mifugo lita 52,560; kuzalisha na kusambaza chanjo 7 za magonjwa ya mifugo; na kuendelea na utafiti wa uzalishaji wa chanjo mpya ikiwemo Chanjo ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo. Jumla ya shilingi bilioni 12 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Kuboresha Huduma za Ugani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua pikipiki 2,000 kwa ajili ya maafisa ugani; kununua magari 50 kwa ajili ya kutoa huduma za ugani; kununua vifaa vya uhimilishaji katika Halmashauri 184; kuanzisha mashamba darasa 330 ya ufugaji; kuanzisha vituo 18 atamizi vya vijana; na kutolewa kwa mafunzo rejea kwa maafisa ugani 1,000 na wafugaji 150,000. Jumla ya shilingi bilioni 40.01 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Kuimarisha Huduma za Utafiti na Mafunzo ya Taaluma za Mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya utafiti wa uboreshaji wa mbari za mifugo na malisho ili kuongeza uzalishaji na tija (TALIRI); kujenga na kukarabati miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika vyuo nane (8) vya LITA; na kujenga Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni

11.4 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Kuwezesha Uongezaji Thamani Mazao ya Mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuwezesha unenepeshaji wa ng'ombe, kondoo na ufugaji bora wa mbuzi kupitia vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana 5,000; kujenga minada 38 ya mifugo (24 ya awali, 8 ya upili na 6 ya mipakani) na kuweka vitendea kazi ikiwemo mizani 50; kuendelea na ukarabati wa machinjio ya Serikali ya Dodoma; kujenga machinjio moja (1) ya Nguruwe mkoani Njombe na machinjio moja (1) ya kuku Jijini Dar es Salaam; na kukarabati vituo vya kupumzisha mifugo na karantini ili kuwezesha biashara ya mifugo hai ndani na nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 13.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Kuimarisha Kampuni za Ranchi za Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kujenga miundombinu ya uzalishaji katika ranchi za Kongwa na Ruvu; kuanzisha skimu za uwekezaji za vijana katika ranchi za NARCO na maeneo ya kupumzishia mifugo. Jumla ya shilingi bilioni 550.8 fedha za ndani zimetengwa.

**C. Uvuvi**

**(b) Mradi Na. 4703: Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi; ukarabati wa jengo la zamani la utawala la Ras Mkwavi (Kigamboni - Dar es Salaam), jengo la Mtambo wa Barafu Ras Mkwavi, Ghala la Mwananchi Ocean Product – Kurasini na Ghala la Chang'ombe – Temeke; ukarabati wa Gati la kuegeshea meli; kujenga na kuendesha mtambo wa kuzalisha barafu na ghala la ubaridi la kuhifadhia mazao ya Uvuvi eneo la Ras - Mkwavi. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 fedha za nje na shilingi bilioni 4.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II)**

**(i) Kujenga na Kuimarisha Miundombinu ya Uvuvi (Mialo na Masoko)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa masoko saba (7) ya Samaki katika maeneo ya Tunduma, Kyamkwikwi, Masuche, Manda, Nyamikoma, Zingibari na Kasanga; kuendelea na ujenzi wa mialo saba (7) ya Igabiro, Chifunfu, Igombe, Kayenze, Chato Beach, Karungu na Ng'ombo. Jumla ya shilingi bilioni 1.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa Vituo viwili (2) vya Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Sota (Simiyu) na Nyakaliro (Sengerema); na ukarabati wa kituo cha Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Bukoba. Jumla ya shilingi milioni 860 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Kujenga na Kukarabati Miundombinu ya Ukuzaji Viumbe Maji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa mabwawa, mfumo wa maji na kuchimba visima viwili (2) vya maji katika kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Kingolwira (Morogoro); kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kituo cha Ruhila (Songea); kuendelea na ujenzi wa kitotoleshi pamoja na ukarabati na upanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Nyengedi (Lindi); na kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha vyakula vya samaki. Jumla shilingi bilioni 1.2 fedha za ndani na shilingi milioni 106 fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa Kampasi mpya ya FETA Zanzibar; kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2) katika Kampasi ya Nyegezi (Mwanza); kuendelea na ujenzi wa Maabara katika Kampasi ya Gabimori (Mara); kuendelea na ujenzi wa Maabara ya Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (*Mariculture Laboratory*) katika Kampasi mpya ya Mikindani (Mtwara); na ununuzi wa vifaa vya maabara katika kampasi za Mikindani na Gabimori. Jumla shilingi milioni 990 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utafiti wa wingi na mtawanyiko wa Samaki katika Bahari ya Hindi (EEZ); kuendelea na utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika; kubainisha maeneo yenye rasilimali za uvuvi hususan mazalia ya samaki katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa kutumia satelaiti; na Kuangalia uwepo wa gesi za nitrojeni na phosphorasi kwenye maeneo yanayozunguka bonde la Ziwa Victoria kwa ajili ya kufahamu athari za mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 fedha za ndani na shilingi milioni 388.2 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Programu 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni**:** Kuendelea na ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi (Pangani); kukamilisha utambuzi wa maeneo ya kuweka vifaa vya kuvutia samaki (Fish Aggregate Device – FADs) katika pwani ya bahari ya Hindi na ununuzi wa vifaa hivyo; kukamilisha tathmini ya athari za kimazingira na kijamii pamoja na kujenga vichanja 10 vya kuanikia dagaa katika maeneo ya (Pangani, Bagamoyo, Kilwa na Mafia) na vibanda vinne (4) vya kukaushia mazao ya uvuvi (Pangani, Kilwa na Lindi) kwa kutumia Sola; uendelezaji wa Programu ya Vituo Atamizi vya Ukuzaji Viumbe Maji kwa kujenga vizimba 40, kitotoleshi kimoja (1), mtambo mmoja (1) wa kutengeneza chakula cha samaki; na kufunga mitambo minne (4) ya umeme ya kukaushia dagaa katika mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara na Geita. Jumla ya shilingi bilioni 5.1 fedha za nje zimetengwa.

Serikali inatekeleza Mradi wa Nufaika na Ukuzaji Viumbe maji ambapo imekamilisha kuainisha wanufaika wa mikopo ya Pembejeo za ufugaji samaki kwenye vizimba na kilimo cha mwani kupitia mradi wa ECF/IMF. Aidha, Serikali imeingia mkataba na wazabuni sita **(6)** kwa ajili ya kusambaza pembejeo na zana zenye thamani ya shilingi bilioni 14.08 zitakazotolewa kama mikopo ya masharti nafuu isiyo na riba kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa wafugaji samaki **3,154** na wakulima wa mwani **2,030.** Mradi huu utachangia katika kufikia lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki wa kufuga kwa mwaka kutoka tani **25,000** hadi tani **50,000,** na mwani kutoka tani **3,500** hadi tani **10,000** kwa mwaka ifikapo mwaka 2025/2026. Kwa upande wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba**, S**erikali imebainisha jumla ya wanufaika **3,154** wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba kati ya hao **91** ni wa vyama vya ushirika na vikundi, makampuni **10** na watu binafsi **32**. Wanufaika hao wanatoka katika halmashauri **19** zinazozunguka ziwa Victoria. Vilevile, hadi kufikia Januari, 2023 vizimba katika Ziwa Victoria vimeongezeka hadi **911** kutoka **653** mwaka 2021/2022

### 3.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia

(i) **Mradi Na. 1119: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (Sustainable Management of Mineral Resources Project- SMMRP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa Jengo la ofisi ya makao makuu ya Tume ya Madini - Dodoma; kuimarisha miundombinu ya TEHAMA Mirerani; kuanza kwa ujenzi wa ofisi ya afisa madini mkazi Geita; kuimarisha kanzidata ya miamba; ununuzi wa vifaa vya utafiti wa jiosayansi na vifaa vya maabara na uchunguzi kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); kuendelea na ujenzi wa ofisi na maabara ya *GST* katika Wilaya ya Chunya (Mbeya) kwa lengo la kusogeza huduma za taasisi karibu na wadau.

Shughuli zingine ni: Ununuzi wa mashine tano (5) za uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo; ununuzi wa mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala *(Coal Briquette)* kwa ajili ya matumizi ya nishati rafiki ya kupikia; ununuzi wa mtambo wa kuchenjulia madini ya *limestone* katika kituo kipya cha Mfano cha wachimbaji wadogo mkoani Tanga. Jumla ya shilingi bilioni 15.0 fedha za ndani zimetengwa.

(ii) **Mradi Na. 1120: Kituo cha Jemolojia Tanzania (Tanzania Geomological Centre -TGC)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya Kituo cha Jimolojia Tanzania; kujenga uwezo kwa wataalamu nane (8) wa Kituo cha Jimolojia Tanzania katika shughuli za uongezaji thamani madini; ununuzi wa vifaa vya kufundishia, mashine na mitambo ya kuchakata madini; ununuzi wa vifaa vya maabara; na uwekaji wa samani na vifaa kwenye madarasa na mabweni ya wanafunzi. Jumla ya shilingi bilioni 7.0 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.3.4. Huduma

#### 3.3.3.4.1. Maliasili na Utalii

(i) **Mradi Na. 5203: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuchimba makingio ya maji (weir) manne (4) katika maeneo ya Ngiriama, Telekimboga, Nyamakuyu B na Nyamakuyu C na visima virefu vitatu (3) katika maeneo ya Mbagi, Breakfast Point na Mdonya Falls; na kujenga mabwawa manne (4) katika maeneo ya Ikowoka, Igohuninga, Ilalangulu na Ngalambula kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha; kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za umwagiliaji za Chosi, Herman, Gonakuvagogolo na Matebete katika bonde dogo la Mto Chimala; kupanda miti 30,000 ili kutunza mabonde ya maji Kanda ya Kusini; ujenzi wa majengo ya watumishi (8), malango matatu (3) ya kuingia hifadhini, nyumba za kulala wageni (23), vituo (8) vya watalii na utalii katika hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Nyerere, Udzungwa na Msitu wa Asili wa Kilombero; kufanya tafiti mbalimbali zenye lengo la kuhifadhi maliasili na kuendeleza utalii katika Hifadhi za Taifa Ruaha na Nyerere. Jumla ya shilingi milioni 250.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 125.7 fedha za nje zimetengwa.

(ii) **Mradi Na. 4812: Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ununuzi wa vifaa vya doria na kufanyika kwa doria; kuandaa kanzidata kwa ajili ya kutunza taarifa na kumbukumbu mbalimbali za ujangili na biashara haramu ya nyara; kununua samani kwa ajili ya chumba maalum cha kuratibu kazi za kudhibiti ujangili “central operations and control room” Wizarani; kuandaa kanuni za “compounding”. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za nje zimetengwa.

(iii) **Mradi Na. 4651: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki – BEVAC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanzisha hifadhi za nyuki, manzuki na kanda za ufugaji nyuki katika mikoa ya Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Tabora, Katavi na Kigoma; kutoa pikipiki 20 kwa wasimamizi wa mradi katika Wilaya 19; kuandaa mipango ya biashara na ya usimamizi wa vituo sita (6) vya ukusanyaji, uchakataji na usindikaji vilivyowekezwa na Serikali; kuwatafutia fursa ya masoko ya nje wafanyabiashara wa mazao ya nyuki katika mikoa ya Magharibi Pemba; kutoa mafunzo kwa mafundi seremala 95 kuhusu utengenezaji wa mizinga waliopo katika maeneo ya mradi; na kuwezesha uandaaji wa Mkakati wa Ufugaji nyuki Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 fedha za nje zimetengwa.

(iv) **Mradi Na. 4816: Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio – MICE**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza kwa maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Utalii wa Mikutano na Matukio katika halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

(v) **Mradi Na. 4648: Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kusimamia Rasilimali za Misitu na Nyuki**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kujenga maabara ya mafunzo na kituo cha kuandaa malkia wa nyuki katika Chuo cha Viwanda vya Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI); na kukarabati majengo katika Chuo cha Misitu Olmotonyi. Jumla ya shilingi milioni 400 fedha za ndani zimetengwa.

(vi) **Mradi Na.4810: Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha miundominu (majengo na barabara) katika maeneo ya Hifadhi; kupima eneo na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ghala la nyara Jijini Dodoma; kununua vitendea kazi (magari, vifaa vya doria na mavazi ya Jeshi la Uhifadhi) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi. Jumla ya shilingi milioni 807 fedha za ndani zimetengwa.

**3.3.3.4.2. Tasnia ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**(a) Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukarabati wa maeneo manne (4) ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika; kukamilisha ukarabati wa jengo (*landscaping*) lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya O.A.U lililopo Jijini Dar es Salaam; ujenzi wa minara ya ukumbusho ya mashujaa wawili wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na kuadhimisha Siku ya Afrika, Siku ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika na Maadhimisho ya Siku ya Uanuai wa Utamaduni kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika. Jumla shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mikopo nafuu kwa wasanii 100 wa utamaduni na sanaa; kuendesha mafunzo kwa wasanii 1,000 na vikundi 10; na ununuzi wa vifaa na samani za Ofisi (Dar es Salaam). Jumla shilingi bilioni 3.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6521: Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa machapisho 30 kwa ajili ya kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni; kutoa mafunzo elekezi kwa

diaspora 20 wanaofundisha Kiswahili kwa wageni katika nchi mbalimbali; kuendelea kutoa mafunzo kwa Walimu wa Walimu wa Kiswahili 1,130 kuhusu namna ya kutumia Mwongozo wa Taifa wa Kufundisha Kiswahili kwa Wageni; na kuadhimisha siku ya Kiswahili Duniani. Jumla shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na.4353: Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya chuo; ununuzi wa vifaa vya kufundisha na kujifunzia; ujenzi wa studio ya kisasa za kurekodi filamu na kituo cha redio na Televisheni; kuanza ujenzi wa uzio; na kuendesha Tamasha la Kimataifa la 42 la Utamaduni na Sanaa. Jumla ya shilingi bilioni 3.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6385: Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha kukuza na kuendeleza vipaji (Akademia ya Michezo). Jumla shilingi bilioni 12.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 6503: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kusafisha eneo la ujenzi wa uwanja; na kuanza ujenzi wa uwanja. Jumla shilingi bilioni 20.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 6504: Ujenzi wa Vituo vya mazoezi na Kupumzikia Wananchi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha taratibu za manunuzi na kuanza ujenzi wa viwanja vya mazoezi na kupumzikia wananchi; na kuanza ujenzi wa Sports Arena katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Jumla shilingi bilioni 24.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 6527: Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya shule maalumu za michezo saba (7) kati ya shule 56; na kuendelea na ununuzi wa vifaa vya michezo. Jumla shilingi bilioni 2.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 6523: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuboresha kumbi za mikutano kwa kununua samani pamoja na kuweka miundombinu stahiki; kukamilisha ukarabati wa eneo la kufanyia mazoezi ya viungo (Gym) na kumpata mzabuni wa kuendesha; na kukarabati eneo la kukimbilia kwa kuweka zulia jipya (Tatan) la kisasa. Shughuli nyingine itakayotekelezwa ni ukarabati wa Viwanja saba (7) vya mpira wa miguu nchini. Jumla ya shilingi bilioni 8.0 fedha za ndani zimetengwa.

**3.3.3.4.3. Sekta ya Fedha, Biashara na Masoko**

**(a) Mradi Na. 6326: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi (Treasury Building)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati majengo, ujenzi wa nyumba moja (1) ya viongozi na ujenzi wa jengo la Ofisi za Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6388: Uboreshaji wa Miundombinu ya Mifumo ya Usimamizi wa Fedha na TEHAMA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kusimika Mfumo wa MUSE katika balozi kumi (10) na kambi 14 za TPDF; kufanya tathmini ya ubora na ufanisi wa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma (NPMIS, GAMS, TPPS, GACS, CBMS, GeFTP, GePG, MUSE na TSA Portal) pamoja na kuboresha mifumo ya ulinzi na usalama wa TEHAMA. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6550: *UNDP Support Programme***

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya mapitio ya hiari ya utekelezaji wa Ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) 2030; kuandaa mikakati ya ufadhili kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; na kuendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV 2050).

**(d) Mradi Na. 6291: Mradi wa Kuendeleza na Kuimarisha Sekta ya Fedha (Financial Sector Deepening Project)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa elimu kuhusu fursa zilizopo katika sekta ya fedha kwa maeneo ya vijijini na kwa makundi maalum (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) na kujenga uwezo wa namna ya kulinda wawekezaji katika sekta ya fedha.

**(e) Mradi Na. 6573: Mpango Kabambe wa Takwimu Tanzania (TSMP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuwezesha usimamizi wa Kamati za Sensa za Kitaifa, Mikoa, Wilaya na Mitaa; uchapishaji wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; uchoraji ramani ya GIS na Sensa; uchambuzi zaidi wa TDHS-MIS kwa kutumia matokeo ya PHC 2022; kufanya Tathmini ya Kitaifa ya WASH katika vituo vya afya (Health Care Facilities - HCFs); kuandaa mfumo wa kutathmini ubora wa Takwimu unaofuata miongozo ya IMF; kufanya utafiti wa tathmini ya watumiaji wa Takwimu nchini; usambazaji wa Takwimu ghafi (microdata) ya tafiti na sensa mbalimbali zilizofanyika tangu mwaka 2000; kufanya majaribio ya methodolojia ya EAC ya kupima umaskini nchini na utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya; na usanifu wa ramani za majengo ya takwimu yatakayojengwa Lindi, Simiyu na Pemba.

### 3.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji

#### 3.3.4.1. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji

**(a) Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuboresha na kuimarisha mfumo wa Dirisha la Pamoja la Uwekezaji (TeIW) kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa mfumo, kutunga na kuboresha sera, sheria na mikakati mbalimbali inayohusu masuala ya uwekezaji.

**(b) Kuratibu, kuhamasisha, kutangaza na kuwezesha uwekezaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuboresha mifumo ya ukusajili ili kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na Kituo; kuboresha na kuimarisha huduma zitolewazo katika Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja (One Stop Facilitation Centre) ili kufanikisha uwekezaji; kuendelea na mkakati wa kufuatilia na kutathmini miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa; kuendelea na kutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji na uanzishwaji wa benki ya ardhi; kuhamasisha uwekezaji ndani na nje ya nchi kupitia makongamano na semina; kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya uwekezaji nchini kupitia vyombo vya habari na mitandao; kutatua migogoro na changamoto za uwekezaji; kufanya tafiti za kuibua fursa za uwekezaji nchini, tafiti za kuboresha mazingira ya uwekezaji, tafiti za kuibua maeneo yenye fursa za uwekezaji; kushirikiana na Balozi za Tanzania katika kuitangaza Tanzania ili kuvutia uwekezaji ; na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**(c) Kukuza Ushiriki wa Watanzania kwenye Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji na miradi ya kimkakati pamoja na mkakati wake wa utekelezaji. Jumla ya shilingi milioni 739.00 fedha za ndani zimetengwa.

#### 3.3.4.2. Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za kiuchumi pamoja na kuwawezesha kupata mitaji kupitia mikopo yenye masharti nafuu; kukuza ujuzi na maarifa kwa wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa ili kukuza biashara zao na kuzalisha kwa tija na ubora; kuimarisha vituo vya uwezeshaji ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi kwa kujenga vituo vipya katika mikoa 11 pamoja na kufanya ukarabati wa vituo 17 vilivyoanzishwa katika mikoa 6; Kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu fursa zilizopo kutoka katika mifuko na programu za uwezeshaji katika kujikwamua kiuchumi; Kuandaa mfumo wa kidigitali wa ufuatiliaji wa utendaji wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji nchini pamoja na kukamilisha mwongozo wa usimamizi wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Jumla ya shilingi bilioni 1.99 fedha za ndani zimetengwa.

#### 3.3.4.3. Kukuza Sekta Binafsi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika miradi na programu za maendeleo nchini; kufanya tathmini ya mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi; kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta Binafsi pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji; kuanzisha kanzidata ya sekta binafsi nchini kwa lengo la kuimarisha uratibu wa taasisi za sekta binafsi nchini; kuimarisha majadiliano na mashirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi kwa kuandaa zana za kufundishia uendeshaji wa majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa wajumbe wa mabaraza ya biashara ngazi za mikoa (Regional Business Coucils – RBC) na ngazi ya wilaya (Distric Busines Coucils – DBCs) pamoja na wananchi kwa ujumla. Jumla ya shilingi milioni 474.83 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.4.4. Huduma za Biashara na Masoko

**(a) Mradi Na. 6260: Mradi wa kusaidia Taasisi**

**Uendelezaji wa Masoko ya Bidhaa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa ofisi za makao makuu ya Bodi (WRRB) jijini Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 800.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DTIF) - TANTRADE**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha soko la ndani kwa kuratibu matukio ya ukuzaji wa biashara ikiwemo maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Dar es Salaam International Trade Fair - DITF); kuboresha miundombinu ya uwanja wa Maonesho wa Mwl. J. K. Nyerere; kuendeleza mazao ya kipaumbele ikiwemo Asali, Korosho, Viungo, ngozi, mchikichi, zabibu, nyama, matunda na mbogamboga; kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya kibiashara iliyoingiwa; kutafuta fursa za masoko kwa bidhaa mbalimbali nchini hususani za viwanda; kuratibu maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya dunia ya Expo 2025 – Osaka; kuratibu misafara na ushiriki wa Maonesho katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Malawi, Falme za Kiarabu, Rwanda, Kenya, Uganda na Zimbabwe ili kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma katika soko la Kimataifa. Jumla ya shilingi bilioni 6.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa – TBS**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maabara na ofisi ya Kanda ya Kati Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Ziwa jijini Mwanza. Jumla ya shilingi bilioni 5.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Kuendeleza Biashara Kupitia Wakala wa Vipimo (WMA)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya

Wakala Mkoa wa Dodoma; na kununua *Flow Meter (3)* za kuhakiki Mita za mafuta kwenye Maghala ya mafuta na Migodini. Jumla ya shilingi bilioni 3.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Kuendeleza Biashara Kupitia Tume ya Ushindani (FCC)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki kwa ajili ya kutoa huduma zinazotolewa na FCC; kuwajengea uwezo watumishi (10) kuhusu masuala ya ushindani, kumlinda mtumiaji na mapambano dhidi ya Bidhaa Bandia; kufanya utafiti (1) kuhusu masuala ya ushindani; na kununua magari (2) kwa ajili ya kuhudumia ofisi za Kanda. Jumla ya shilingi bilioni 1.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Kuendeleza Biashara Kupitia Baraza la Ushindani (FCT)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa mfumo wa kurekodi mwenendo wa mashauri yanayosikilizwa na kutolewa maamuzi na Baraza; kujenga uelewa kwa wawekezaji, wafanyabiashara, watoa huduma, walaji (wananchi) na wadau mbalimbali kuhusu shughuli za Baraza na namna ya kulifikia Baraza; kujenga uwezo (mafunzo) kwa wajumbe na watumishi wa Baraza; kufanya tafiti (1) za kisheria na kiuchumi katika ushindani wa kibiashara na udhibiti wa soko ili kusaidia uendeshaji wa mashauri yanayowasilishwa na kutolewa katika Baraza. Jumla ya shilingi bilioni 1.84 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.4.5. Mahusiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia

**(a) Mradi Na. 6391: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Vitega Uchumi, Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukarabati wa majengo ya makazi na ofisi za Ubalozi wa Tanzania Washington D.C Marekani, Brussels (Ubelgiji), Stockholm (Sweden), Khartoum (Sudan); Pretoria (Afrika Kusini), Balozi kwenye Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania New York, Marekani; kuanza ujenzi wa majengo ya makazi ya Vitega Uchumi Ubalozi wa Tanzania Nairobi (Kenya), Ubalozi wa Tanzania Kinshasa (DRC) na Ubalozi wa Tanzania Muscat (Oman); kuanza ujenzi wa miradi 10 ya kimkakati ya ujenzi wa vitega uchumi katika Ubalozi wa Lusaka kwa kushirikiana na Serikali ya Zambia kwa utaratibu maalum; kukamilisha usanifu na ujenzi wa majengo mapya ya Makazi na Vitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Kampala (Uganda), Abuja (Nigeria), Adis Ababa (Ethiopia) na Riyadh (Saudi Arabia); na kufanya upembuzi yakinifu wa miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika Balozi 23 za kipaumbele. Jumla ya shilingi bilioni 53.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6317: Ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa miundombinu na majengo ya Bodi ya Ushauri ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu katika eneo la LakiLaki Jijini Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 20.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

**Upanuzi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni ujenzi wa vyumba vya mihadhara tisa (9) katika Chuo cha Diplomasia, Kurasini, Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 4.64 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu

#### 3.3.5.1. Afya

**Hospitali za Kitaifa**

**(a) Mradi Na. 5487: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la kutoa huduma kwa wagonjwa binafsi na wagonjwa mashuhuri. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 5491: Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba (vipandikizi (inplants revolving fund);. Jumla ya shilingi Milion 500 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la (Oncology) la kusimika vifaa vya uchunguzi wa Saratani katika kituo cha Mbeya. Jumla ya shilingi Bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5419: Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na upanuzi wa chumba cha kutakasia vifaa ili kuimarisha huduma za upasuasi wa moyo.Jumla ya shilingi Bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 5424: Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi – Kibong'oto (Kilimanjaro**)

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi na ukarabati mkubwa wa jengo la radiolojia kwa ajili ya kusimika CT Scan; kuendelea na ukarabati wa jengo la utawala; kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje na kukamilisha ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi. Jumla ya shilingi bilioni 3 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na 5425: Hospitali ya Rufaa ya Afya ya Akili - Mirembe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje. Jumla ya shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na.5445: Hospitali ya Taifa ya Mama na Mtoto - Dodoma**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa hospitali ya kibingwa na ubingwa bobezi ya Afya ya Mama na Mtoto -Nala katika mkoa wa Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 5 fedha za ndani na shilingi bilioni 11 fedha za nje zimetengwa.

**Hospitali za Rufaa za Kanda**

**(a) Mradi Na. 5426: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa, Bugando**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya kuimarisha uchunguzi na tiba ya saratani. Jumla ya shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 5427: Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba ili kuimarisha huduma. Jumla ya shilingi bilioni 1 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5422: Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za watoto-Meta. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5428: Hospitali ya Benjamin Mkapa**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la Radiotherapy na *Nuclear medicine*. Jumla ya shilingi bilioni 4 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 5408: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Burigi**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya Jengo la mama na mtoto, na vifaa. Jumla ya shilingi bilioni 10 fedha za Ndani zimetengwa

**(f) Mradi Na. 5423: Hospital ya Rufaa ya Kanda ya Kusini - Mtwara**
Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya hospitali ikiwemo ujenzi wa jengo la mama na mtoto awamu ya kwanza, sehemu ya kufulia, kichomea taka na nyumba 10 za watumishi. Jumla ya shilingi bilioni 3 fedha za Ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 5443: Hospital ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi – Kigoma**
Shughuli itakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi katika mkoa wa Kigoma. Jumla ya shilingi bilioni 10 fedha za ndani zimetengwa.

**Hospitali za Rufaa za Mikoa**

**(h) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi na ukarabati katika Hospitali za

Rufaa za Mikoa ya Katavi, Geita, Songwe, Simiyu, Shinyanga, Singida, Mwl. Nyerer Mara, Bombo, Ligula, Maweni - Kigoma,, Kitete, Sekou Toure – Mwanza, Mawenzi – Kilimanjaro,Songea, Manyara, Sokoine, Kagera, Ukerewe. Miundombinu hiyo inahusisha majengo mbalimbali kama vile ya kutolea huduma za mama na mtoto, majengo ya wagonjwa wa nje, dharura,wodi za upasuaji, radiolojia, vichomea taka na kuhifadhia maiti. Jumla ya shilingi bilioni 77.4 fedha za ndani zimetengwa.

**Tafiti na uboreshaji wa upatiakanaji wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na Vitendanishi**

**(i) Mradi Na 2208: Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMR)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kugharamia utafiti wa magonjwa ya binadamu, tiba asili na tiba mbadala, kuimarisha utengenezaji wa dawa za tiba asili na tiba mbadala na kutoa mafunzo kwa wataalam wa tiba asili na tiba mbadala. Jumla ya shilingi bilioni 1 fedha za ndani na shilingi bilioni 37 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini na ugomboaji wa dawa za msaada na kugharamia huduma za uchunguzi. Jumla ya Shilingi bilioni 200 na shilingi biioni 5 fedha za nje zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo**

Shughuli itakayotekelezwa ni: Kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kupitia huduma za chanjo pamoja na kugharamia uchangiaji gharama za chanjo zinazofadhiliwa na Shirika la GAVI (co-financing). Jumla ya shilingi bilioni 40 fedha za ndani zimetengwa na shilingi bilioni 74 fedha za nje.

**(l) Mradi Na. 5492: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma kwa watu wenye VVU na UKIMWI ili kufikia malengo ya asilimia 95 – 95– 95 (kutambua - kutumia dawa - kujikinga). Jumla ya shilingi bilioni 326.3 fedha za nje zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 5498: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuongeza huduma za kinga na kinga ya kifua kikuu kwa vituo vya msingi vya huduma ya afya; kutoa mafunzo kazini ya kuwajengea wafanyakazi uwezo wa kuongeza ufanisi wa uibuaji wa wahisiwa na utoaji wa huduma wa Kifua Kikuu (QI Mentorship); na kutoa huduma za ufuatiliaji na upimaji wa wahisiwa wa Kifua Kikuu magerezani. Jumla ya shilingi bilioni 40 fedha za nje zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 5406: Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza na Mlipuko**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko. Jumla ya shilingi bilioni 326.3 fedha za nje zimetengwa.

**(o) Kudhibiti Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya yasiyo ya kuambukiza kwa kuwekeza katika elimu kwa umma, upimaji na kujenga uwezo wa vituo vya kutolea huduma kudhibiti magonjwa hayo. Jumla ya shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa na Shilingi bilioni 326.3 fedha za nje zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 2204: Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Upanuzi, ukarabati na ujenzi wa mabweni, maabara, katika vyuo vya mafunzo ya afya, ujenzi wa maabara za kujifunzia na madarasa na kugharamia mafunzo ya uzamili. Jumla ya shilingi bilioni 15 fedha za ndani zimetengwa.

**(q) Mradi Na. 5416: Mipango ya Afya na Uendeshaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo tiba mtandao, mafunzo, utawala, usimamizi wa fedha, dawa na bidhaa zote za dawa pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji na matumizi ya takwimu za afya katika ngazi zote za hospitali, vituo vya afya na zahanati. Jumla ya shilingi milioni 301 fedha za nje zimetengwa.

**(r) Bima ya Afya kwa Wote**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kutoa elimu kuhusu dhana na utekelezaji wa sheria ya Bima ya afya kwa wote na kuweka mifumo ya utekelezaji wa mpango wa Bima kwa wote. Jumla ya shilingi milioni 121 fedha za ndani na shilingi bilioni 10 fedha za nje zimetengwa.

**(s) Mradi Na. 5401: Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hospitali 37 kwa halmashauri ambazo hazikuwa na Hospitali na ukamilishaji wa hospitali 27 za halmashauri zinazoendelea; na ukarabati wa hospitali kongwe za halmashauri 31. Jumla ya shilingi bilioni 80.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(t) Mradi Na. 5429: Huduma ya Afya ya Msingi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya vituo vya afya 185 na maboma ya zahanati 359 yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi; ujenzi wa nyumba 342 za watumishi; na ujenzi mpya wa wodi katika vituo vya afya 303.

Shughuli nyingine zitakazofanyika ni: ujenzi na ukarabati wa vituo 12 vya Afya kupitia ahadi za viongozi. Jumla ya shilingi bilioni 218.24 fedha za ndani na nje zimetengwa.

**(u) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na**

**Vitendanishi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye hospitali 127 za halmashauri, vituo vya afya 751 na zahanati 564. Jumla ya shilingi bilioni 43.75 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye hospitali 127 za halmashauri, vituo vya afya 751 na zahanati 564. Jumla ya shilingi bilioni 43.75 fedha za ndani zimetengwa.

**(w) Mradi Na. 5488: Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU); kutekeleza programu za kinga hasa utoaji wa elimu ya kujikinga na VVU na kubadili tabia; na uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF). Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii

**(a) Mradi Na. 6330: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukarabati nyumba 6 za watumishi Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale; kujenga hosteli (awamu ya pili) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 na kukarabari hosteli 5 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi; kuendelea na ujenzi wa hosteli (awamu ya tatu) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole; kujenga hosteli (awamu ya pili) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli; kujenga ukumbi wa mihadhara (awamu ya pili) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare; ujenzi wa Hosteli (awamu ya kwanza), Darasa la Kompyuta na uzio na ukarabati wa hosteli, nyumba 3 za watumishi na jengo la utawala katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha; ujenzi wa hosteli na maabara ya kompyuta katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba; na ujenzi wa jengo la utawala, ununuzi wa samani na vifaa vya TEHAMA katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Jumla ya shilingi bilioni 13.98 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6259: Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ni: kujenga uwezo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii na Wanasheria kuhusu utoaji wa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia; kutekeleza Programu ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum) kwa kufanya tathmini ya awali ya utekelezaji wa programu na kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya kizazi chenye usawa; kutekeleza afua za MTAKUWA II; kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa

wanawake wajasiriamali 75 na vikundi 35 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF); kuanzisha madawati ya jinsia 589 katika vyuo vya elimu ya juu (76), vya elimu ya kati (473) na vyuo vya Elimu ya Ufundi VETA (40); na kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya taarifa za jinsia nchini. Jumla ya shilingi bilioni 2 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanzishwa kwa Dawati la Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya watoto ndani na nje ya shule za msingi na sekondari; kuanzishwa kwa vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto katika halmashauri 185; na kuendelea kuimarisha mabaraza ya watoto kwa kuanzisha mahali ambapo hayapo na kutoa mafunzo kwa wajumbe wa mabaraza hayo kuhusu haki na ustawi wao. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5451: Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga Kituo cha Taifa cha kuhifadhi kwa muda watoto wanaopatikana wakiishi na kufanya kazi mitaani kabla ya kuunganishwa na familia zao Kigamboni, Dar es Salaam; kuendelea na ujenzi wa bweni katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara); kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu katika mahabusu ya watoto katika mikoa ya Mbeya, Arusha na Dar es salaam; ujenzi wa mahabusu ya watoto katika mkoa wa Mwanza; ujenzi wa makazi sita (6) ya kikanda ya wazee katika maeneo ya Misufini (Tanga), Ipuli (Tabora), Magugu (Manyara), Liteta Mingoyo (Lindi), Irambo (Mbeya) na Bukumbi (Mwanza); na ujenzi wa miundombinu ya mradi wa ufugaji katika makazi ya wazee Misufini (Tanga). Jumla ya shilingi bilioni 98 fedha za ndani na shilingi bilioni 6 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6290: Uchakataji wa Taarifa na Uandaaji Programu (Programming and Data Processing)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika taasisi mbili (2), vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii, makazi 14 ya wazee, Mahabusu 5 za watoto na Shule ya Maadilisho Irambo); na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Jumla ya shilingi milioni 200 fedha za ndani na shilingi milioni 273 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 6339 Ukarabati wa Nyumba za Serikali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino na kuanza ujenzi ukumbi wa madhumuni mbalimbali (multi-purpose hall), ofisi; na kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Tunguu, Mwanza, Tabora, Shinyanga, Lushoto, Arusha na Rest house Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni 13 fedha za ndani zimetengwa.

#### 3.3.5.3. Elimu

**(a) Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukusanyaji wa mikopo ya shilingi bilioni 230 kutoka kwa wanufaika wa mikopo iliyoiva; kuendelea na ugharamiaji wa mikopo ya wanafunzi 223,688 ambapo wanafunzi 72,357 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 151,331 ni wanaoendelea na masomo; kufanya ukaguzi kwa waajiri 8,000 pamoja na kuwabaini wanufaika wapya 40,000; na kutoa mikopo kwa wanufaika 640 wa *Samia Scholarship*. Jumla ya shilingi bilioni 693. 3 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6363: Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha - ATC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,200. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki - TAEC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara changamano (Arusha); na ununuzi wa samani na vifaa vya maabara. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R II)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa vyuo vitatu (3) vya Ualimu Sumbawanga, Dakawa na Mhonda na shule ya Mfano ya Sekondari Dodoma; ujenzi wa shule mpya 40, madarasa 96, mabweni manne (4), nyumba za walimu saba (7) katika shule za msingi; ujenzi wa mabweni 62, madarasa 46, maabara 16, maktaba 4, nyumba za walimu 13, mabwalo 22 katika shule za sekondari; ujenzi wa ofisi tano (5) za wathibiti ubora wa shule katika halmashauri za Njombe, Tarime, Pangani, Bunda na Ubungo; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika vyuo vya ualimu Mamire, Vikindu, Songea, Singachini na Katoke; na kuendelea na ukarabati wa shule kongwe 61 (msingi 45, Sekondari 16). Jumla ya shilingi bilioni 25.5 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuwezesha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kuchapa na kusambaza miongozo ya masomo tisa (9) hatua ya kwanza, moduli ya hatua ya Pili za masomo tisa (9) na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu 600 kutoka vituo 151 vya taasisi kuhusu Moduli za masomo tisa (9) hatua ya Pili; na kukarabati vituo sita (6) (Tabora, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Dodoma na Mwanza) na kujenga vituo vinne (4) (Lindi, Songwe, Kagera na Manyara) vya watu wazima; kuwezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kuchapa na kusambaza nakala milioni 2 za masomo manne (4) ya Hisabati, Fizikia, Kemia na Bailojia. Jumla ya shilingi bilioni 170.82 fedha za nje zimetengwa.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa shule mpya 184 za Kata; kuendelea na ujenzi wa shule mpya za sekondari 16 za bweni za mikoa; kuanza kwa ujenzi wa shule mpya 184 za kata; ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya shule mpya 300 za sekondari za kata; ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule 500 za sekondari; kuwajengea uwezo timu za uratibu wa mradi wa SEQUIP katika utekelezaji wa mradi; na kuwezesha shughuli za kuutangaza mradi wa SEQUIP kwa jamii na wadau.

**(f) Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mafunzo ya Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa halmashauri 86; na kufanya ufuatiliaji wa miundombinu ya vyoo. Jumla ya shilingi Milioni 230.0 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4315: Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu Kwa ajili ya Mabadiliko ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project - HEET)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali (mabweni, vyumba vya madarasa, maabara, kumbi za mikutano, ofisi, samani na vituo atamizi) katika vyuo Vikuu na taasisi; kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA katika vyuo na taasisi 17; Kuzijengea Uwezo Taasisi za Elimu ya Juu katika kuendeleza Mbinu za Elimu Masafa; kuwezesha mafunzo kwa wahadhiri 700 na watumishi 128 wa Serikali; kuendesha mafunzo ya muda mfupi na ya viwandani kwa wahadhiri 3,500; kuwezesha Mapitio ya Mitaala ya Elimu ya Juu na kuanzisha Mbinu bunifu za Ufundishaji; kukuza uwezo wa Utafiti na Uvumbuzi katika Taasisi za Elimu ya Juu; kuwezesha uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na kufadhili masomo kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu Binafsi 12. Jumla ya shilingi bilioni 58.0 fedha za nje zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4309: Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki (EASTRIP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ikiwemo karakana, maabara, madarasa na hosteli katika taasisi zinazotekeleza mradi (Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji); kununua na kufunga mitambo na vifaa katika karakana na maabara; kuwezesha ununuzi wa Zana, Vifaa na Mashine katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa Kilichopo Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam - DIT Kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza; kuwezesha uandaaji wa Mwongozo wa Ulinganifu wa Sifa na Tuzo za Kitaaluma Tanzania; kuwezesha Mapitio ya Miongozo ya Uandaaji wa Mitaala ya Vipaumbele katika Vituo vya Umahiri (ATC - Nishati Jadidifu, DIT Mwanza – Bidhaa za Mazao ya Ngozi, NIT – Usafirishaji, na DIT Dar es Salaam – TEHAMA); na kujengea uwezo wakufunzi 100 wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika ufundishaji na upimaji wa wanafunzi. Jumla ya shilingi bilioni 23.0 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4319: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST Primary Student Learning)**

Shughuli zitakazotekelezwa: Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3,000; kuwezesha mafunzo kwa walimu kazini katika halmashauri 50; ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA katika vituo 200 vya mafunzo ya walimu kazini; kuendelea na mpango salama wa shule katika shule 2000 na kutoa mafunzo ya usimamizi na utawala bora katika utoaji wa elimu msingi. Jumla ya shilingi bilioni 225.2 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 6350: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na upanuzi wa hosteli ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongeza ghorofa mbili (2); kuendelea na ujenzi wa maabara kuu ya kemikali itakayotumika kwa ajili ya utafiti na utoaji wa huduma za kupima sampuli za viwandani, Shule Kuu ya Uchumi na kituo cha wanafunzi; ununuzi wa samani; na kukarabati nyumba za watumishi. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 6365: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la maktaba, jengo jipya la kumbi za mihadhara; kujenga hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500; kukarabati miundombinu mbalimbali ya Chuo iliyopo Kampasi kuu ya Moshi, Taasisi ya Elimu ya Ushirika na Biashara Kizumbi (Shinyanga) na ofisi za Chuo za mikoani; na kununua samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 6345: Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na tafiti mbili (2) zenye lengo la kutatua changamoto za wananchi katika afya, kilimo na mifugo zilizopo katika vipaumbele vya tafiti vya Taifa MTUSATE; kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya ubunifu, uendelezaji wa wabunifu na kubiasharisha matokeo ya tafiti nchini; kuandaa mfumo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia (Inventory of emerging technologies); na kuimarisha uwezo wa kusimamia na kuendesha Kongano nchini. Jumla ya shilingi bilioni 4.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 6333: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala na hosteli za wanafunzi katika kampasi Kuu; ununuzi wa samani na vifaa vya kisasa vya maabara, maktaba pamoja na karakana kwa ajili ya kufundishia; kuweka nishati ya jua kama chanzo mbadala cha nishati na kufunga mfumo wa gesi katika majiko na bwalo la chakula; kuanza ujenzi wa *cafeteria* na ukarabati miundombinu mbalimbali

ya chuo. Jumla ya shilingi bilioni 4.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 6354: Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga miundombinu katika Kampasi ya Mwanza; kujenga ukuta wa mzunguko kando ya jengo la Ardhi; kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa midahalo, madarasa, maabara, studio, karakana, jengo la shahada za juu na utafiti pamoja na mabweni; kuwezesha ujenzi wa maabara yenye malengo na matumizi mbalimbali; na kuendelea na ujenzi wa jengo la ardhi (Lands Building) 'Wing A'. Jumla ya shilingi bilioni 2.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(o) Mradi Na. 6361: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – SUA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa ofisi na majengo ya taaluma katika hosteli ya Kihonda; ujenzi wa majengo mawili (2) ya taaluma yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,500, hosteli mbili (2) za wanafunzi, vibanda vya biashara katika kampasi ya Edward Moringe na Solomoni Mahlangu na ujenzi wa ukumbi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, Mnaibu na Mapumziko katika Kampasi ya MPCC; kuanzisha shamba la mbegu katika kampasi ya Edward Moringe na Solomoni Mahlangu; kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Ndaki ya Uchumi na Mafunzo ya Biashara, ujenzi wa maabara ya mafunzo ya Anatomi ya Mifugo na Teknolojia ya Wanyama na Maabara ya Bioteknolojia ya Wanyama, ujenzi wa vitalu nyumba 10 vya kupangisha kwa wahitimu, ujenzi wa jengo la Uhandisi na Ubunifu unaohusiana na TEHAMA (Innovation Hub in Engineering technologies viz.incubation of technologies) na ujenzi wa maabara na bweni katika kampasi ya Mizengo Pinda; na kuendelea na upandaji wa miti katika kituo cha mafunzo Madaba; na kuanza kwa tafiti mpya 45 na kuendelea na tafiti 120 kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuviJumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 4323: Kuendeleza Elimu ya Ualimu - TESP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga; kuendelea na uunganishwaji wa vyuo vya ualimu 15 na Mkongo wa Taifa wa Serikali; kuwezesha ununuzi wa vifaa, na mashine rahisi katika karakana 10 za vyuo vya ualimu; kuwezesha vyuo vya ualimu kujiunga na umoja wa Maktaba za tafiti na vyuo vikuu Tanzania (Consortium of Tanzania University and Research Libraries-COTUL); kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa wataalamu 50 wa maabara kuhusu utunzaji na manejimenti ya maabara za sayansi; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maabara ya lugha, sayansi na TEHAMA; na kuendelea na uandaaji wa mfumo wa usahihishaji kwa njia ya kielektroniki na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA. Jumla ya shilingi bilioni 7.0 fedha za nje zimetengwa.

**(q) Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majiko na ununuzi wa vifaa

vya karakana kwa ajili ya vyuo 20 vya maendeleo ya wananchi; kuanza kwa ufungaji wa mfumo wa gesi katika majiko kwa vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vingine 30 vya maendeleo ya wananchi. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(r) Mradi Na. 4384: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam – DIT**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kwa ujenzi wa mabweni miwili (2) Kampasi ya Mwanza yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300; na kutoa mafunzo kwa washiriki 71 kuhusu TEHAMA, Sayansi ya Maabara na Teknolojia ya Ngozi. Jumla ya shilingi bilioni 3.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(s) Mradi Na. 6364: Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Mloganzila**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa Kliniki ya Uporoto; kuendelea na ujenzi wa miundombinu (mihadhara, madarasa, ofisi za utawala na walimu) ya kufundishia Mloganzila; na kuendelea na ukarabati wa miundombinu (maabara, nyumba ya wahadhiri na mifumo ya maji na umeme). Jumla ya shilingi bilioni 4.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(t) Mradi Na. 4314: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa awamu ya pili yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500; na kuanza kwa ujenzi wa hosteli mbili (2) awamu ya pili zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300. Jumla ya shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(u) Mradi Na. 4341: Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa Mpango Kabambe kwa maeneo ya chuo yaliyopata hati miliki ikiwemo Oswald Mang'ombe Butiama (Ekari 86), Kinesi - Rorya (Ekari 95) na Kisangura- Serengeti (Ekari 136); kuendelea na ukarabati na ujenzi wa majengo ikiwemo bweni moja (1) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 katika Kampasi ya Oswald Mang'ombe; na kuendelea na ujenzi wa Ndaki moja (1) ya Kilimo na Shule kuu tatu (3) katika Kampasi Kuu ya chuo eneo la Butiama. Jumla ya shilingi milioni 500.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 4385: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa madarasa katika shule ya Msingi Mazoezi Chang'ombe na kukarabati mabweni na kumbi za mihadhara; na kuendelea kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na ujenzi wa mfumo wa ukusanyaji wa maji. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(w) Mradi Na. 4322 & 4393: Elimu msingi Bila Ada**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa elimu msingi bila ada ikijumuisha ruzuku ya uendeshaji wa shule, ruzuku ya ununuzi wa vitabu, posho ya madaraka kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na maafisa elimu kata, fidia ya ada kwa shule za bweni na kutwa na kugharamia chakula cha wanafunzi kwa shule za bweni na kutwa za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum. Jumla ya shilingi bilioni 488.53 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa 96 katika shule 32, mabweni 30 katika shule 30 za sekondari, maabara za sayansi 20 katika shule 10 za Sekondari na nyumba za walimu 60 katika shule 15 (msingi na sekondari) zenye mahitaji makubwa; kuanza ujenzi wa matundu 720 ya vyoo katika shule 30 zenye upungufu mkubwa; ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule 10 (mabweni 3, madarasa 14 na matundu ya vyoo 70); kuwezesha ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa katika elimu ya juu; na ujenzi wa maktaba tano (5) na vituo vya walimu katika shule tano (5). Jumla ya shilingi bilioni 14.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(y) Mradi Na. 4306: Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo lenye ofisi 10 na kumbi nne (4) za mihadhara katika Kampasi ya Mwanza; kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa matumizi mbalimbali na majengo matatu (3) katika Kampasi ya Bagamoyo. Jumla ya shilingi bilioni 3.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(z) Mradi Na. 4`304: Ujenzi na Ukarabati Chuo Kikuu cha Dodoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hosteli moja (1) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 152 katika kampasi ya Iringa; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara na magari manne (4); na ujenzi wa maabara ya anatomia na visima vitatu (3) vya maji; na kuendelea na ukarabati wa majengo 34, kumbi 10 za mihadhara, vyumba vya maabara na viwanja vitano (5) vya michezo. Jumla ya shilingi bilioni 3.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(aa) Mradi Na. 6353: Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala na jengo la madarasa sita (6) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,129 Kampasi Kuu; kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara na madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000, jengo la maktaba (wanafunzi 3,000), jengo la taaluma lenye madarasa mawili (2) (wanafunzi 1,000), jengo la TEHAMA, Kituo cha Kuatamia Ubunifu, bwalo la chakula (wanafunzi 900), mabweni manne (4) (wanafunzi 400); kuendelea na ukarabati wa mabweni nane (8) ya wanafunzi, Kampasi Kuu na Ndaki ya Mbeya; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa jengo la Lumumba Complex, zahanati ya Ndaki ya Mbeya na madarasa manne (4) ya kompyuta. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa

**(bb) Mradi Na. 4381: Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) ya wanafunzi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,536 pamoja na nyumba tatu (3) za wafanyakazi zenye uwezo wa kuhudumia watumishi 30 katika Kampasi ya Karume Zanzibar; kuendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 Kampasi ya Kivukoni; ujenzi wa jengo la utawala na madarasa matatu (3) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(cc) Mradi Na. 4397: Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa Ofisi ya VETA Makao Makuu jijini Dodoma na Chuo cha VETA Mkoa wa Dar es salaam Kampasi ya Kigamboni; kufanya upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya mafunzo ya Ufundi Stadi katika vyuo vya VETA Namtumbo, Kanadi (Itilima), Nyamidaho, Ileje, Simanjiro, Kihonda, Arusha, Ngorongoro, Mara, Karagwe na Lindi; kuboresha huduma na miundombinu ya Maktaba katika vyuo vya VETA vya Mikoa ya Pwani, Iringa, Tabora, Kigoma na Mbeya; kukarabati vyuo vya mafunzo vya ufundi stadi katika Mikoa Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mtwara, Njombe, Morogoro na Kigoma; na kununua vifaa na mitambo ya kujifunzia na kufundishia. Jumla ya shilingi bilioni 54.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(dd) Mradi Na. 4358: Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Afrika ya Nelson Mandela**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi litakalo hudumia wanafunzi 500, ofisi ya utawala; na ukarabati wa miundombinu mbalimbali. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(ee) Mradi Na. 6321: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa bweni la wasichana Kampasi ya Babati – Manyara na ujenzi wa Kampasi Mpya Songea (Ruvuma); na kuanza ujenzi wa madarasa na maktaba katika Kampasi ya Babati na Songea. Jumla ya shilingi bilioni ---- fedha za ndani na shilingi bilioni 14.0 fedha za nje zimetengwa.

**(ff) Mradi Na. 6322: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mabweni, madarasa na ofisi za Kampasi ya Mwanza; na kuboresha mitaala ya elimu, mifumo ya TEHAMA pamoja na ujenzi wa mabweni, maktaba, jengo la kufundishia na jengo la mihadhara katika Kampasi ya Simiyu. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 12.17 fedha za nje zimetengwa.

**(gg) Mradi Na. 6323: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa, mabweni mawili (2) na ofisi katika Kampasi ya Nyang'homango, Misungwi - Mwanza; ujenzi wa jengo la utawala, madarasa, maktaba na maabara ya kompyuta katika Kampasi ya Kigoma; kuendelea na ujenzi wa darasa, kusimika vifaa vya kieletroniki vya kufundishia na ununuzi wa gari kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini katika Kampasi ya Singida; na ujenzi wa jengo la utawala, madarasa na mabweni katika Kampasi ya Zanzibar.

**(hh) Mradi Na. 6206: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa mabweni mawili (2), ukumbi wa mihadhara, kuboresha mtaala, kuwajengea uwezo watumishi na kusimika mifumo na miundombinu ya mafunzo kwa njia ya mtandao katika Kampasi Kuu Dodoma; na ujenzi wa bweni moja (1) katika Kampasi ya Mwanza.

**(ii) Mradi Na. 6389: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala, kuwajengea uwezo watumishi na kuboresha mitaala.

**3.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**(a) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutayarisha skimu za uendelezaji maeneo ya mijini kwa majiji ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha; na kupima na kuidhinisha viwanja 300,000; kuendelea kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kwa Vijiji 975. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 Fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 2324: Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa alama za mipaka ya kimataifa kati ya Tanzania na Kenya (km 110) na kufanya utafiti kuhusu teknolojia mpya ya upimaji ndani ya maji. Jumla ya shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na 2329: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuboresha Mtandao wa Geodetic kwa kusakinisha na kufanya kazi kwa vituo 30 CORS (CORS- Continuously Operating Reference Station) katika miji ya makao makuu ya mikoa yote; kutayarisha ramani za msingi za kidijitali nchini kote; kuanzisha Mfumo wa Wavuti wa usambazaji wa habari za anga; kuwajengea uwezo wataalam wa GIS (100) kuhusu maendeleo ya National Spatial Data Infrastructure (NSDI); na kuongeza alama za upimaji 357 nchini kwa lengo la

kupunguza gharama za upimaji ardhi; na kuwezesha utekelezaji wa shughuli za mradi wa National Spatial Data Infrastructure (NSDI). Jumla ya shilingi bilioni 4.47 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4953: Uboreshaji wa Milki za Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa Ofisi za ardhi za mikoa 25 nchini; kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi 150,000; kutoa Leseni za Makazi 100,000; kuandaa na kutoa Hati Miliki 330,000 na Haki za Hati miliki za Kimila 50,000 (Certificate of Customery of Right of Occupancy (CCROs); Kuwezesha ununuzi wa vifaa vya TEHAMA (kompyuta, printa n.k) kwa ofisi 25 za mikoa na ofisi 41 za wilaya; kupima mipaka ya vijiji 50; kusimika vifaa vya kudhibiti majanga na vihatarishi kwa ajili ya mifumo ya taarifa za ardhi; kuanza ukarabati wa Ofisi za Ardhi za Halmashauri 40; na kujenga kumbi nne (4) za Mihadhara katika Chuo cha Ardhi Tabora (2) Morogoro (2). Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 156.5 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya ukarabati wa majengo matatu (3) ya Ofisi za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za Hai, Chato na Lungwe; kuendelea na ujenzi wa majengo ya maabara katika vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro (Ardhi Institute of Tabora (ARITA) na Ardhi Institute of Morogoro (ARIMO)) na kukarabati miundombinu ya ofisi ya Wizara na Mikoa (10). Jumla ya shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuwezesha utayarishaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika Vijiji 333 vilivyopo kando ya Tanzania Standard Gauge Railway (SGR) (80), The East African Crude Oil Pipeline EACOP (53), Julius Nyerere Hydroelectric Power Plant (JNHPP) (200) na Vijiji 100 vinavyokabiliwa na migogoro ya matumizi ya ardhi; maandalizi ya Mpango wa Mfumo wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya 14; kuwezesha utayarishaji wa mipango 84 ya kina ya matumizi ya ardhi na hati 25,200 za Haki ya hatimiliki ya Kimila (Certificate of Customery of Right of Occupancy (CCROs); kuwezesha kufanya ukaguzi na tathimini katika vijiji 100 vilivyofanyiwa mpango wa matumizi. Jumla ya shilingi bilioni 15.73 za fedha za ndani zimetengwa

**3.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira**

**(a) Mradi Na. 3280: Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha miradi ya maji 647 inayoendelea kutekelezwa vijijini; na kuunda, kuhuisha na kusajili Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) 640. Jumla ya shilingi bilioni 95 fedha za ndani na shilingi bilioni 350 fedha za nje zimetengwa**.**

**(b) Mradi Na. 3306: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika**

**Miji Mikuu ya Mikoa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Dodoma, Morogoro, Arusha, Shinyanga na Kigoma; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji ya Musoma, Bukoba na Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 45 fedha za ndani na shilingi bilioni 21 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha utekelezaji wa mradi wa maji Mgango – Kiabakari – Butiama (Mara); na kuanza ujenzi wa miradi ya kuboresha huduma za maji katika miji 28. Jumla ya shilingi bilioni 46.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 121.3 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 3341: Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi inayohusisha ujenzi wa chanzo na mitambo ya kusafisha maji; na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza maji katika miji ya Mwanga na Same. Jumla ya shilingi bilioni 11.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.0 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 3403: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na Miji Mingine**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya karibu na bomba kuu la maji kwenda miji ya Malampaka, Sumve na Malya; na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mkoa wa Simiyu. Jumla ya shilingi bilioni 5.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 22.0 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 3437: Kuboresha Huduma za Maji Katika Jiji la Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya usambazaji maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya Dar es Salaam na Pwani; na kujenga mitambo ya kutibu majitaka, mabomba ya kutolea majitaka kutoka maeneo ya makazi na kupelekwa kwenye mitambo ya usafishaji. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 45.0 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 3439: Mradi wa Maji wa Mpera na Kimbiji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwa wananchi umbali wa kilomita 65 katika maeneo ya Kigamboni. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani na zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 6545: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa mipango shirikishi ya

usimamizi na utumiaji wa rasilimali za maji nchini kwa kukarabati na kujenga vituo 180 vya kufuatilia mwenendo wa maji katika mito; kuhuisha na kutoa leseni 50 za uchimbaji visima maeneo mbalimbali nchini; kutoa vibali 450 vya matumizi mbalimbali ya maji; kuanzisha jumuiya 45 za watumia maji; kufanya utafiti wa maeneo ya kuchimba visima; kuweka mipaka na kutangaza vyanzo vya maji katika Gazeti la Serikali; kuanza ujenzi wa bwawa la Farkwa; kujenga mabwawa 20 ya ukubwa wa kati; na kuanza ujenzi wa majengo ya maabara za maji katika mikoa ya Dodoma, Tanga na Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 27.0 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 3435: Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufuatilia ubora wa maji kwa kukusanya na kuhakiki usalama wa sampuli za maji kutoka katika vyanzo mbalimbali vya maji na mifumo ya kusambaza maji; kuwezesha Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kuandaa Mipango ya Usalama wa Maji inayohimili mabadiliko ya Tabia nchi; kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma juu ya usimamizi wa ubora wa maji; na kuwezesha maabara nne (4) za ubora wa Maji kupata ithibati. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.5 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 3436: Ufuatiliaji na Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuratibu utekelezaji wa programu ya maji (WSDP III); na kuwezesha uratibu wa masuala ya mazingira katika sekta ya maji. Jumla ya shilingi bilioni 3.98 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.88 fedha za nje zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 3438: Mradi wa Bwawa la Kidunda**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Jumla ya shilingi bilioni 100.0 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

**(a) Programu Na 5301: Programu ya Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi**

**(i) Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia Vijijini**

Shughuli zitakazotekelezwa: Kuendelea na uchimbaji wa visima virefu viwili katika Halmashauri za Mpwapwa (1) na Mvomero (1); kuendelea na uchimbaji wa malambo matatu katika Halmashauri za Kishapu (2) na Mpwapwa (1); kuendelea na ujenzi wa kiwanda kidogo cha bidhaa za ngozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na ujenzi wa kituo cha kukusanyia maziwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha huduma za mifugo katika Halmashauri ya

Wilaya ya Mpwapwa. Jumla ya shilingi bilioni 6.63 fedha za nje zimetengwa.

**(ii) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo wa Ikolojia, Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai Tanzania.**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa mafunzo maalum kwa maafisa ngazi ya kitaifa () na mabonde kuhusu uanzishwaji na usimamizi wa miradi ya SLR; kuandaa na kusambaza nyenzo za mawasiliano kuhusu masuala ya SLR, katika usimamizi wa mabonde pamoja na kutoa uzoefu wa nchi nyingine; kuandaa mafunzo kuimarisha kikosi kazi cha kitaifa cha SLR; kuwezesha maafisa ugani kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji kupitia mashamba darasa; kutoa mafunzo kwa watumishi wa halmashauri kutoka maeneo ya mradi kuhusu nyenzo za ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mazingira na nyenzo za ufuatiliaji za tija na uhimilivu wa kilimo; kuandaa na kusambaza bidhaa za maarifa (knowledge products), kuandaa mwongozo wa kushirikisha umma na sekta binafsi katika mfumo wa uzalishaji unaohusiana na urejeshaji wa mazingira; . Jumla ya shilingi bilioni 6.74 fedha za nje zimetengwa.

**(iii) Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa malambo (2) na ukarabati lambo moja (1), mfumo mmoja wa uvunaji wa maji, ujenzi wa mabirika matatu (3) ya kunyweshea mifugo na ujenzi wa mashojo mawili (2) katika Halmashauri ya Magu; kuwezesha ujenzi na kukarabati malambo (3) na ujenzi wa bwawa moja (1), mifumo miwili (2) ya uvunaji wa maji ya mvua, ujenzi wa mabirika manne (4) ya kunyweshea mifugo na ujenzi josho moja (1) na ukarabati wa mashojo mawili (2) katika Halmashauri ya Nzega; na Kuwezesha ujenzi na kukarabati mabwawa manne (4) na malambo mawili (2), mifumo miwili ya uvunaji wa maji ya mvua, ujenzi wa mabirika matano (5) ya kunyweshea mifugo na ujenzi na ukarabati wa mashojo matano (5) na kukabarati moja (1) katika Halmashauri ya Mkalama. Jumla ya shilingi bilioni 4.31 fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi ili Kupunguza Hewa Ukaa Inayosababishwa na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha kanuni za Biashara ya Kaboni kwa upande wa Zanzibar; kufanya mapitio ya mkakati wa kupunguza hewa ukaa inayosababishwa na ukataji na uharibifu wa misitu nchini wa mwaka 2013. Jumla ya shilingi milioni 500.0 fedha za nje zimetengwa.

**(v) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni:kutoa mafunzo kwa makundi ya wavuvi katika Halmashauri za Kyela, Ludewa na Nyasa; kutoa mafunzo na kuwezesha wanavikundi (375) kuhusu kilimo cha biashara ya miti katika halmashauri

zinazotekeleza mradi; na kuwezesha mafunzo kwa wanavikundi (75) kwa kubadilishana uzoefu kwa kutembeleana katika maeneo wanayofanya shughuli zao. Jumla ya shilingi milioni 501.57 fedha za nje zimetengwa.

**(vi) Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa kingo za fukwe katika Mwambao wa Sipwese Pemba na Mikindani - Mtwara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa kuta za bahari katika maeneo ya Mikindani Mtwara (mita 1,750) na Sipwese Pemba (mita 500). Jumla ya shilingi billioni 4.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

**Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa kanuni tano (5) na miongozo mitano (5) ya usimamizi wa hifadhi ya mazingira; kuanzisha mfumo wa utoaji leseni na vibali; kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mazingira; kuandaa mpango na mkakati wa kitaifa wa usimamizi wa taka; kutoa mafunzo kwa mamlaka mbalimbali kuhusu dhana za uhifadhi wa mazingira; kuandaa mpango wa usimamizi wa mazingira katika halmashauri moja; kuanzisha jukwaa la kitaifa la usimamizi wa mazingira ili kubadilishana uzoefu wa masuala ya mazingira; kununua vitendea kazi kwa ajili ya mradi; na kuendesha shughuli za usimamizi wa mradi. Jumla ya shilingi billioni 2.58 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5305: Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga vituo vitatu vya kuchambua taka zinazorejelezeka katika Manispaa za Kigamboni na Ubungo; na kumuwezesha mtaalam elekezi kukusanya, kuhifadhi na kuteketeza mafuta ya transfoma zilizobainika kuwa na kiwango kikubwa cha kemikali ya PCBs kwa njia salama. Jumla ya shilingi milioni 281.41 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5304: Kudhibiti Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa mafunzo kwa maafisa forodha (200) na wasimamizi wa sheria (100) kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali zinazomong’onyoa tabaka la ozoni; kuwezesha vyuo vyenye fani ya viyoyozi na majokofu kwa utoaji wa vifaa, teknolojia na utaalam; kutoa mafunzo kwa maafisa ugavi 30 kutoka wizara za kisekta; kutoa mafunzo kwa mafundi 300 wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna bora ya kuhudumia vifaa hivyo kwa kutumia kemikali pasipo kuharibu tabaka la ozoni; na kujenga uelewa kwa walaji wa mwisho na wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya teknolojia na kemikali mbadala wa kemikali; Jumla ya shilingi 356.46 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6309: Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa makazi ya Mhe. Makamu wa Rais Kilimani (Dodoma) na Oysterbay (Dar es salaam); na ukarabati jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais kwenye eneo la Luthuli II (Dar es Salaam). Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.5.7. Hifadhi na Kinga ya Jamii

**(a) Mradi Na. 6575: Kuimarisha uwezo wa kujiandaa na kukabili Maafa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuzijengea uwezo Kamati tano (5) za Usimamizi wa Maafa na waratibu wa maafa katika Mikoa mitano; kuandaa na kutekeleza mkakati wa utafutaji wa rasilimali kwa ajili kukabiliana na dharura za Maafa; kuandaa mipango ya kuzuia na kujiandaa na maafa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati; kutekeleza mpango wa kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya maafa; na kuratibu shughuli za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kupitia Mfuko wa Maafa. Jumla ya shilingi bilioni 2.55 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

**Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa Nchini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa kituo cha Usimamizi wa Maafa Nzuguni (Dodoma) ambao unahusisha ujenzi wa jengo la utawala, jengo la operesheni na mawasiliano ya dharura, kituo cha matangazo kwa umma na uzio. Jumla ya shilingi bilioni 3.75 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao (National Rehabilitation Centre)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao (National Rehabilitation Centre) cha waraibu wa dawa za kulevya eneo la Itega, Dodoma, ujenzi wa karakana mbili (2), ujenzi wa jiko na ukumbi wa chakula, ujenzi wa mabweni mawili (2) na ujenzi wa Ofisi za Wakufunzi; na ununuzi wa vifaa na samani. Jumla ya shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5488: Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (WAVIU); kutekeleza programu za kinga hasa utoaji wa elimu ya kujikinga na VVU na kubadili tabia; na uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF). Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6220: Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na utambuzi na uhakiki kwa walengwa

walioboresha hali zao na utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini ambazo hazikufikiwa; kuendelea na uhawilishaji fedha kwa kaya maskini zisizo na uwezo wa kufanya kazi; kuendelea na utoaji wa ajira za muda kwa kaya maskini zenye uwezo wa kufanya kazi; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuboresha miundombinu; kuendelea Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na upanuzi wa mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya kielektroniki; na kuendelea na uundaji na Usimamizi wa mifumo ya uendeshaji wa mpango. Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani na bilioni 60.0 fedha za nje zimetengwa.

### 3.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu

#### 3.3.6.1. Ujuzi na Uwezeshaji

**(a) Mradi Na. 6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kufanya Utafiti wa Kitaifa wa nguvu kazi (National Manpower Survey) na kutoa viashiria muhimu vya Soko la Ajira nchini; Kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa njia ya Uanagenzi (Apprenticeship) kwa vijana 10,000; kuwezesha Mafunzo ya Uzoefu wa Kazi (Internship) kwa wahitimu 10,000 wa elimu ya juu na ya kati kupitia waajiri wa Sekta Binafsi na Umma; kutoa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kwa Watanzania 10,000; na kuwaunganisha watanzania 10,000 na fursa za ajira nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 36.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana vilivyokidhi vigezo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (Youth Development Fund – YDF); na kutoa mafunzo kwa wakopaji na wasimamizi wa Mfumo wa Maendeleo ya vijana. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6205: Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutoa elimu kuhusu Sera ya Maendeleo ya vijana na kuisambaza kwa wadau; kuendelea kutoa mafunzo ya *soft skills* kwa vijana 500 pamoja na kununua vifaa kwa ajili ya kuwawezesha kufanya shughuli za uzalishaji mali; kuandaa na kuratibu Programu ya Kitaifa ya vijana ya kuzalisha fursa za ajira nchini; Kukamilisha Mwongozo wa upimaji Tija katika sekta mbalimbali za uzalishaji na huduma; kutoa mafunzo ya ufundi stadi na huduma za marekebisho kwa Vijana wenye ulemavu 800 kupitia vyuo vya Sabasaba – Singida, Yombo – Dar es Salaam, Luanzari – Tabora, Mirongo – Mwanza na Masiwani – Tanga; na kufanya kampeni ya upimaji na utoaji wa viungo bandia kwa Watu wenye Ulemavu wapatao 300. Jumla ya shilingi bilioni 1.3 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4954: Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuviwezesha vyuo vitano (5) vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu ambavyo ni Sabasaba – Singida, Yombo - Dar es Salaam, Luanzari – Tabora, Masiwani – Tanga na Mirongo – Mwanza kwa kuwapatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia, gharama ya kuendesha vyuo ikiwemo kulipa umeme, maji, usafi, chakula pamoja na malazi; kukarabati vyuo vinne (4) vya

Ufundi Stadi na Huduma za Utengamao kwa Watu Wenye Ulemavu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Singida na Tabora; na Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vinne (4) vya watu wenye ulemavu katika maeneo ya Songwe,Kigoma, Ruvuma na Mwanza mtawalia. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

### 3.3.7. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Katika mwaka 2023/24 shilingi bilioni 10.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: ufanikishaji wa maandalizi ya miradi ya PPP; kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali katika kuandaa miradi ya PPP; kujenga uwezo wa maafisa wanaosimamia miradi ya PPP nchini; kuzijengea uwezo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa miradi ya PPP; na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya ubia kwa njia ya VGF.

Aidha, shughuli mahsusi zitakazotekelezwa katika baadhi ya miradi mbalimbali ya PPP ni pamoja na:

(i) Kuanza ujenzi wa barabara ya Morogoro – Dodoma yenye urefu wa km 256 kwa utaratibu wa PPP;
(ii) Kuendelea na mchakato wa ununuzi wa mbia wa miradi ya ujenzi wa viwanda vya dawa muhimu na vifaa tiba itakayotekelezwa chini ya Bohari ya Dawa (MSD) katika mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya;
(iii) Kuendelea na majadiliano ya mkataba wa kuwezesha utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza;
(iv) Kuendelea na hatua ya ununuzi wa mbia wa miradi ya Hoteli ya Nyota Nne na Jengo la Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
(v) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza kwa hatua ya ununuzi wa mbia wa mradi wa ujenzi wa hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam;
(vi) Kuendelea na maandalizi ya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Kampasi za Dar es Salaam na Mbeya;
(vii) Kuanza hatua ya ununuzi wa mbia wa mradi wa kuimarisha huduma za saratani nchini kwa kujenga kituo cha ubingwa bobezi wa tiba ya saratani eneo la Mloganzila (*Ultra- Modern Oncology Centre* - UMOC) na Kituo cha Saratani Mbeya (Mbeya *Cancer Centre* - MCC) eneo la Iwambi - Mbeya chini ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI);
(viii) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa barabara ya tozo kutoka Kibaha-Mlandizi – Chalinze - Morogoro (205 km) na kuanza taratibu za ununuzi;
(ix) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa awali na kuanza na upembuzi yakinifu wa mradi wa barabara ya tozo Mbeya By - pass (Uyole – Sogwe 48.9km);
(x) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa ukaguzi wa lazima kwa vyombo

vya moto na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mbia; na

(xi) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa awali na kuanza upembuzi yakinifu wa kina wa mradi wa ujenzi wa kituo cha mazoezi tiba Mbweni Dar es Salaam chini ya Taasisi ya Mifupa ya MOI.

**3.3.8. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuweka mfumo madhubuti wa ukusanyaji mapato, kusimamia matumizi; kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye mikataba ya utendaji kazi ili kuhakikisha Uwekezaji wa Serikali unakuwa na tija zaidi; na kufanya tathmini ya kina kwenye maeneo yaliyobinafsishwa ili kubainisha faida na changamoto kwa wawekezaji pamoja na upande wa Serikali.

# SURA YA NNE

## UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2023/24

### 4.1. Utangulizi

Sura hii inaainisha mikakati ambayo Serikali itachukua ili kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali vinafikiwa katika ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Katika kutekeleza vipaumbele vilivyopo katika Mpango, Serikali itahakikisha inatenga rasilimali fedha za kutosha za kugharamia Mpango ili kufikia malengo yaliyowekwa.

### 4.2. Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2023/24

Katika mwaka 2023/24 Serikali inatarajia kutenga shilingi bilioni 15,156.0 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 34.1 ya bajeti ya mwaka 2023/24. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 11,873.9 sawa na asilimia 78.3 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,282.1 sawa na asilimia 21.7 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Fedha hizi zitakusanywa kutoka mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada na mikopo nafuu, mikopo ya ndani na mikopo ya nje yenye masharti ya biashara.

### 4.3. Mikakati ya Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Mpango kwa Mwaka 2023/24

Katika kugharamia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24, vyanzo vya mapato vitakavyotumika ni mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, mikopo na misaada pamoja na vyanzo mbadala vya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo.

### 4.4. Mapato ya Ndani

#### 4.4.1. Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi

Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani ili kuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wateja wanadai risiti wanaponunua bidhaa;

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa mlipakodi kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, semina na warsha;

(iii) Kupanua wigo wa kodi kwa kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi kupitia kampeni ya Mlango kwa Mlango;

(iv) Kuendelea kutumia Mpango wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Compliance Risk Management Plan) ili kubaini na kutambua wakwepaji wa

kodi;

(v) Kuimarisha ushirikiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na vyombo vya ulinzi na usalama nchini ili kudhibiti bidhaa za magendo na tatizo la ukwepaji wa kodi katika mipaka yote ya Tanzania;

(vi) Kuimarisha mazingira rafiki ya ulipaji kodi kwa hiari kwa kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo itakayosaidia kurahisisha ulipaji kodi;

(vii) Kuhamasisha ulipaji kodi katika sekta isiyo rasmi kwa kuijumuisha kwenye mfumo rasmi wa ulipaji kodi;

(viii) Kurasimisha shughuli zisizo rasmi zikiwemo shughuli za wajasiriamali wadogo kwa kuwatengea maeneo maalum;

(ix) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wapya, kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kuongeza wigo wa kodi;

(x) Kufanya tafiti katika maeneo mapya ambayo yanaweza kuwa vyanzo vya utozaji kodi;

(xi) Kuimarisha usimamizi wa tozo na ada mbalimbali ili kuhakikisha zinakusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(xii) Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kufuatilia Mizigo inayokwenda nchi jirani (Eletronic Cargo Tracking System) ili kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mizigo inayopita kwenda nchi jirani;

(xiii) Kuendelea kusimamia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway- GePG) ili kurahisisha ulipaji na kudhibiti upotevu wa mapato;

(xiv) Kuimarisha mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki la Uondoshaji wa Mizigo Bandarini (e-Single Window System) ili kurahisisha uondoshwaji wa mizigo katika vituo vya mipakani pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini;

(xv) Kuimarisha na kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (Integrated Domestic Revenue Administration System - IDRAS) utakaounganisha mifumo yote ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali ili kuimarisha usimamizi wa mapato yatokanayo na kodi za ndani nchini;

(xvi) Kuboresha Mfumo wa mawasiliano kati ya NIDA na TRA ili kurahisisha usajili na ufuatiliaji wa walipakodi; na

(xvii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati.

## 4.5. Mikopo na Misaada

### 4.5.1. Mikopo ya Nje

Serikali itaendelea na majadiliano na Taasisi mbalimbali za nje ya nchi ili kuhakikisha kiasi cha mikopo ya nje kilichopangwa kwa mwaka 2023/24 kinafikiwa. Aidha, Serikali itaendelea kuchukua jitihada za kuongeza ukusanyaji wa mapato ya

ndani na kukamilisha zoezi la nchi kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa madeni katika mwaka 2022/23 kwa lengo la kuongeza wigo wa wakopeshaji hususan katika masoko ya mitaji ya kimataifa. Sanjari na hilo, Serikali itaendelea kujikita kwenye Mkakati wa Usimamizi wa Madeni wa Muda wa Kati 2022/23-2024/25 (Medium Term Debt Strategy-MTDS) kwa kukopa zaidi mikopo yenye masharti nafuu na kuziba pengo la upungufu utakaojitokeza kwa kukopa mikopo yenye masharti ya kati kwa utaratibu wa udhamini kutoka taasisi za udhamini wa mikopo (*Export Credit Agencies - ECAs*), ambayo masharti yake yana unafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara.

### 4.5.2. Mikopo ya Ndani

Katika mwaka 2023/24, Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani kupitia hatifungani za Serikali kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa kati wa Usimamizi wa Madeni 2022/23-2024/25. Vilevile, katika muda wa kati, Serikali itatumia hatifungani za muda mrefu na mfupi ili kupunguza gharama na viatarishi kwenye deni la Serikali. Serikali itaendelea na mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kiasi kilichopangwa kukopwa katika soko la ndani kinapatikana bila kuathiri ukopaji wa sekta binafsi na kuongeza ushindani. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu zaidi kwa nchi wanachama wa SADC na watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora) ili waweze kuwekeza katika dhamana za Serikali.

### 4.5.3. Misaada ya Nje

Ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo utaendelea kuimarika kwa kutekeleza kikamilifu Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework – DCF) pamoja na Mpango Kazi wake. Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa *D-Fund Management Information System*. Aidha, Serikali itaendelea kuibua miradi na kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo.

## 4.6. Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo

Katika kuongeza wigo wa vyanzo vya fedha za kugharamia miradi ya maendeleo (hususan miradi inayozalisha mapato na kuweza kutekelezwa kibiashara), Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kupitia njia Mbadala. Njia hizo zinajumuisha: Hatifungani za Manispaa (Municipal Bonds); Hatifungani ya Miundombinu (Infrastructure Bond); Hatifungani ya Buluu (Blue Bond); Hatifungani za Kampuni (Corporate Bond); Dhamana za Muda wa Kati; Hatifungani ya Mazingira (Green Bonds); Hatifungani ya Kiislam (SUKUK); *Micro-Saving Bond na Lease Financing*; mitaji ya muda mrefu kupitia utaratibu wa *leveraging*; bima na ugharamiaji hatarishi (risk financing).

Katika kuimarisha matumizi ya vyanzo mbadala na bunifu vya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikijumuisha: kuundwa kwa *National Facilitation Team*; kutolewa mafunzo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma ambazo zimewasilisha miradi ambayo itatekelezwa kwa utaratibu wa vyanzo mbadala na bunifu na kuendelea na maandalizi ya Mwongozo wa kuanzisha *Special Purpose Vehicles* zitakazosimamia miradi inayogharamiwa na vyanzo mbadala na bunifu. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Vile vile, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuandaa maandiko ya miradi inayoweza kutekelezwa kwa njia mbadala (Alternative Project Financing-APF).

# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

## 5.1. Utangulizi

Ufuatiliaji na Tathmini (U&T) ni nyenzo muhimu ya kuiwezesha Serikali kupima hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa kulinganisha malengo na vipaumbele vilivyowekwa ili kufanya maamuzi yanayoongozwa na uwepo wa taarifa sahihi na kwa wakati. U&T pia husaidia kupima mwelekeo wa kufikia malengo na matokeo tarajiwa yaliyowekwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26). Kwa msingi huo, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 kupitia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma; Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha; Waraka Na. 5 wa Hazina wa Mwaka 2020/21 Kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); na Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti.

Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa utafanyika katika ngazi mbalimbali ambapo katika kila ngazi itaandaliwa taarifa ambayo itawasilishwa kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo baina ya watekelezaji na waratibu wa miradi na programu za maendeleo. Taarifa hizo zitajumuisha: taarifa za utekelezaji wa miradi za kila robo mwaka; na taarifa za ufuatiliaji na tathmini. Taarifa za ufuatiliaji na Tathmini ziandaliwe kwa kuzingatia viashiria vilivyowekwa katika mfumo madhubuti au bangokitita la mradi (Logframe) na kuziwasilisha kila mwezi kupitia NPMIS. Aidha, watekelezaji wote wa miradi ya maendeleo wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya Waraka Na. 5 wa Hazina wa mwaka 2020/21 kuhusu NPMIS.

## 5.2. Misingi na Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina wajibu wa kuzingatia maelekezo kuhusu misingi na mbinu kama zilivyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo *(National Monitoring and Evaluation Framework)* wa Mwaka 2022. Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini utawezesha kupatikana kwa taarifa za utekelezaji kwa lengo la kuwezesha watunga sera, wafanya maamuzi na wadau muhimu kufahamu mwenendo wa utekelezaji mipango, miradi na programu za maendeleo kwa kuainisha hatua iliyofikia pamoja na mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa malengo.

### 5.3. Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo yatasaidia kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafaniko, kuainisha changamoto na mapendekezo ya kuzitatua. Aidha, taasisi zote zinazofanya ufuatiliaji na tathmini zinaelekezwa kutoa mrejesho baada ya kufanya ufuatiliaji kwa wadau wote wanaohusika na utekelezaji miradi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyobainishwa.

### 5.4. Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ikiwa ni pamoja na: mawanda na malengo ya mradi, hali ya utekelezaji, taarifa za ugharamiaji, taarifa za mikataba, changamoto na mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, muundo wa Taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Miaka Mitano utatolewa na Idara ya Mipango ya Kitaifa na kujadiliwa na wadau kila mwaka. Vilevile, muundo wa Taarifa hiyo utajielekeza kufanya uchambuzi wa matokeo tarajiwa yaliyoainishwa katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Miaka Mitano.

### 5.5. Mgawanyo wa Majukumu

Ufuatiliaji na Tathmini ni suala mtambuka kwa sababu linahusisha wadau mbalimballi katika ngazi tofauti. Ushirikishwaji wa wadau muhimu katika kufanikisha ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango ni suala la msingi na la kipaumbele kwa Serikali. Aidha, mgawanyo wa majukumu umefafanuliwa vyema katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo ambao umeainisha wadau mbalimbali na majukumu yao mahsusi katika ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha ufasaha na ufanisi unazingatiwa katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi unafuatiliwa na kufanyiwa tathmini ipasavyo. Kwa upande wa kufuatilia matokeo yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Miaka Mitano, mgawanyo wa majukumu umeainishwa katika Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Miaka Mitano. Ufuatiliaji huo utafanyika kwa kutumia uchambuzi wa kina juu ya matokeo tarajiwa kupitia tafiti na takwimu zilizozalishwa na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

# SURA YA SITA

# VIHATARISHI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

## 6.1. Utangulizi

Malengo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 yanaweza yasifikiwe kama ilivyopangwa ikiwa vihatarishi na mikakati ya kukabiliana navyo haitabainishwa na kutekelezwa sanjari kupitia mipango ya Serikali. Vihatarishi vinaweza kusababisha mradi kutotekelezwa, kutekelezwa chini ya kiwango, kuongezeka gharama au kutokamilika kwa wakati. Ili kuhakikisha malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 yanafikiwa kwa ufanisi, Mpango huu umezingatia Mwongozo wa Kuandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma wa Mwaka 2012, ambapo Serikali itahakikisha utekelezaji wa Mpango unaenda sambamba na utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Aidha, vihatarishi vinavyoweza kuukabili Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 vimegawanyika katika makundi makuu mawili (2). Makundi hayo ni vihatarishi vya ndani vitakavyotokana na utendaji au mifumo ya Serikali na vihatarishi vya nje vitakavyotokana na masuala yaliyoko nje ya udhibiti wa Serikali.

## 6.2. Vihatarishi vya Ndani na Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

**Vihatarishi vya Ndani:** Hivi ni vihatarishi ambavyo nchi ina uwezo wa kuvizuia kutokea. Vihatarishi hivyo ni pamoja na: Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya maendeleo; upotevu wa mapato ya Serikali yanayotokana na biashara mtandao; mabadiliko ya viwango vya riba katika soko la fedha la ndani; uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za binadamu; vitendo vya rushwa na ubadhilifu wa rasilimali. Serikali ina uwezo wa kudhibiti kutokea au kukabili athari za vihatarishi hivi kupitia utekelezaji wa mikakati iliyowekwa.

**Vihatarishi vya Nje:** Hivi ni vihatarishi ambavyo nchi haina uwezo wa kuvizuia kutokea. Vihatarishi hivyo ni pamoja na: Mabadiliko ya tabia ya nchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; Mdororo na Mitikisiko ya Kiuchumi duniani; kuongezeka kwa kiwango cha riba katika masoko ya kimataifa; Migogoro na hali ya siasa inayojitokeza kwa nchi jirani, kikanda na kimataifa; na Kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia. Mikakati ya kukabiliana na vitaharishi hivi ipo ndani ya uwezo wa Serikali. Serikali haina udhibiti wa kutokea kwa vihatarishi bali ina uwezo wa kupunguza athari zitakazosababishwa kupitia utekelezaji wa mikakati iliyowekwa. Uchambuzi wa vihatarishi vya ndani na nje pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo umeainishwa katika **Jedwali Na. 6.1 (a)** na **Jedwali Na. 6.1 (b).**

**Jedwali 6.1 (a): Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | (i) Kutokutekelezwa kwa mradi au kutekelezwa kwa kasi ndogo na hivyo kutokamilika kwa wakati;<br>(ii) Kuongezeka kwa gharama za mradi; na<br>(iii) Kuchelewa kwa upatikanaji wa huduma zilizotarajiwa. | (i) Kuimarisha sera za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ikiwemo kuhakikisha kila mfanyabiashara anatoa risiti ya kielektroniki anapouza na mnunuzi anadai risiti anaponunua bidhaa au huduma;<br>(ii) Kuongeza wigo wa walipa kodi kwa kuhamasisha sekta isiyo rasmi kujumuishwa katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi;<br>(iii) Kudhibiti upotevu wa mapato kwa kusimamia ipasavyo mifumo ya ukusanyaji, ikiwemo Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway - GePG);<br>(iv) Kutekeleza miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP;<br>(v) Kuimarisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye kuongeza mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;<br>(vi) Kuimarisha sekta ya fedha na kuendeleza soko la fedha la ndani *(domestic debt market)* ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo; |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | | (vii) Kupata fedha kupitia mikopo yenye masharti nafuu; na<br>(viii) Matumizi ya Vyanzo Mbadala na bunifu vya utekelezaji wa mradi. |
| 2. | Ushiriki mdogo wa Sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya maendeleo | (i) Uwekezaji mdogo wa Sekta binafsi katika miradi ya kimkakati; na<br>(ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi kutokana na uhaba wa mitaji, teknolojia na mazingira duni ya kufanya biashara; | (i) Kufanya majadiliano na Sekta binafsi ili kuweka mikakati ya kutatua changamoto zinazowakabili;<br>(ii) Kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ili kuvutia uwekezaji katika maeneo yanayofaa kwa Sekta binafsi;<br>(iii) Kuendelea kuandaa miundombinu wezeshi katika maeneo mapya ya uwekezaji; na<br>(iv) Kuziwezesha kifedha taasisi za Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi ya PPP na kuiuza kwa Sekta Binafsi kwa ajili ya uwekezaji. |
| 3. | Upotevu wa mapato ya Serikali yanayotokana na biashara ya mtandaoni | (i) Kupungua kwa mapato ya Serikali; na<br>(ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo | (i) Kuongeza matumizi ya kidigitali katika ukusanyaji wa kodi; na<br>(ii) Kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuboresha usimamizi wa mifumo ya kisheria iliyopo. |
| 4. | Mabadiliko ya viwango vya riba katika soko la | (i) Kuongezeka kwa matumizi ya malipo ya riba na nakisi ya bajeti; | (i) Kuendelea kutekeleza Sera za fedha zitakazowezesha |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | fedha | (ii) Serikali kutumia fedha kutoka kwenye vifungu vingine vya bajeti kugharamia malipo ya riba; na<br>(iii) Sekta binafsi kutofikia malengo ya mikopo na hivyo kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kusababisha Serikali kukosa mapato. | viwango vya riba kuwa himilivu;<br>(ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ili kupunguza utegemezi katika misaada na mikopo kutoka nje; na<br>(iii) Kuimarisha soko la fedha la ndani. |
| 5. | Uharibifu wa Mazingira kutokana na shughuli za binadamu. | (i) Kubadilika kwa hali ya hewa na kusababisha uharibifu wa miundombinu kutokana na mvua nyingi;<br>(ii) Kutoweka kwa bioanuai;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za utoaji wa huduma za afya kutokana na kuongezeka kwa magonjwa yanayotokana na uharibifu wa mazingira;<br>(iv) Kuongezeka kwa gharama za kurejesha mazingira katika hali ya awali na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa; na<br>(v) Kupungua kwa uzalishaji wa mazao na bidhaa viwandani. | (i) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira ili kudhibiti uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu;<br>(ii) Kuhamasisha wananchi kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.<br>(iii) Kudhibiti uharibifu wa uoto wa asili na bioanuai;<br>(iv) Kuimarisha usimamizi wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji na misitu; na<br>(v) Kutekeleza ipasavyo miongozo na kanuni za usimamizi wa mazingira. |
| 6. | Vitendo vya rushwa na ubadhilifu wa rasilimali | (i) Upotevu wa fedha za umma;<br>(ii) Miradi kutekelezwa chini ya kiwango;<br>(iii) Kuongezeka kwa muda na gharama za utekelezaji wa miradi; na<br>(iv) Kasi ndogo ya ukuaji wa | (i) Kuimarisha utekelezaji wa sheria ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wanaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa;<br>(ii) Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya Maendeleo. | miradi;<br>(iii) Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara yaliyoboreshwa na yenye uwazi ili kuruhusu sekta binafsi kushamiri na kurasimisha sekta isiyo rasmi; na<br>(iv) Kuimarisha mfumo wa utoaji motisha kwa watoaji taarifa zinazohusiana na rushwa. |
| 7. | Uhalifu wa kimtandao wa mifumo ya Serikali | (i) Kuharibiwa kwa mifumo ya kielektroniki ya Serikali; na<br>(ii) Upotevu wa mapato na taarifa. | (i) Kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Udhibiti wa Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma;<br>(ii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo ya taarifa ya kielektroniki ya Serikali; na<br>(iii) Kuimarisha usalama wa maeneo ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali (Data recovery sites). |

**Jedwali 6.1 (b): Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko | (i) Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi;<br>(ii) Kuathiri mapato ikiwemo mapato ya kodi yatokanayo na kipato;<br>(iii) Raslimali fedha kuelekezwa kukabiliana na majanga badala ya kuelekezwa | (i) Kuboresha mifumo ya kuzuia na kukabiliana na majanga;<br>(ii) Kuimarisha mifuko ya maafa;<br>(iii) Kutekeleza na kuendelea kuridhia itifaki za kimataifa |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | kwenye miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa;<br>(iv) Kuathiri ikolojia | kuhusu utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; na<br>(iv) Kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021. |
| 2. | Mtikisiko na Mdororo wa uchumi duniani | (i) Kuathirika kwa mikopo na misaada kutoka kwa washirika wa Maendeleo;<br>(ii) Kukosekana kwa masoko ya uhakika ya bidhaa nje ya nchi;<br>(iii) Kupungua kwa uwekezaji kutoka nje ya nchi; na<br>(iv) Kuongezeka kwa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia zikiwemo bidhaa za mafuta, malighafi na bidhaa za viwandani. | (i) Kuimarisha mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi duniani;<br>(ii) Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini; na<br>(iii) Kuimarisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuhimili ushindani katika masoko ya kimataifa. |
| 3. | Migogoro na hali ya siasa isiyo imara ya nchi jirani, kikanda na kimataifa. | (i) Kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu katika soko la dunia kama bidhaa za petroli, mafuta ya kula, vyakula, mashine na mitambo;<br>(ii) Kupungua kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi hususan inayotumia vifaa kutoka nje;<br>(iv) Kupungua kwa uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja;<br>(v) Kupungua kwa mikopo na misaada kutoka nje; na<br>(vi) Kukosekana kwa masoko | (i) Kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia na malighafi za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje; na<br>(ii) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi Jirani, kikanda na kimataifa ili kukuza masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa viwandani. |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | nje ya nchi kwa ajili ya kuuza bidhaa zinazozalishwa nchini. | |
| 4. | Kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia | (i) Mifumo ya kisheria, kisera, na kitaasisi iliyopo kutoendana na mabadiliko ya teknolojia hivyo kuongezeka kwa gharama za uwekezaji katika mifumo ya teknolojia mpya; na<br>(ii) Kupungua kwa uwezo wa kiushindani katika soko la kikanda na kimataifa. | (i) Kuendelea kuboresha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi ili iendane na mabadiliko ya teknolojia duniani; na<br>(ii) Kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza ujuzi, uhawilishaji wa teknolojia na kuhamasisha ubunifu wa teknolojia kwa wataalam wa ndani. |
| 5. | Wadau wa maendeleo kutotekeleza ahadi kwa wakati na kiwango kilichoahidiwa | Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi. | Kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. |

**Kiambatisho A: Miradi Iliyofuatiliwa katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2022/23**

| NA | JINA LA MRADI | MAHALI |
|---|---|---|
| 1. | Mradi Wa Kuzalisha Umeme Kwa Kutumia Maji Wa Julius Nyerere - Mw 2,115 | Pwani |
| 2. | Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Katikwa Kiwango Cha Kimataifa (SGR) | Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza |
| 3. | Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP) | Tabora |
| 4. | Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi (Km 3.2) na Barabara Unganishi (Km 1.66) | Mwanza |
| 5. | Mradi Kufufua Shirika La Ndege Tanzania (ATCL) | Dar es Salaam |
| 6. | Ujenzi wa Kiwanda na Uendelezajiwa Shamba la Miwa Mkulazi – Mbigiri Estate | Morogoro |
| 7. | Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) - Awamu ya II | Dar es Salaam |
| 8. | Ujenzi Wa Bandari ya Uvuvi Kilwa | Lindi |
| 9. | Mradi wa Maji Suguti/Kusenyi - Kwikonero | Mara |
| 10. | Mradi wa Maji Iramba | Mara |
| 11. | Mradi wa Maji Kenyana- Nyamitita | Mara |
| 12. | Mradi wa Maji Bunda | Mara |
| 13. | Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara | Mara |
| 14. | Barabara ya Nyamuswa – Bulamba (km 56.4) | Mara |
| 15. | Ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Butiama | Mara |
| 16. | Ujenzi wa Jengo la Utawala Tarime Mji | Mara |
| 17. | Mradi wa kuboresha hospitali ya rufaa Mkoa wa Mara - KWANGWA | Mara |
| 18. | Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Musoma | Mara |
| 19. | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A – Tarime | Mara |
| 20. | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A – Rorya | Mara |
| 21. | Ujenzi wa Soko la Kisasa Tarime | Mara |
| 22. | Ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama ya wilaya ya Butiama | Mara |
| 23. | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Simiyu cha Ngazi ya B | Simiyu |
| 24. | Mradi wa Maji Nyamalapa | Simiyu |

| NA | JINA LA MRADI | MAHALI |
|---|---|---|
| 25. | Mradi wa maji Mkula | Simiyu |
| 26. | Mradi wa Maji Ngulyati – Nyamswa | Simiyu |
| 27. | Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Maji - Maswa | Simiyu |
| 28. | Barabara ya Maswa Bypass (km 11.3) | Simiyu |
| 29. | Mradi wa Barabara ya Mwigumbi - Maswa (km 50.3) | Simiyu |
| 30. | Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa Biashara Sekondari (EP4R) | Simiyu |
| 31. | Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa Bariadi Sekondari (EP4R) | Simiyu |
| 32. | Kiwanda cha kuzalisha chaki | Simiyu |
| 33. | Kudhibiti Sumukuvu - Simiyu | Simiyu |
| 34. | Mradi wa maji Msandamuungano | Rukwa |
| 35. | Mradi wa ujenzi wa bwawa la maji Ikozi | Rukwa |
| 36. | Ujenzi wa bwawa la maji kijiji cha Kalepula | Rukwa |
| 37. | Ujenzi wa bwawa la maji Kilewani | Rukwa |
| 38. | Mradi wa maji Matai Mradi wa maji Isale | Rukwa |
| 39. | Mradi wa maji Matala | Rukwa |
| 40. | Mradi wa maji Kasu | Rukwa |
| 41. | Hospitali ya wilaya ya Sumbawanga – Mtowisa | Rukwa |
| 42. | Mradi wa maji Muze Group | Rukwa |
| 43. | Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga (km 112) | Rukwa |
| 44. | Mradi wa usambazaji wa umeme vijijini (Awamu ya Pili ya Mradi wa REA III) | Rukwa |
| 45. | Ujenzi wa bwawa la maji kijiji cha Nsenkwa | Katavi |
| 46. | Mradi wa maji Shankala | Katavi |
| 47. | Mradi wa maji Kanoge II | |
| 48. | Mradi wa maji kijiji cha Vikonge | Katavi |
| 49. | Ununuzi wa Rada | Katavi |
| 50. | Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Katavi | Katavi |
| 51. | Mradi wa ujenzi wa bweni la wasichana shule ya Sitalike | Katavi |
| 52. | Mahakama ya Wilaya Tanganyika | Katavi |
| 53. | Uboreshaji wa hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Sumbawanga | Katavi |
| 54. | Mradi wa usimamizi Rasilimali Madini | Katavi |
| 55. | Mradi wa maji Ruvumachini | Ruvuma |
| 56. | Mradi wa maji Mangamao | Ruvuma |
| 57. | Mradi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mputa | Ruvuma |
| 58. | Usimamizi endelevu wa Rasilimali za Madini – | Ruvuma |

| NA | JINA LA MRADI | MAHALI |
|---|---|---|
| | SMMRP kwenye kituo cha umahiri Songea | |
| 59. | Chuo cha maendeleo ya Wananchi – Mbinga | Ruvuma |
| 60. | Mradi wa Maji Liuli Group | Ruvuma |
| 61. | Mradi wa ujenzi wa ghala la kudhibiti Sumukuvu | Ruvuma |
| 62. | Mradi wa Maji Mabuni | Ruvuma |
| 63. | Ujenzi wa Barabara Mbinga - Mbamba Bay kwa kiwango cha lami (km 66) | Ruvuma |
| 64. | Ujenzi wa barabara ya Kitai - Lituhi kwa kiwango cha lami (km 84.5) | Ruvuma |
| 65. | Mradi wa ukarabati na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Songea | Ruvuma |
| 66. | Mradi wa kuongeza thamani kwa mazao ya misitu – FORVAC (Ruvuma) | Ruvuma |
| 67. | Mradi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Njombe | Njombe |
| 68. | Mradi wa maji kijiji cha Nyombo | Njombe |
| 69. | Mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Njombe | Njombe |
| 70. | Mradi wa Maji Kibena Howard | Njombe |
| 71. | Mradi wa Maji Igula | Njombe |
| 72. | Mradi wa maji Idende – Unenamwa | |
| 73. | Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe Awamu ya Pili | Njombe |
| 74. | Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4) kwenye kipande Moronga – Makete (km 53.5) | Njombe |
| 75. | Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Njombe | Njombe |
| 76. | Mradi wa Maji Mkutano | Lindi |
| 77. | Barabara ya Nachingwea-Ruangwa-Nanganga (106km): Lot 2: Ruangwa - Nanganga (Km 53,2) | Lindi |
| 78. | Ujenzi wa Mradi wa Maji Mchangani | Lindi |
| 79. | Mradi wa Maji Makanjiro – Ruangwa | Lindi |
| 80. | Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mkoa wa Lindi | Lindi |
| 81. | Mradi wa Maji Kiwawa | Lindi |
| 82. | Mradi wa Maji Marendego | Lindi |
| 83. | Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Lindi | Lindi |
| 84. | Ujenzi wa Ghala na Miundombinu Nanyumbu | Mtwara |
| 85. | Ujenzi na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Mtwara | Mtwara |
| 86. | Mradi wa Maji – Chemchem | Mtwara |
| 87. | Mradi wa Maji Namanjele – Njumbuli | Mtwara |

| NA | JINA LA MRADI | MAHALI |
|---|---|---|
| 88. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mkunwa | Mtwara |
| 89. | Mradi wa Maji Mkululu | Mtwara |
| 90. | Mradi wa Maji Kilombero | Mtwara |
| 91. | Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano Likombe | Mtwara |
| 92. | Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) | Mtwara |
| 93. | Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara | Mtwara |
| 94. | Mradi wa Chujio la Maji | Mtwara |
| 95. | Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Mtwara | Mtwara |
| 96. | Mradi wa Maji Namatunu | Mtwara |
| 97. | ETC Cargo Limited | Dar es Salaam |
| 98. | Mradi wa Chuma Ghafi na Makaa ya Maganga Matitu na mgodi wa Katewaka | Njombe |
| 99. | Mradi wa Mchuchuma na Chuma – Liganga | Njombe |
| 100. | Mradi wa Makaa ya mawe Ngaka | Ruvuma |
| 101. | Mradi wa shamba la mpira – Kalunga, | Morogoro |
| 102. | Mradi wa Magadi Soda katika bonde la Engaruka | Manyara |
| 103. | Shamba la Mpira – Kihuhwi | Tanga |
| 104. | Kiwanda cha kutengeneza matairi (GTEA) | Arusha |
| 105. | Mradi wa majengo - Dar es Salaam | Dar es Salaam |
| 106. | Kiwanda cha kutengeneza vifungashio (Global Packaging Ltd) | Pwani |
| 107. | Mradi wa kuunganisha magari | Pwani |
| 108. | Kiwanda cha Hester Bioscience Africa | Dar es Salaam |
| 109. | Kiwanda cha viuadudu - Tanzania biotech products Limited | Pwani |
| 110. | Mradi wa kuunganisha matrekta ya URSUS | Pwani |
| 111. | Kiwanda cha Nyanza Glass | Mwanza |
| 112. | Kiwanda cha Mashine na Vipuri (KMTC) | Kilimanjaro |